# Nipashe

Jumanne Mei 14, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579917

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Ndugai aibana Serikali kusitisha ujenzi wa bandari ya Bagamoyo

UKURASA 2







UKURASA 13

# Mvua yaleta maafa


• **Watoto** wawili wafa, maeneo mengi yazingirwa na maji, TMA yaonya mvua zaidi zinakuja... *Endelea ukurasa wa 2*



Watumiaji wa barabara ya Morogoro wakivushwa na guta kwa malipo ya Sh. 500 na Sh. 1,000 kwa pikipiki katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam jana kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wakenya wamtafuta Rais wao mtandaoni

UKURASA 25



## Shamim Mwasha, mumewe wafikishwa mahakamani

UKURASA 2

**MICHEZO** ZAHERA: HURUMA SASA BASI UK.32 | MAONI, KATUNI UK.6

# Mafuriko yaleta maafa Dar

**Na Waandishi Wetu**

WATOTO wawili wamepoteza maisha kutokana na athari za mvua kubwa za masika zinazoendelea kunyesha katika jiji la Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema tukio la kwanza lilitokea Mei 8, mwaka huu, saa 9:00 alasiri maeneo ya Goba wilayani Kinondoni.

Alimtaja mtoto aliyefariki dunia ni Francis Byabato (6), baada ya kutumbukia kwenye kisima cha futi 30 kilichokuwa wazi nyumbani kwao.

Alieleza kuwa mtoto huyo alitoweka kwa siku mbili na baadaye alikutwa ndani ya kisima hicho akiwa ameshafariki dunia.

Kamanda Mambosasa alisema mtoto mwingine ambaye anakadiriwa kuwa na umri wa miaka (4-5), alifariki dunia Mei 12, mwaka huu maeneo ya Mongo la Ndege.

Alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa ukielea katika Mto Msimbazi ukiwa hauna jeraha lolote na umehifadhiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Kadhalika, alisema, mvua hizo zinazoendelea kunyesha zimesababisha uharibifu wa baadhi ya majengo ya Shule ya Msingi Mwale iliyopo Kiwalani, Majani ya Chai Kiwalani na Shule ya Sekondari Kibasila iliyopo Manispaa ya Temeke ambayo imejaa maji na kusababisha kushindwa kuendelea na masomo.

Kamanda Mambosasa alitaja madhara mengine ni kufungwa kwa baadhi ya barabara za jiji hilo ikiwamo barabara ya Morogoro katika eneo la Jangwani.

TMA YAZUNGUMZA

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema mvua kubwa za masika zitaendelea hadi Jumamosi.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Uhusiano wa TMA, Monica Mutoni, alisema kwa mujibu utabiri uliotolewa kuanzia Jumapili mvua hizo zitaendelea hadi Jumamosi.

Alisema mvua hizo zitaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema pia mvua hizo zitaambatana na upepo mkali na mawimbi makubwa kwa baadhi ya maeneo ya Ukanda wa Pwani.

"Watu wajiandae kwa sababu kuna uwezekano wa kutokea kwa wastani kiwango cha athari zinazoweza tokea kama maji kuzunguka nyumba, uchelewaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa shughuli za uchumi na kijamii na kutawanyishwa na kupeperushwa kwa takataka mitaani," alieleza katika taarifa hiyo.

Alitaja madhara mengine ni kuanguka

INAENDELEA UK 8



Watumiaji wa barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam, wakivushwa na guta kwa malipo ya Sh. 500 na pikipiki kwa Sh. 1,000 katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam kufuatia mvua kubwa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shamim Mwasha, mumewe wafikishwa mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MMILIKI wa blogu ya 8020 Fashion, Shamim Mwasha (41) na mumewe, Abdul Nsembo (45), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride zenye uzito wa gramu 232.70.

Wanafamilia hao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali, Costastine Kakula.

Kakula alidai kuwa washtakiwa hao, wakazi wa Mbezi Beach, wanatuhumiwa kwa shtaka moja la kusafirisha dawa za kulevya.

Alidai kuwa Mei mosi, mwaka huu, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wanatuhumiwa kusafirisha dawa hizo kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi. Kakula alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi, Hajra Mungula, aliomba upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka ili hatua nyingine iweze kuendelea licha ya kwamba jana ndiyo siku ya kwanza kwa kesi hiyo kusomwa mahakamani hapo.

Hakimu Mhina alisema shtaka lao ni la uhujumu uchumi, mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hadi upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu, kitengo cha uhujumu uchumi yenye mamlaka ya kuisikiliza.

Alisema kesi hiyo itatajwa Mei 27, mwaka huuu, na kuangalia kama upelelezi umekamilika au la.

Washtakiwa wanaendelea kukaa mahabusu mpaka siku ya kwenda tena mahakamani.

# Ndugai aibana Serikali kusitisha ujenzi bandari ya Bagamoyo

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

KUSITISHWA kwa mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo mkoani Pwani jana kulizuia mjadala mkali bungeni huku Spika Job Ndugai akiitaka serikali kulieleza Bunge sababu za kusitishwa kwa mradi huo.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa agizo hilo bungeni jijini Dodoma jana baada ya wabunge wa pande zote mbili kuhoji kuhusu kusitishwa kwa mradi huo wa bandari walipochangia hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya mwaka ujao wa fedha.

Hotuba hiyo iliwasilishwa bungeni Alhamisi na Waziri Isack Kamwelwe, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 4.963 kwa ajili ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Ndugai alisema anaamini kukamiika kwa mradi huo wa ujenzi wa bandari kutakuwa na tija kubwa kwa nchi, akieleza kuwa bila bandari bora, hata ujenzi unaoendelea wa reli ya kisasa (SGR) hautakuwa na maana

"Yaani bora tungeanza na bandari hii ya kisasa kabisa, tukaja reli," Spika Ndugai alisema huku akishangiliwa na wabunge wa pande zote mbili.

Alisema kukamilika kwa mradi wa reli ya kisasa bila kuwa na bandari ya kisasa kama hiyo iliyopangwa kujengwa Bagamoyo, ni kazi bure kwa kwa kuwa mpaka sasa, nchi haina bandari nzuri na hivyo serikali inapaswa kuliangalia kwa kina suala hilo.

Spika Ndugai alimtaka Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Kamwelwe), kulitolea ufafanuzi suala hilo baadaye jana jioni wakati wa kuhitimisha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara yake.

"Sifahamu kipi kimekwamisha mradi wa Bagamoyo. Waziri akipata muda anaweza kutufafanulia vizuri hapa. Niliwahi kwenda China kwenye Jiji la Shenzhen, nikiwa na baadhi ya wabunge tulipata nafasi ya kukutana na waliokuwa wakitaka kujenga Bandari ya Bagamoyo walitufanyia uwasilishaji wa mradi huo.

"Ukiusikiliza huwezi kuacha kuunga mkono Bandari ya Bagamoyo. Wachina walitueleza sijui kwanini Watanzania mnapofikia jambo kubwa kama hili mnavuta miguu, hamuamui," Spika Ndugai alisema.

Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa (CCM), alikuwa miongoni mwa wabunge waliohoji kuhusu kusitishwa kwa mchakato wa utekelezaji wa mradi huo, akimwomba Spika Ndugai kuunda kamati ya kwenda kuchunguza suala hilo ili kile alichokiita ukweli wa mkwamo wa ujenzi kijulikane na Bunge litekeleze wajibu wake wa kuishauri vyema serikali.

Wabunge wengine walihoji kuhusu kusitishwa kwa mradi huo ni pamoja na wa CCM; Charles Tizeba (Buchosa), Dk. Shukuru Kawambwa (Bagamoyo), Hawa Ghasia (Mtwara Vijijini), Mussa Zungu (Ilala) na Hussein Bashe (Nzega Mjini). Wengine ni Lucy Magereli (Viti Maalum-Chadema) na Ally Saleh (Malindi - CUF).

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA

# Mwili wa mtu aliyekufa wazua taharuki Mwanza

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

TAHARUKI imewakumba wakazi wa Jiji la Mwanza jana asubuhi baada ya kukuta mwanamume anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka kati ya 25 na 30 akiwa amefariki dunia na mwili wake ukiwa barabarani nje ya hoteli.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna Muliro Jumanne, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa Jeshi la Polisi bado linaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha kifo hicho huku akikanusha taarifa zilizoenea awali kuwa mtu huyo alijirusha kutoka ghorofani.

"Tumepata hizi taarifa majira ya saa 3:30 asubuhi kwamba maeneo ya Gold Crest, hoteli ambayo ipo katika ya Jiji la Mwanza kuna mtu amefariki dunia baada ya kujirusha, tumefika kwenye eneo la tukio, baada ya kukagua uchunguzi wa awali unaonyesha kwamba taarifa zile za awali hazikuwa za kweli," alisema na kuongeza:

"Kwa sababu ukiangalia mwili wa mtu ambaye amefariki na ukiangalia umbali wa sehemu ambayo ilikuwa inazungumziwa kwamba amejirusha, haiingii akilini kwamba mtu anaweza akajirusha kutoka umbali ule akafika chini akawa mgongo wake mzima, miguu mizima na kichwa kizima hakuna hata tone la damu."

Kamanda Muliro alisema kuwa kwa kutumia tu uchunguzi wa awali wa kawaida hata kama mtu ambaye hakusomea upelelezi anaweza akabaini kuwa zile zilikuwa habari za kufikirika na kuwa habari kuwa mtu huyo amejirusha kutoka kwenye ghorofa si za kweli.

Shuhuda wa tukio hilo Neli Edward, alisema kuwa tukio hilo limewashangaza kutokana na kuwa mtu anadaiwa kujirusha kutoka ghorofani anaonekana mwili wake kutokuwa na jeraha lolote na kuiomba serikali ifanye uchunguzi wa tukio hilo.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (Mb.), akila kiapo cha utii mbele ya Bunge la Afrika Mashariki kama Waziri anayeshughulikia masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutoka Tanzania. Tukio hilo ambalo limefanyika kwenye Makao Makuu ya Bunge la Afrika Mashariki jijiji Arusha jana, limeshuhudiwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro na Spika wa Bunge hilo Martin Ngoga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vifaa upimaji dengue Dar vyasambazwa

**Na Mary Geofrey**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile, amesema wameshasambaza vitendanishi vya maabara kwa ajili ya ugonjwa wa homa ya dengue katika hospitali zote za Serikali jijini humo.

Jiji la Dar es Salaam lina wagonjwa zaidi ya 1,200 ambao wameshabainika kuwa na homa hiyo ya dengue, hivyo vifaa hivyo vitasaidia kupunguza gharama za upimaji kutoka Sh. 65,000 hadi Sh. 15,000.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk Ndugile, alisema kuwapo kwa vipimo hivyo kumerahisisha huduma ya upimaji wa homa hiyo kutokana na awali wananchi walikuwa wakitumia fedha nyingi katika hospitali binafsi.

"Tayari katika hospitali zote za Serikali za mkoa huu tumeshasambaza vitendanishi vya maabara kwa ajili ya kupima homa ya dengue. Sasa wagonjwa watapata huduma bila ya usumbufu kwa gharama nafuu kabisa," alisema Dk. Ndugile.

Alisema vipimo hivyo vinapatikana katika hospitali za Mwananyamala, Ilala, Temeke, vijibweni na Mnazi Mmoja.

Kuhusu wagonjwa waliopo katika hospitali za binafsi, Dk. Ndugile alisema, wanaweza kupata huduma ya vipimo kwa bei nafuu endapo wataenda kutibiwa katika hospitali za Serikali.

"Lakini hatuwezi kwenda kuwalazimisha kwenda kutibiwa katika hospitali za umma," alieleza Dk. Ndugile.

Naye Dk. Ford Chisongela, kutoka ofisi ya mganga mkuu wa mkoa, akizungumza na kituo kimoja cha redio cha jijini Dar es Salam jana, alisema mbu wanaoambukiza ugongwa wa dengue hupenda kuzaliana katika mikoa yenye joto ndio sababu ya kuwapo Dar es Salaam na Tanga.

Alisema pia Mbu hao wanatabia ya kuruka umbali mdogo, hivyo hushambulia maeneo ya miguu zaidi, lakini wanatoa tahadhari watu kujikinga maeneo yote ya mwili.

Dk. Chisongela alisema, mbu hao pia hushambulia wakati wa mchana na huathiri watu wa rika zote hasa watoto wadogo.

Alisema awali katika mkoa wa Dar es Salaam, vituo vya kutoa huduma vilikuwa vichache ndio sababu watu kushindwa kubaini ugonjwa huo kwa haraka.

Alisema baada ya kusambazwa vitendanishi hivyo wagonjwa wengi watapata fursa ya kupata vipimo.

Alisisitiza kuwa, wagonjwa wanaofika hospitali hawapimi ugongwa huo moja kwa moja, isipokuwa daktari atakavyomsikiliza mgonjwa atamshauri upime homa hiyo kwa sababu si kila homa ni dengue.

Alitahadharisha kuwa, ugonjwa huo hauna dawa na hivyo moja ya athari yake ni kupunguza kiwango cha maji yanayozunguka mwilini na kuharibu figo na ndio sababu wamekuwa wakishauri mwenye dalili hizo kunywa maji mengi.

"Watu wanaougua homa na dengue wanashauriwa kunywa maji mengi ili kuongeza maji mwili na kupunguza kasi ya kukaushwa na homa hiyo," alisema Dk. Chisongela.

Mwishoni mwa wiki Naibu Waziri wa Afya, Dk.Faustine Ndugulile, alisema kuwa vitendanishi vya maabara vya kupima homa ya dengue, viliwasili nchini na tayari kwa kusambazwa katika vituo vilivyotengwa kufuatilia ugonjwa huo.

"Tumeleta vipimo vya maabara vya kutosha na vingine vipo njiani na sasa bei imeshuka itakuwa kati ya Sh. 15,000 mpaka Sh. 20,000," alisema Dk Ndugulile.

Tangu Januari hadi sasa, wananchi wamekuwa wakitumia kati ya Sh. 40,000 hadi Sh. 65,000 katika hospitali binafsi kupima virusi vya homa hiyo ambayo hadi sasa waliothibitika kuugua wamefikia 1,237 kutoka jijini Dar es Salaam na Tanga, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Homa ya dengue ni ugonjwa wa kitropiki unaosababishwa na virusi maarufu kama dengue. Homa ya dengue pia hujulikana kama, homa ya kuvunja mifupa kwa sababu inaweza kuwafanya watu wawe na maumivu makali hadi wahisi kama mifupa yao inavunjika.

Dalili za ugonjwa huu huanza siku tatu hadi kumi na nne baada ya kuambukizwa.

Baadhi ya dalili ni homa kali, kuumwa na kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungio.

Kwa watu wachache, homa ya dengue inaweza kubadilika na kuwa aina zinazohatarisha maisha.

Dalili kubwa ni ile ya kuvuja damu, ambayo huifanya mishipa ya damu inayobeba damu kupasuka.

Kwa kawaida matibabu huchukua siku tatu hadi saba hadi mgonjwa kupona na hakuna dawa ya chanjo inayofanya kazi kuwakinga watu dhidi ya virusi vya dengue.

# Habari njema wateja wa benki ya FBME

**Peter Haule na Josephine Majura, DODOMA**

SERIKALI inafanya mazungumzo na Serikali ya Cyprus ili kutatua changamoto za malipo kwa wateja walioweka amana zao katika Benki ya FBME ambayo ilifutiwa leseni ya kufanya shughuli za kibenki hapa nchini na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Hayo yalisemwa bungeni jana jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum, Asha Abdullah Juma, aliyeuliza kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali kuwasaidia wananchi walioweka amana zao katika Benki ya FBME.

Dk. Kijaji alisema kuwa kazi ya kukusanya mali na fedha zilizokuwa za Benki ya FBME katika taasisi mbalimbali za fedha hasa zilizopo nje ya nchi, imekumbwa na changamoto za kisheria kati ya Tanzania na Cyprus ambako benki ya FBME ilikuwa ikiendesha sehemu kubwa ya biashara zake hivyo kusababisha ucheleweshaji wa ukusanyaji na ugawaji wa fedha na ufilisi.

"Hakuna tarehe rasmi ya kuanza kulipa fedha kwa sasa kutokana na uwapo wa kesi zinazokwamisha zoezi la ukusanyaji mali na madeni ya Benki ya FBME," alieleza Dk. Kijaji (pichani).

Alisema Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 inaeleza kuwa amana au akiba za wateja katika benki au taasisi zina kinga ya bima ya amana ya kiasi kisichozidi Sh. milioni 1.5, na iwapo mteja ana salio la amana la kiasi kisichozidi Sh. 1.5 atapata fidia ya asilimia 100.

Aidha, alisema wateja walio na zaidi ya Sh. milioni 1.5 wanalipwa Sh. milioni 1.5 kama fidia ya bima ya amana na kiasi kinachobakia kinalipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi.

Hata hivyo, alisema malipo kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi yanategemea makusanyo ya fedha kutoka kwenye mauzo ya mali pamoja na fedha zilizowekwa na benki katika taasisi mbalimbali za fedha za ndani na nje ya nchi.



## HABARI KITAIFA

# Sangoma, mke wa mmiliki shule mbaroni mauaji mtoto

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SAKATA la mauaji ya mtoto Rose Japhet (6), mkazi wa Kijiji cha Msewe wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya, linalowahusisha baba wa mtoto huyo Japhet Nguku (37) na mmiliki wa Shule ya Sekondari ya Ushindi iliyopo Mbalizi, Anganile Mwamburuma (43), limechukua sura mpya baada watu wengine wawili akiwamo sangoma kunaswa.

Akizungumza na wandishi wa jana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ulrich Matei, alimtaja mganga wa Jadi aliyekamatwa ni Meja Sanga maarufu kwa jina la 'Mwakipande' au 'Mesia' (48), mkazi wa Makete mkoani Njombe.

Alisema sangoma huyo ndiye aliyekuwa anatakiwa kupelekewa viungo vya marehemu ikiwamo kanyagio la mguu wa kulia na ndipo wauaji wakaamua kufanya unyama huo. Kamanda Matei alimtaja mhusika mwingine kuwa ni mke wa mmiliki wa shule, Agatha ambaye anadaiwa kuwa mara ya mwisho marehemu alilala nyumbani kwake na hivyo anasadikika kuwa anajua kilichotendeka.

"Lakini pia kwenye nyumba ya Agatha ambaye ni nyumba ndogo (mke mdogo) wa Anganile tulizikuta baadhi ya nguo za marehemu ambazo zilibaki na kwa taarifa za awali ni kwamba mara ya mwisho mtoto alilala kwake hivyo lazima anajua siri," alisema Kamanda Matei.

Aidha Kamanda Matei alisema katika upekuzi zaidi walilikuta sime (panga) kwenye moja ya nyumba za Mwamburuma (mmiliki wa shule) ambalo linasadikika kuwa lilitumika kwenye mauaji ya mtoto huyo.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema awali wahusika wakuu ambao ni baba mzazi wa marehemu na mmiliki wa shule ya Ushindi walifahamiana miaka 20 iliyopita na kwamba walikutana kwa mganga ambako walienda kutibiwa.

Alisema Japhet alitibiwa kwa mganga huyo na akakosa fedha za kulipa gharama za matibabu akabaki kwa mganga huyo kwa ajili ya kufanya kazi ili aweze kulipa gharama za matibabu yake na ndipo alipofahamiana.

Hata hivyo alisema licha ya taarifa za awali kuonyesha kuwa marehemu alikuwa amekatwa kanyagio la mguu wa kulia pekee, lakini walipoukuta mwili ukiwa umetelekezwa kwenye Msitu wa Hifadhi wa Chimala wilayani Mbarali walibaini kuwa pia wauaji walimkata kiganja cha mkono wa kushoto ambacho mpaka sasa hakijulikani kilipo.

Kamanda Matei aliwaomba waganga wa jadi pamoja na machifu wa Mkoa wa Mbeya kuwafichua waganga wa jadi wanaohusika na mauaji ya watoto ili vitendo hivyo vidhibitiwe.

Awali watuhumiwa wawili ambao ni Japhet Nguku na Andrew Mwamburuma walikamatwa wakidaiwa kushiriki kumuua mtoto Rose na kumkata kanyagio la mguu wa kulia kwa lengo la kupeleka kwa mganga wa jadi ili kutengeneza dawa ya biashara.

Ilidaiwa kuwa Japhet alikubaliana na Mwamburuma kuuziana mtoto kwa Sh.milioni tano ili auawe na kukatwa viungo vyake kwa ajili ya kwenda navyo kwa mganga wa jadi kutengeneza ndagu (dawa ya biashara). Mwamburuma anadaiwa kuwa alikuwa anataka dawa kwa ajili ya kuendesha biashara ya shule ambayo anaimiliki na inadaiwa kuwa na wanafunzi wa chache hivyo alikuwa anataka waongezeke.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa, Mzee Mkongea Ali, akizindua mradi wa maji safi na salama ambao utatumiwa na wananchi wa Kata ya Masekelo na Ndala Shinyanga Mjini na kuwaondolea adha ya kutumia maji machafu. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Kortini kufanyakazi nchini bila kibali Uhamiaji

**Na Hellen Mwango**

WALIMU watano wakiwamo raia wa Kenya, wanne wa shule ya msingi na sekondari ya Kings wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na shtaka la kufanya kazi nchini bila ya kuwa na kibali.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni, Esrom Maina (45), Ruth Njuguna (30), Joseph Kuria (30), Charles Sakawa (32) na Mtanzania Stella Bizulu (44).

Nguka alidai kuwa kati ya Septemba 2018 na Machi 18, mwaka huu, katika shule ya msingi na sekondari ya Kings iliyoko eneo la Goba, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao raia wa Kenya walikutwa wakifanya kazi ya ualimu katika shule hiyo bila ya kuwa na kibali kutoka Idara ya Uhamiaji.

Katika shtaka la pili imedaiwa siku na mahali hapo mshtakiwa Bizulu, akiwa kama meneja wa shule hiyo, aliwaajiri walimu hao bila ya kuwa na kibali cha kufanya kazi nchini kutoka Uhamiaji.

Hata hivyo, washtakiwa hao wamekana mashtaka hayo na wameachiwa kwa dhamana hadi leo wakati upande wa mashtaka unatarajiwa kufanyia mabadiliko hati ya mashtaka.






## W'biashara wa China waonyeshwa fursa

**Novatus Makunga, ARUSHA**

WAFANYABIASHARA wa China wametakiwa kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya chakula kwa kutumia malighafi inayopatikana nchini ili kutosheleza mahitaji ya soko ifikapo mwaka 2050 ambapo inakadiriwa asilimia 50 ya watu barani Afrika watakuwa wamekimbilia maeneo ya mijini.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, wakati akifungua kongamano la uwekezaji kati ya China na Tanzania katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), jana.

Kairuki alisema kuwa mahitaji ya chakula yatakuwa makubwa kutokana na ongezeko kubwa la watu wanaokimbia uchumi wa vijijini wa kilimo na kwenda mijini kutafuta kazi za viwandani na huduma.

Alisema Tanzania ina ardhi nzuri yenye rutuba pamoja na maji ya kutosha, hivyo kuwezesha uzalishaji wa mazao yanayotumiwa sana na jamii barani Afrika kama vile nafaka, maharage, mihogo, viazi vitamu na matunda ya aina mbalimbali yakiwamo maparachichi.

"Tanzania ina kila kitu na hamtahitaji kuleta mazao kutoka nje kwani kwa ardhi iliyopo na maji kuna uwezekano mkubwa wa kulisha kwa chakula majirani zetu kutokana na mahitaji yaliyopo," alifafanua.

Aidha, Kairuki alisema fursa nyingine ni usindikaji wa nyama pamoja na samaki ambapo alibainisha kuwa kuna mahitaji makubwa sana kwa soko la nchi za Asia.

"Lazima uwekezaji wenu ujikite katika viwanda, lakini kubwa kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini," alisema.

Kairuki alisema mpaka sasa Tanzania ina soko la uhakika kutokana na kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yenye watu milioni 152 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yenye watu milioni 800.

Akizungumzia biashara kati ya China na Tanzania, Kairuki alisema imekua kutoka dola za Marekani bilioni 3.9 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 7 kwa mwaka jana.

Alifafanua kwamba kuongezeka kwa kasi kwa biashara na uwekezaji kutachangia katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Alisema uchumi wa Tanzania hivi sasa unakua kwa kasi ikiwa ya nchi ya tano katika bara la Afrika.

"Hali ya mazingira ya uwekezaji ni nzuri na ina fursa katika sekta za madini, kilimo, viwanda, ufugaji na sekta ya utalii kutokana na kuwapo kwa rasilimali za kutosha katika maeneo yote ya nchi," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa China kuingia ubia na wenzao wa Tanzania katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya gesi asilia, makaa ya mawe, uchimbaji wa madini, utalii, sekta ya hoteli na nyumba za malazi katika hifadhi za taifa.

Alisema ni matumaini ya Tanzania ni kuona makampuni kutoka China yanakuja kwa wingi kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwamo ya miundombinu

Ujumbe wa wafanyabiashara kutoka China unaongozwa na Mwenyekiti wa Makampuni ya Touchroad International Holding Group kutoka Jimbo la Zhejiang, Liehui.

Kongamao hilo limeshirikisha wafanyabiashara zaidi ya 60 kutoka China na 90 kutoka Tanzania Bara na Visiwani

# Waziri atamani sera ya ugatuzi wa madaraka

**Na Paul Mabeja,DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, ofisi ya Rais, Tawala za mikoa na serikali za Mitaa, Selemani Jafo, amesema kuwa kutokuwapo kwa sera ya ugatuaji madaraka iliyojengwa kwenye mfumo wa kisheria ni moja ya changamoto iliyosababisha Serikali kufanya mapitio.

Jafo aliyabainisha hayo jana alipokuwa akifungua kikao kazi kilichokutanisha wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kutoka mikoa yote 26 kwa ajili ya kutoa maoni na mapendekezo kwenye rasimu ya Sera ya Taifa ya Ugatuaji Madaraka.

Alisema changamoto moja wapo ni kutokuwapo kwa sera ya ugatuaji iliyojengwa kwenye mfumo wa kisheria inayoelekeza mipaka, majukumu na utaratibu wa utekelezaji wake, jambo ambalo linafanya ionekane kama ni hiari na utashi.

Aidha Jafo alisema changamoto nyingine ni kuwapo kwa mitazamo inayokinzana kati ya watendaji na viongozi wa kisiasa katika ngazi ya vijiji, kata na halmashauri katika kuweka vipaumbele na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema pia Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitegemea fedha kwa kiasi kikubwa kutoka Serikali kuu na kutolea mfano kwa mwaka 2018 zilitegemea zaidi ya asilimia 88 ya mapato.

Jafo amewataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kutoa maoni na mapendekezo hayo ili kuboresha rasimu hiyo kwa maslahi mapana ya wananchi, wadau na taifa kwa ujumla.

Jafo alitumia fursa hiyo kuwahimiza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kuhakikisha wanasimamia kwa ukabilifu fedha na utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, ujenzi wa hospitali za wilaya, ujenzi wa mabweni, madarasa, vyoo katika shule za msingi na sekondari ambayo tayari fedha zake zimeshatolewa na serikali. Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, aliahidi ushiriki mzuri wa wa wakuu hao kwa kuwa wao ndio wanaotoka kwa wananchi.

Pia alimwakikishia Waziri Jafo kuwa watasimamia kwa umakini utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwa itakamilika katika muda uliopangwa na kwa ubora unaotakiwa.

Mwakilishi wa UNICEF, Pius Chaya, alisema ajenda ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ugatuaji Madaraka imekuja wakati mwafaka, kwa sababu serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma wanazostahili na ambazo zinawafikia kwa wakati.

Aidha, Chaya alisema wadau wa maendeo ambao pia wameshiriki katika machakato wa mapitio ya sera hiyo wameahidi kuendelea kushirikiana na serikali ya awamu ya tano katika kuwaletea wananchi wake maendeleo



RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe.Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Uongozi wa Wizara ya Afya Zanzibar, wakati wa Mkutano wa Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Wizara ya Afya Zanzibar kwa Kipindi cha Julai 2018 -Machi 2019. **PICHA: IKULU**



# Jamhuri yaibua mapya ushahidi kesi ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa na shahidi wa kwanza wa Jamhuri katika kesi kufanya mkusanyiko isivyo halali inayomkabili Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake wanane kuwa askari polisi walifyatua risasi zaidi ya 90 kuzuia waandamanaji wa chama hicho.

Shahidi huyo ambaye ni Mkuu wa Operesheni Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mrakibu Mwandamizi, Gerald Ngichi, alitoa madai hayo jana wakati akihojiwa na wakili wa utetezi, John Malya, kutaka kufahamu idadi ya risasi zilizofyatuliwa. Kesi hiyo inasikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Ngichi alidai waandamanaji walikuwa zaidi 500 na waliokamatwa ni waandamanaji 43 ambapo hakuna aliyeangukiwa na risasi.

Mahojiano ya wakili wa utetezi Malya na shahidi huyo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Mallya:** Shahidi kati ya waandamanaji mliowakamata miongoni mwao kuna mliowakuta na silaha?

**Shahidi:** Hapana.

Mallya: Je, askari uliowaamrisha kupiga risasi za moto hewani walitumia silaha ya aina gani?

**Shahidi:** Ak47.

Mallya: Shahidi risasi ya aina hiyo ya bunduki ikipigwa inakwenda wapi?

Shahidi: Inaenda hewani, halafu inarudi chini.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Zanzibar,Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Katika kesi hiyo jopo la mawakili wa serikali linaongozwa na Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Wankyo Saimon na Jacline Nyantori. Jopo la Mawakili wa utetezi linaongozwa na Prof. Abdalh Safari, Peter Kibatala, John Malya, Hekuma Mwasipu na Jeremiah Ntobesya.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 13 ikiwamo kula njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali.

# Neema malipo makandarasi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imetangaza kuwa kufikia mwishoni mwa mwezi huu, itakuwa imelipa Sh. bilioni 609 kati ya Sh. bilioni 962 inazodaiwa na makandarasi waliotekeleza miradi yake mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana jioni jijini Dodoma na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alipohitimisha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Waziri huyo alibainisha kuwa hadi Juni mwaka jana, serikali ilikuwa inadaiwa na makandarasi Sh. bilioni 833 ambazo haikuzilipa hivyo kuvuka na kuingia katika mwaka huu wa fedha.

"Katika mwaka huu, makandarasi waliendelea kutekeleza miradi na kuzalisha madeni mapya. Hadi Machi mwaka 2019, madeni yalifikia Sh. bilioni 962.

"Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Fedha itakuwa imelipa Sh. bilioni 609 kwa makandarasi mwezi huu," Waziri Kamwelwe aliahidi.

Waziri huyo pia alifafanua kuhusu deni la wafanyakazi wa reli ya Tazara, akieleza kuwa limefikia Sh. bilioni 434, lakini akasisitiza kuwa deni hilo linapaswa kulipwa na nchi mbili; Tanzania na Zambia.

"Lakini katika deni hilo, ikumbukwe kwamba Sh. bilioni 237 ni itifaki ya Serikali ya China ambayo pia inahusisha nchi mbili za Tanzania na Zambia," alisema.

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001:2015 Certified

Mamlaka ya Mapato Tanzania Mkoa wa Kikodi Kahama una waarifu wamiliki wa pikipiki zilizo kamatwa kwa makosa mbalimbali zifuatazo wafike ofisi za Mamlaka ya Mapato Kahama kwa ajili ya kufanya Taratibu za kuchukua pikipiki zao.

| S/N | MOTOVEHICLE | TIN | MMILIKI |
|---|---|---|---|
| 1 | T.357BVR SUNLG | 113-764-279 | GODFREY MPONZI |
| 2 | T.121CUU SUNLG | 114-172-529 | GEOFFSONS ENTERPRENEURSHIP CO LTD |
| 3 | T.610BXG SUNLG | 113-764-279 | GODFREY MPONZI |
| 4 | T.773 CZQ SUNLG | 119-036-356 | YUANSHI MOTOR CYCLE (T2) LTD |
| 5 | T.271 CRP SUNLG | 122-387-217 | GARRISON INVESTMENT CO LTD |
| 6 | T.836 CCE SUNLG | 101-887-618 | KAHAMA IMPORTS & EXPORT |
| 7 | T.318 CZY SUNLG | 107-258-183 | RPS TRADING CO LTD |
| 8 | T.253 AFD SUNLG | 101-909-433 | MOHAMED ABDALLAH |
| 9 | T.924CJR SUNLG | 114-172-529 | GEOFFSONS ENTERPRENEURSHIP CO LTD |
| 10 | T.295CFG | | |
| 11 | T.587CDA | | |
| 12 | T.964AXX | 102-106-229 | GEOFREY MALIYAMONDA |
| 13 | T746CDW | 106-668-620 | LEILA IBRAHIM BA |

Pamoja Tunajenga Taifa Letu.

Tangazo hili limetolewa Meneja wa Mkoa wa Kikodi Kahama

2152224802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wauguzi waendelee kuzingatia maadili

**WAUGUZI** ni miongoni mwa wafanyakazi muhimu wanaotegemewa katika sekta ya afya, Mei 12, wameungana na wenzao kuadhimisha ya siku ya Uuguzi na Ukunga Duniani.

Mwaka huu kitaifa maadhimisho hayo yamefanyika mkoani Katavi kauli mbiu ya mwaka huu ni "Wauguzi Sauti inayoongoza Afya kwa Wote.

Katika maadhimisho ya siku hiyo yaliyofanyika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kuudhuriwa na wauguzi na wakunga wa MNH na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) ambapo walikumbushwa mambo kadhaa.

Pamoja na mambo mengine wametakiwa kuendelea kutekeleza majukumu ya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za kitaaluma kwa lengo la kutoa huduma bora za afya kwa wagonjwa.

Wito huo ulitolewa na Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Agnes Mtawa, aliwakumbusha wauguzi kuzingatia mafunzo yanayotolewa mahala pa kazi kwani ndio yanayochochea kutoa huduma bora ya afya kwa wagonjwa.

Aliwataka wauguzi kutambua kwamba huduma wanayotoa kwa wagonjwa ni ya kibinadamu, pia aliwatia moyo kuwa hivi sasa malalamiko mengi yamepungua.

Tunaunga mkono pongezi hizo, hata hivyo tunawataka wasibweteke wakawa kama mgema kwa kusifiwa tembo akalitia maji, tunatamani kuona kwamba wagonjwa wanapata huduma bora zinazowasaidia kuokoa maisha yao.

Tunaelewa kuwa kuna malalamiko ya msingi na mengine yanachangiwa na mazingira, lakini ukweli unabaki kuwa mgonjwa anahitaji huduma bora. Wapo wauguzi wenye maneno makali ambayo huwafanya wagonjwa kuzidiwa, kwa kifupi tumeshuhudia malalamiko mengi hadi kutoka kwa wajawazito wanapokwenda kujifungua, wapo wauguzi kadhaa ambao wamechukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na makosa mbalimbali waliyoyafanya.

Miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kuwatelekeza wajawazito wakiwa kwenye hatua ya kujifungua, wapo wanaodaiwa kusababisha vifo kutokana na huduma mbovu kwa wagonjwa.

Pia wapo wauguzi ambao wamepata tuzo za aina mbalimbali kutokana na kuzingatia maadili ya kazi zao na kufanya kazi kwa kujituma.

Pamoja na kwamba kuna wakati mnaweza kukumbana na wakati mgumu kutokana na sababu mbalimbali, bado mnawajibika kutumia lugha nyepesi kuwaelewesha wagonjwa ili waelewe badala ya kuwafokea.

Tunatambua wauguzi ni wanataaluma, hivyo wana mafunzo maalum ambayo wamepewa ili kutoa huduma bora kwa wagonjwa, ni vyema wakizingatia ikiwa ni pamoja na kujitahidi kuwa wavumilivu hata wanapokutana na wagonjwa machachari wajue jinsi ya kuwahudumia.

Ni vyema wanapokutana na udhalilishaji wa aina yoyote wajitahidi kuhakikisha wanaushughulikia jinsi inavyotakiwa, siyo vyema kubeba chuki na kuihamisha kwa wagonjwa wengine.


Kazi ya uuguzi na ukunga licha na kuwa ni ya wito, lakini pia inahitaji kuwa na hofu ya Mungu, ili kumudu kujituma kuokoa maisha ya wagonjwa kwa kuwapa huduma inayostahili kwa mujibu wa maelekezo ya mafunzo mliyopata.

Huwezi kuzungumzia huduma bora ya tiba kwa mgonjwa pasipo kuhusisha pembe tatu, ambazo ni madaktari, wauguzi pamoja na vifaa tiba na dawa.

Tunawasisitiza wauguzi watambue umuhimu wao katika huduma ya afya, ni wazi kwamba madaktari wataelemewa iwapo wauguzi hawatakuwapo kwenye sekta hii hii ya huduma ya afya, hivyo jamii inawategemea katika kupata tiba bora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# TRC itupie macho upungufu huu kuboresha zaidi huduma

Na Raphael Kibiriti

YUMKINI huduma zinazidi kutengemaa kwa wasafiri wanaotumia usafiri wa treni au abiria kama ilivyokuwa inafahamika kwa baadhi ya wakazi wa Kanda ya Ziwa nyakati hizo.

Ninazungumzia nyakati za miaka ya 1980 na mwanzoni ya miaka ya 1990 kwa wale waliokuwa wakitumia usafiri wa vyombo vya Shirika la Reli nchini (TRC) nyakati hizo.

Kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa, treni au garimoshi lilijulikana pia kama abiria, nyakati ambazo mbali na kung'aa katika eneo la usafirishaji mizigo, ni usafiri ambao ulitegemewa na wengi katika safari zao.

Si kutokana na bei ya nauli ambayo wengi waliimudu, lakini pia uwezo wa kuchukua abiria wengi kwa wakati mmoja, katika kipindi ambacho usafiri huo ulipatikana karibu kila siku ya wiki.

Ni kipindi ambacho si tu kilirahisisha gharama za usafiri kwa wananchi na wafanyakazi wa serikali, lakini pia kwa wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari nchini, wengi wakiwa wanasoma mbali na makwao.

Muungwana anasema kwamba kuna mambo ambayo yanazidi kuboreshwa katika usafiri wa treni za shirika hilo lililopitia misukosuko mingi ya utoaji huduma kwenye miaka ya katikati ya 1990 hadi ya 2010, baada ya kuwa ameutumia usafiri huo.

Ilikuwa ni mwezi Machi mwaka huu aliposafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mpanda mkoani Katavi, kwa ajili ya kusalimia ndugu na jamaa.

Hiyo ni safari yake ya kwanza akitumia treni kutoka mwaka 1995, na moja ya sababu zilizosababisha kutotumia usafiri huo ilitokana na uduni wa huduma uliojitokeza katika kipindi hicho, kujaza abiria kupita kiasi ikiwa ni sababu mojawapo.

Moja ya mambo yaliyomvutia Muungwana ni utaratibu mpya wa kufanya malipo ya tiketi katika Stesheni ya Dar es Salaam ambapo mkatisha tiketi hagusi fedha ya msafiri.

Kutokana na uamuzi wa serikali ya awamu ya tano kwamba malipo yote ya serikali pamoja na mashirika yake yatumie mfumo wa kielektroniki kufanya malipo, TRC nao wameshaanza kutumia mfumo huo.

Kwa uzoefu alioupitia Muungwana, anaona utaratibu huo pamoja na mengine umepunguza suala la ulanguzi wa tiketi kwani msafiri anatakiwa kuwa na kitambulisho ili aweze kuhudumiwa.

Ni kipindi ambacho si tu kilirahisisha gharama za usafiri kwa wananchi na wafanyakazi wa serikali, lakini pia kwa wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari nchini, wengi wakiwa wanasoma mbali na makwao.

Si hilo tu la kununua tiketi lililoboreshwa, bali hata suala la eneo la kujihifadhi abiria katika Stesheni ya Reli Dar es Salaam pia limeboreshwa likiwa na huduma zote zinazohitajika kwa abiria muda wote anapokuwa pale.

Aidha, suala la kutoa taarifa ya sababu za treni kuchelewa kuondoka au kunapokuwa na dharura ambalo ni la msingi kwa abiria kujua nalo linafanyika kama ilivyotokea kwa Muungwana siku aliposafiri, ambapo ilibidi achelewe kuondoka kwa saa tisa.

Hiyo ilitokana na mazonge yaliyojitokeza njiani kwa treni iliyokuwa ikitokea Mwanza na Kigoma kuja Dar es Salaam.

Hata hivyo, Muungwana alibaini baadhi ya mapungufu katika safari yake ambayo TRC inaweza kuyafanyia kazi kwa sababu hayahitaji uwekezaji mkubwa ama msaada kutoka nje ya nchi.

Mojawapo ya mapungufu hayo ni kukosekana kwa maji kwenye vyoo kwa muda mwingi wa safari.

Wakati stesheni ya treni jijini ina maji ya kutosha, Muungwana alishangaa ni kwa nini maji hayakuwekwa katika vyoo kiasi cha mmoja wa wafanyakazi wa treni hiyo kushauri abiria wa moja ya mabehewa ya daraja la tatu, kula vyakula vikavu ili kuepuka suala la kwenda chooni mara kwa mara.

Ni mpaka treni ilipofika Tabora, ndipo Ofisi ya Stesheni Tabora ilipowataka wahudumu wa mabehewa kuhakikisha kwamba mabehewa na vyoo vyote vina maji na ikafanyika hivyo.

Upungufu mwingine ambao TRC inaweza kurekebisha ni wa baadhi ya abiria na hasa wa njiani kukatiwa tiketi ya kusimama, ambao pia Muungwana aliushuhudia.

Ni rai ya Muungwana kwa TRC kurekebisha mapungufu haya ili kuendelea kuboresha huduma za usafiri huo.

## HABARI KITAIFA

## Tulinde uhai wa binadamu kwa nguvu zote za kijamii

*Mhariri,*

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinasisitiza juu ya hilo.*

*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo jalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia.*

*Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona.*

*Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

***Jupilo Abdul- Singida***

## Tuvuta sigara hadharani si uungwana kwa kweli

***Mhariri Pole na majukumu ya kila siku.***

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyonayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*


*Tabia hii inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

*Bahati mbaya zaidi hata pale wananchi wenzetu hawa wavutaji wanapokanywa ama kunasibiwa waache kuwakera wenzao, baadhi yao huziba masikio na wengine hutoa majibu yasiyofaa.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

***Mwanaidi Ayoub, DSM***




# Mavazi yasiyo na staha hayajengi taswira yetu

**Na Mwandishi Wetu**

MAVAZI ni moja ya vitambulisho vya taifa lolote lile, jamii, kabila na hata makundi mbalimbali katika jamii.

Na ndiyo maana ya maneno kama vazi la taifa, vazi la michezo, sare za mahitaji mbalimbali na hata kuna baadhi ya watu hujiwekea utambulisho binafsi kupitia mavazi.

Uzuri au ubaya wa kitu, ni tafsiri mbalimbali ambazo zinafanya nafsi ya mtu kujieleza, mara nyingi mavazi katika namna ya kipekee yana nafasi kubwa zaidi ya kuwasilisha ujumbe.

Pamoja na uzuri wa kitu au mambo, unaopatikana kupitia mavazi, katika sura ya pili matumizi mabaya au upotoshaji wa namna yoyote katika matumizi yake, yamezua matatizo makubwa katika jamii, hata kufarakanisha wanafamilia.

Sasa malalamiko yametawala, kiasi cha kwamba hata kwenye nyumba za ibada, ambako kunaheshimiwa kwa namna ya kipekee, matumizi mabaya ya mavazi moja kwa moja huwasilisha ujumbe wa kutoheshimu sehemu hizo.

Kimsingi, tafsiri ya mavazi ya heshima hutegemea imani, mila na desturi ya jamii husika.

Hivyo, mavazi ya heshima ni yale yanayozingatia mila na desturi za jamii katika hatua mbalimbali zilizoko, hadi ngazi ya taifa.

Vazi linaloendana na mahitaji ya jamii na miongozo ya ngazi hizo husika, yana maana kubwa sana.

Mathalani, katika sehemu nyingi staha ya mwanadamu ni kuvaa nguo inayohifadhi baadhi ya sehemu za maungo ya miili yao, ambayo kwa mujibu wa imani na desturi, si mahali pa kuachwa wazi.

Kwa kutumia kigezo hicho hicho, ndiyo inazaa marufuku kwa baadhi ya mavazi, ama yasivaliwe kabisa au hayapaswi kuvaliwa katika baadhi ya mazingira na maeneo mbalimbali, mfano hai ukiwa ni kutoruhusu mavazi ya michezo kuvaliwa na wafanyakazi katika sehemu wanakotumikia.

Tafsiri hiyo inaenda mbali zaidi kwa kina mama kuambiwa mavazi yanayobana, mafupi yanayoacha magoti na sehemu za mwili wazi, hali kadhalika kitovu na kifua.

Mwaka 1971, chama cha TANU ambacho kilikuwa kimeshika hatamu za uongozi wa nchi wakati huo, kilitoa waraka maalumu wenye mwongozo kuhusu mavazi.

Madhumuni ya waraka huo, yalikuwa kuimarisha heshima ya taifa, kwa mujibu wa imani ya jamii yake, ikilenga kuhakikisha kuwa watumishi katika sehemu za kazi wanadumisha staha ya heshima wawapo kazini.

Tukichukua kinachojiri leo mbele ya umma kuhusu mavazi na kilichoagizwa kwenye waraka huo wa Tanu, tofauti ni ya kutisha.

Mitindo ya mavazi hivi sasa inaporomosha thamani ya jinsia zote mbili katika jamii. Kwa kifupi hali ni tete.

Pengine hali ingekuwa ni mbaya zaidi, lakini tunapaswa kuzishukuru asasi za kidini, sehemu ambako imani ya umma imeshikiliwa.

Kwa watoto wa kike, imekuwa sehemu ya maisha yao kuvaa nguo fupi zinazoonyesha umbile la miili yao.

Kwa tafsiri yao, wanajihisi wanakuwa warembo zaidi na wanakubalika katika jamii yao ya Kitanzania, kwa kukumbatia utashi huo wenye mzizi kwenye utandawazi.

Ni jambo linalowagharimu wengi katika jamii, baadhi wakifukuzwa au kuzuiwa kuingia kwenye ofisi na nyumba za ibada au hata kutokukubalika katika makazi binafsi. Jumuiya ambayo msingi wake ni mkusanyiko wa watu kwa lengo maalumu ina tafsiri pana, pia huendana na haja ya mtu mmoja mmoja au kikundi kutaka kukubalika nayo.

Inaweza kuwa kwenye kituo cha basi, sokoni, hospitali, nyumba za ibada, shuleni au vyuoni.

Moja ya tiketi muhimu katika kujumuika nayo ni vazi linalokubalika, kama nguo ndefu kwa kinamama ambayo ina kawaida ya kumbandika alama ya kimantiki kuwa mvaaji ni mstaarabu.

Katika mavazi kuna neno kujisitiri ambalo maana yake ni kuficha kitu mahali ili kisionekane.

Lakini kwa karne ya sasa wanaume kwa wanawake, wamekuwa wakivaa mavazi yasiyo na staha kwenye jamii.

Mjadala una rai kwa jamii ya sasa kujirekebisha kimavazi kwa kuvaa nguo zenye staha, na kujikita kwenye maadili kama jinsi mababu zetu walivyokuwa wakiishi, kwa kufuata mila na desturi za taifa letu.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED





Spika wa Bunge, Job Ndugai (Kushoto), akiteta jambo na Mwenyekiti wa Bodi wa Benki ya Biashara ya DCB, Prof. Lucian Msambichaka (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Godfrey Ndalahwa walipomtembelea ofisini kwake bungeni Jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafuriko yaleta maafa Dar

INATOKA UK 2

kwa majani, matawi na miti, kuathirika kwa baadhi ya shughuli za uvuvi na usafiri baharini na ugumu wa upatikanaji wa samaki.

**MKANDAMIZO MKUBWA**

Mutoni alisema katika kipindi cha kuanzia Mei 10 hadi 20, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika.

Alisema hali hiyo inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea Kaskazini mwa dunia na kuwapo nchini hususan maeneo ya Ziwa Victoria.

Alieleza zaidi kuwa joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la Kusini-Magharibi mwa Bahari ya Hindi, linatarajiwa kuendelea na kupelekea pepo kuvuma kutoka Kusini Mashariki na kusababisha kuendelea kwa mvua katika maeneo ya pwani.

Mutoni alieleza zaidi kuwa joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini- Mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

"Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa Ziwa Victoria," alisema Mutoni.

MUELEKEO WA MVUA KWA SIKU 10

Alisema ukanda ya Ziwa Victoria katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara, mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo zinatarajiwa.

Alisema katika Nyanda za Juu Kaskazini-Mashariki katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro mvua katika maeneo machache zinatarajiwa.

Alisema kwa upande wa Pwani ya Kaskazini katika mikoa ya Tanga, maeneo ya Kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo mengi zinatarajiwa. Kuhusu Magharibi mwa nchi katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora, mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache zinatarajiwa kunyesha pia.

Utabiri huo wa TMA unaonyesha pia katika Kanda ya Kati ya mikoa ya Dodoma na Singida itaendelea kuwa mikavu na Nyanda za Juu Kusini-Magharibi katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa, mvua katika maeneo machache zinatarajiwa.

Pwani ya Kusini katika mikoa ya Mtwara na Lindi, mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache zinatarajiwa.

Alisema katika Kanda ya Kusini, mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro, mvua katika maeneo machache zinatarajiwa.

**DART WASITISHA SAFARI**

Kutokana na mfululizo wa mvua zinaoendelea kunyesha, Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART), imesitisha usafiri huo kuanzia jana saa 10:00 alfajiri katika safari za kuelekea, Gerezaji, Posta na Muhimbili.

Aidha, katika barabara ya Morocco ambayo nayo mradi wa mabasi hayo umepita, ililazimika kufungwa baada ya mafuriko kutokea eneo la Kinondoni Mkwajuni.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa Udart, Deus Buganywa, alilieleza Nipashe jana kuwa kabla ya mvua hizo kuanza walishachukua tahadhari ya kuhamisha mabasi yao kwenye ofisi zao za Jangwani.

Bugaywa alizitaja njia ambazo huduma zimesitishwa kuanzia jana saa 10:00 alfajili ni kati ya Kimara-Kivukoni, Kimara-Gerezani, Morocco-Kivukoni na Morocco-Gerezani.

Bugaywa alisema huduma zinazoendelea kutolewa ni kwa mabasi yanayohudumia barabara ya Kimara-Mbezi, Kimara-Magomeni Mapipa, Kimara-Morocco, Gerezani-Muhimbili, Kivukoni-Muhimbili na Gerezani-Kivukoni.

"Tunaendelea kufuatilia hali ya maji katika eneo la Jangwani, yakipungua huduma zitarejea katika hali ya kawaida. Tunaomba radhi kwa usumbufu unaotokana na kusitishwa kwa safari hizi," alisema.

**DAR WATAHADHARISHWA**

Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametoa tahadhari kwa wakazi wa jiji hilo waishio mabondeni kuhama maeneo yao kutokana na athari ya mvua.

Alisema maeneo yaliyofurika ni Jangwani, Magogoni Kigamboni, Ilala Kata ya Mchikichini, Kipunguni, Viwege, Majohe, Kata ya Tabata Madona na Temeke Shule ya Sekondari Kibasila.

Maeneo mengine ni Kinondoni Kata ya Kigogo, Tandale, Bunju eneo la Basihaya, Mwananyamala Mitaa ya Bwawani, Kambangwa, Msisiri 'A', Mbezi darajani na katikati ya Jiji.

"Serikali inaendela kuchukua hatua kurekebisha athari zilizojitokeza ili kuwaondolea adha wananchi kwa kuhakikisha mifereji iliyoziba inazibuliwa, kuweka madaraja ya muda pale madaraja yalipoharibiwa na maji, na kurekebisha barabara ili wananchi waendelee na shughuli zao," alisema Makonda.

Pia Makonda aliwataka wananchi kuzingatia taratibu na kanuni za afya kwa kutozibua na kutiririsha majitaka katika mifereji na mikondo ya maji kwa kuwa hali hiyo inaweza kusababisha milipuko ya maradhi ambayo ni hatari sana kwa maisha na afya za watu.

Aidha, alitaka Kamati ya Maafa ya Mkoa kushirikiana na kamati zote za Maafa za Wilaya kuratibu ipasavyo suala hilo kwa kuweka utaratibu wa kuwataka wakazi waliopo maeneo hatarishi kuhama maeneo hayo ili kuepuka majanga ya mvua yanayoweza kujitokeza.

HALI ILIVYOKUWA DAR

Nipashe ilipita maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na kushuhudia maji yakiwa yameingia kwenye nyumba za watu na mengine kutuama katika barabara na kusababisha baadhi ya njia kufungwa.

Katika eneo la Jangwani maji yalikuwa yametuama katika eneo hilo na kusababisha Mabasi ya Kwenda Haraka, kusitisha safari zake kwa muda, huku wasafiri wakilazimika kutumia usafiri wa pikipiki, baiskeli aina ya mabuta kuvuka eneo hilo.

Wananchi walilazimika kulipa Sh. 1,000 hadi 2,000 kwa ajili ya kuvushwa eneo la Jangwani kuelekea Kariakoo na Posta kuwahi kutekeleza majukumu yao. Waliiomba Serikali kujenga barabara ya juu ili wakati wa mvua waendelee na shughuli zao.

"Kila mara mvua inaponyesha eneo hili na Jangwani tumekuwa tukisitisha shughuli zetu, kama mimi nimekaa ndani siku tatu, tunaomba wajenge daraja la juu ili tuweze kupita," alisema Juma Mzee, mkazi wa Sinza anatefanya biashara eneo la Kariakoo, alishauri kuwapo na daraja ili kuwarahisishia kazi wafanyakazi na wafanyabiashara wa maeneo ya Posta na Kariakoo.

"Njia zipo nyingi za kupita kuelekea mjini, lakini inasababisha kutumia muda mrefu kufika mjini hivyo ni muhimu Serikali ikajenga daraja la juu," alisema Mzee.

Naye William Jacob alikuwa akivusha watu kwa kutumia baiskeli ya buta kutoka eneo la Magomeni Mapipa kuelekeo kituo cha Jangwani kwa Sh. 1,000, alisema wameamua kuacha kubeba mizigo ili kuvusha watu kwa ajili ya kujipatia kipato. Baadhi ya wananchi na wanafunzi walikuwa wakivuka maji ambayo yalikuwa yamefika kiunoni na wengi walikuwa wakisitisha safari zao na kurudi nyumbani.

Katika eneo hilo Nipashe lilishuhudia wanafunzi nao wakiwa wamekwama kutokana mvua.

Madereva wa pikipiki nao walitumia fursa hiyo ya kubeba abiria kwa Sh. 2,000 kutoka eneo la Magomeni Mapipa hadi Kituo cha Faya.

**KIGAMBONI WALIA MAFURIKO**

Baadhi ya wakazi wa Kigamboni waliiomba Serikali kuchukua hatua dhidi ya kero ya mafuriko katika maeneo yao.

Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Ungindoni, walisema kero hiyo ya kujaa maji katika makazi yao imedumu kwa muda mrefu bila hatua kuchukuliwa.

"Tumeshangaika sana kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali wa Serikali na tuna barua kadhaa kama ushahidi, lakini hakuna kinachofanyika zaidi ya kupewa matumaini hewa kila siku," alisema Hamis Mbonde.

***Imeandikwa na Mary Geofrey, Romana Mallya na Enock Charles (Dar).***

## Ndugai aibana Serikali

INATOKA UK 2

**MASLAHI YA TAIFA**

Kwenye ukurasa wa 99 wa kitabu cha hotuba yake ya bajeti, Waziri Kamwelwe anaeleza kuwa mchakato wa utekekelezaji wa mradi huo umesitishwa kwa maslahi ya taifa.

Inaelezwa katika ukurasa huo kuwa serikali inatambua umuhimu wa bandari hiyo mpya inayotarajiwa kujengwa eneo la Mbegani, Bagamoyo, ikiamini kuwa itasaidia kuimarisha ujenzi wa Tanzania ya viwanda na kuchangia kufikia uchumi wa kati.

"Majadiliano na wawekezaji waliokuwapo, yaani Kampuni ya China Merchant Holdings International Limited (CMHI) na State General Reserve Fund (SFRF) ya Serikali ya Oman yamesitishwa baada ya wawekezaji hao kuweka masharti yasiyokuwa na maslahi ya taifa.

"Masharti hayo ni pamoja na wawekezaji kudai kuachiwa jukumu la kupanga tozo na kutoruhusu wawekezaji wengine katika eneo kati ya Bagamoyo na Tanga.

"Majadiliano hayo yanaweza kuendelea iwapo wawekezaji hao wataondoa masharti yasiyo na maslahi kwa taifa," inaelezwa katika ukurasa huo wa kitabu cha hotuba ya makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

**UFAFANUZI WA SERIKALI**

Akihitimisha mjadala huo kwa kujibu hoja za wabunge, Waziri Kamwelwe, alisema mazungumzo na mwekezaji kuhusu mradi huo yanaendea, kauli ambayo ilikinzana na kilichoko kwenye ukurasa wa 99 wa kitabu cha hotuba yake.

Alisema jambo hilo limezungumzwa kwa hisia kali na baadhi ya wabunge lakini amewasiliana na mamlaka na kuelezwa kuwa mazungumzo yanaendelea..

"Nimewasiliana na mamlaka, nimeambiwa mazungumzo yanaendelea, wabunge waridhie kwamba serikali inaendelea na majadiliano, serikali inaendelea na pale itakapokuwa imefikia ukomo wa mazungumzo, itatoa taarifa kwa wabunge ili nao watoe mawazo yao," alisema.

Waziri Kamwelwe pia alifafanua kuhusu uamuzi wa serikali wa kuahirisha kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam- Chalinze (Expressway), akieleza kuwa wizara iliajiri mhandisi mwelekezi kutoka Korea na alimaliza kazi ya upembuzi Desemba 2016.

Alisema Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa idhini ya kuendelea na mradi Mei 22, 2017, lakini tayari serikali ilikuwa imeshaanza mikakati ya kupungumza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam. "Ilikuwa barabara ianzie Bandari ya Dar es Salaam lakini 'study' ikaonekana mizigo itaanzia Ruvu kwenye Bandari ya Pwani," alisema.= Aliongeza kuwa serikali sasa inatekeleza ujenzi wa reli ya kisasa itakayobeba kiwango kikubwa cha mizigo, hivyo kuna haja upembuzi wa mradi wa Expressway ufanyike upya kwa kuwa serikali pia inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nane jijini Dar es Salaam kwenda Bagamoyo.

HABARI KITAIFA

# Neema umeme kwa wachimbaji wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), imetekeleza ahadi ya kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Nyakafuru wilayani Mbogwe Mkoas wa Geita, hivyo kuwawezesha kutumia umeme badala ya mafuta katika kuendesha mitambo ikiwamo ya kuchenjulia madini.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliwasha umeme katika katika eneo hilo la wachimbaji wadogo juzi ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Februari mwaka huu alipotembelea machimbo hayo, na wachimbaji wadogo wa eneo hilo kumlalamikia kuhusu gharama kubwa wanazotumia katika uunuzi wa mafuta ambazo zinafikia hadi Sh. milioni tatu kwa mwezi.

"Serikali inatekeleza ahadi zake badala ya kupiga maneno, hivyo tumeleta umeme hapa si kwa ajili ya kuwasha taa tu, bali umeme huu utawawezesha kuchimba kwa tija, Serikali inataka mchimbe kwa faida ili nanyi muweze kulipa kodi stahiki serikalini itakayotumika kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo." alisema Dk. Kalemani.

Alisema katika eneo hilo imeshafungwa transfoma moja kubwa yenye uwezo wa kVA 315, na kwamba zitafungwa transfoma nyingine Tatu zenye uwezo wa kVA 315 ili kuwezesha eneo hilo kupata umeme wa uhakika utakaotosheleza mahitaji.

Waziri Kalemani aliwaagiza watendaji wa Tanesco kuhakikisha kuwa hadi ifikapo mwisho wa Mei wawe wameshafunga transfoma tatu na moja iliyosalia ifungwe Juni.

Aidha, Waziri Kalemani aliwaasa wachimbaji hao kuchangamkia fursa ya uunganishaji umeme kwa bei ya REA inayoanzia Sh. 27,000 na pia aliagiza Tanesco kupeleka umeme huo katika vitongoji vyote vya kijiji hicho.

Mwenyekiti wa wachimbaji wa Nyakafuru, Walwa Katemi Walwa, aliishukuru Serikali kwa kupeleka umeme katika eneo hilo ambalo lina wachimbaji zaidi ya 3,000 na kuahidi kulipa kodi stahiki serikalini.

Alisema wakati wakitumia mafuta kuendeshea mitambo katika eneo hilo, walikuwa wakilipa kodi zaidi ya Sh. milioni 400, hivyo sasa wanaamini kodi hiyo itaongezeka maradufu kwa kuwa gharama za uendeshaji zitapungua, na pia wataongeza uzalishaji kwa kuwa kuna uhakika wa nishati ya kuendeshea mitambo yao.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Jenerali mstaafu Geogre Waitara, akimvisha cheo cha Kamishna Mwandamizi Kanda ya Kusini, Dk. Christopher Timbuka. Kishoto ni Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, Dk. Allan Kijazi, akishuhudia uvishwaji.

# Kiongozi wa Mwenge agoma kufungua daraja

**Shaban Njia na Neema Sawaka, KAHAMA**

KIONGOZI wa mbio za Mwenge kitaifa, Mzee Mkongea Ali, amekataa kufungua mradi wa daraja wa Kata ya Ngaya katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kutokana na ujenzi wake kutokidhi viwango.

Ali alikataa kuzindua daraja hilo lenye thamani ya Sh. milioni 157, huku akiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani Kahama kuchunguza kama kuna ubadhirifu wa fedha uliojitokeza katika ujenzi.

Hayo aliyabainisha juzi wakati akifungua daraja hilo linalotenganisha Halmashauri ya Mji wa Kahama na Msalala katika mbio za Mwenge.

Alitoa siku 12 kwa Kamanda wa taasisi hiyo wilayani Kahama, Richard Kiula, kuhakikisha uchunguzi huo unafanyika.

"Sisi kama viongozi wa mbio za Mwenge, tumemwagiza kamanda wa Takukuru kuhakikisha kuwa uchunguzi unafanyika juu ya ujenzi wa daraja hilo na kama hakutakuwa na tatizo lolote, basi Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, anaweza kufungua daraja hilo wakati wowote," alisema.

aidha alisema mkandarasi wa daraja hilo alishapewa kiasi cha Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya manunuzi ya nondo, kumwaga kifusi , zege kwa ajili ya utekelezaji wake, na kuongeza kuwa hakuna kilichofanyika, ingawa kazi ilipaswa kuanza Aprili mwaka huu.

"Ninaweza nikalifungua hili daraja muda mfupi likaharibika na wananchi wakaendelea kupata shida, hivyo mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu hazitaweza kuzindua mradi huu, na kwa sasa ninamkabidhi Mkuu wa Wilaya nyaraka za mradi huu. Uchunguzi utapofanyika atauzindua kwa mamalaka aliyopewa na Rais," aliongeza Kiongozi huyo wa mbio za Mwenge.

Aliongeza kuwa yeyote atayebainika kuhusika na ubadhirifu huo, serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wahusika, akiwamo mkandarasi wa Kampuni ya Mumangi Trans and Construction Limited ambayo imepewa zabuni ya ujenzi wa daraja hilo

Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) Halmashauri ya Msalala, Mhandisi Wilfred Gutta, alisema utaratibu ulifuatwa kwa kuwa manunuzi ya nondo hilo yalifanyika katika duka la Nyanza Steel Mill ambalo ndilo lilielekezwa na serikali katika Kanda ya Ziwa.

# Wataka elimu ya mazingira

**Na George Tarimo, KILWA**

WANANCHI wa Kijiji cha Mchakama wilayani Kilwa mkoani Lindi, wameiomba serikali kwa kushirikiana na wadau wa mazingira kuwapatia elimu ya mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza na Nipashe, mwenyekiti wa kijiji hicho, Salumu Msusa, alisema tatizo kubwa linalowakumba wananchi wengi ni kukosa elimu ya utunzaji wa mazingira, hivyo kukata miti ya asili kwa ajili ya kuni na mkaa badala ya kuhifadhi.

"Huku kwetu elimu ya mazingira inahitajika kwa kiwango kikubwa, na inatakiwa tuanze kuwapa wanafunzi wetu kwa sababu wananchi wetu wanakata misitu ya asili kwa ajili ya kuchoma mkaa jambo linalosababisha vyanzo vya maji kupotea na kuathiri jamii nzima ikiwamo binadamu na wanyama," alisema Msusa.

Nao baadhi ya wananchi Fatuma Mkwepu, Amina Lindu na Salumu Itonga, walisema walikuwa wakitembea umbali mrefu kutafuta kuni kwa ajili ya shughuli za nyumbani.

Walisema majiko ya zamani yaliyokuwa yakitumia kuni yalikuwa yanatumia kuni nyingi sana, lakini sasa hawatumii kabisa baada ya kupata ya kisasa ambayo hayatumii kuni nyingi.

"Nikienda kwenye kuni si chini ya wiki mbili, lakini sasa tangu kupata majiko haya natumia kuni chache zaidi ya mwezi na naishukuru serikali baada ya kuona hili wamekuja na staili nyingine ya kuhifadhi mazingira yetu," alisema Lindu.

Frank Luvanda, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la SUHODE linalofanya kazi ya kupambana na uharibifu wa mazingira, alisema wameamua kuwafikia wananchi kwa lengo kutoa elimu ya mazingira, huku akiwataka wananchi kutumia majiko banifu badala ya kuendelea kutumia kuni ya mkaa.

Luvanda alisema shirika hilo limefanikiwa kujenga majiko banifu ambayo yana nafuu kwa wananchi katika kaya 500 hadi sasa na kubakiza kaya chache ili kukamilisha kijiji chote cha Mchakama kuwa na majiko bora ambayo hayatumii kuni wala mkaa.

Alisema kuna mambo mawili yanasahaulika kwenye suala la uhifadhi, na kuwa ni pale wananchi wanapoona misitu au misitu ya asili haina manufaa kwao watakataa kuhifadhi, lakini kama wataona inawapa manufaa watahifadhi hata ile miti ambayo ipo karibu kutoweka.

# Miradi ya kuhakikisha umeme unaendelea kupatikana vijijini yaja

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imebuni miradi ya ujazilizi ili kuhakikisha nyumba zote katika kila kijiji na kitongoji zinaendelea kupata umeme.

Lengo la mradi huo ni kujaziliza katika mapungufu ya miradi ya umeme iliyotangulia.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni jijini na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Agnes Marwa, ambaye alisema nyumba nyingi vijijini hazikuwekewa umeme wakati wa usambazaji japo baada ya kuweka umeme vijijini kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa nyumba na uzalishaji mali kama ujasirimali.

"Je,serikali ina mpango wa kuhakikisha nyumba zote zilizobaki zinapata umeme kabla mradi wa REA haujamaliza muda wake,?" alihoji.

Akijibu, Mgalu alisema Shirika la Umeme (TANESCO), nalo linaendelea kusambaza na kuunganisha wateja mara baada ya miradi ya REA kukamilika ili kuhakikisha wananchi wote wa vijijini wanaunganishiwa umeme kwa gharama nafuu ya Sh. 27,000.

Alisema lengo la serikali kupitia REA ni kupeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara ifikapo 2021 na ili kutekeleza hilo imeweka kipaumbele kwa kusambaza miundombinu ya umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme na katika taasisi zinazotoa huduma za kijamii.

"Utekelezaji wa Mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza ulianza kutekelezwa mwezi julai 2018 na unaendelea katika maeneo yote nchini ambapo utekelezaji wake utakamilika ifikapo Juni 2019. Mgalu alisema maeneo yatakayobaki ikiwa ni pamoja na nyumba za makazi, taasisi, miradi ya maji na biashara yatapelekewa umeme kupitia mradi wa REA III mzunguko wa pili utakaoanza kutekelezwa Julai 2019 na kukamilika Juni 2021.



Msaidizi Maalum wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA, Yusuph Salum akitoa Elimu ya Kodi kwa Mlipa Kodi, Stephano Mapunda, katika maadhimisho ya wiki ya Elimu ya Mlipa Kodi. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Hatma posho kwa madiwani wiki hii

SERIKALI imesisitiza ahadi yake ya kutoa maelekezo juu ya malipo ya posho ya madiwani ndani ya wiki hii.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mwita Waitara, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Edwin Sanda.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema fursa ya vyanzo vya mapato na uwezekano wa kuongeza mapato inatofautiana kati ya halmashauri na halmashauri, hivyo suala la malalamiko linakosa msingi linabaki kuwa dhana kwa kuwa serikali haiwezi kulinganisha kati ya Halmashauri ya Kondoa, Geita au Dar es Salaam.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kuruhusu halmashauri zilipe kadiri ya uwezo wake ili iwe sehemu ya motisha kwa kuwa madiwani ni sehemu ya wanaoweka nguvu ya kukusanya mapato na kuongeza mapato,"aliuliza mbunge huyo.

Aidha, alitaka kujua ni lini sasa watapata waraka wa kufafanua malipo ya Sh. 40,000 kama ulivyotolewa Januari.

Akijibu, Waitara alikiri Madiwani wamefanya kazi kubwa ya kusimamia ukusanyaji wa mapato na makusanyo na ndio maana fedha nyingi zinazokwenda halmashauri, madiwani kupitia vikao vyao na kamati mbalimbali ndio wanapaswa kusimamia na anashukuru wamekuwa wakifanya hivyo.

"Ni kweli Waziri wa Nchi TAMISEMI wakati anamalizia hoja ya wizara aliahidi jambo hilo linafanyiwa kazi,na niwaombe tu muwe na subira ndani ya wiki hii waziri atatoa maelekezo juu ya hili na litafika mwisho," alisema Waitara.

Katika swali la msingi, Sanda alitaka kujua ni kwa nini serikali isiache halmashauri kulipa posho kadri ya uwezo kama ambavyo msisitizo umekuwa toka awali. Akijibu, Waitara alisema ni kweli serikali imetoa ufafanuzi kupitia barua kumbukumbu namba CCB 215/443/01 ya Januari 2 mwaka 2019 juu ya ulipaji wa posho mbalimbali za madiwani ikiwamo posho za kuhudhuria kikao.

"Sheria ya Serikali za Mitaa sura ya 288 kifungu cha 42 na sura ya 287 kifungu cha 70 inamtaka waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa kupitisha viwango vya posho za madiwani, hivyo posho hizo zinapaswa kulipwa kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa," alisema Waitara.

Alifafanua kuwa maelekezo yanayotolewa yanasaidia kuweka usawa wa viwango vya posho za madiwani katika halmashauri nchini hivyo kuondoa malalamiko kutoka kwa waheshimiwa madiwani.

## Mbunge ahoji ziara viongozi wa kimataifa kutozuru Z'bar

SERIKALI imesema katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Aprili mwaka huu jumla ya viongozi 21 wa kimataifa walitembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia William OleNasha, wakati akijibu swali la Mbunge wa Chumbuni (CUF)Ussi Salum Pondeza, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mbunge huyo alihoji kwa nini katika siku za hivi karibuni viongozi hao wamekuwa wakiishia Tanzania Bara tu.

"Mheshimiwa Spika,viongozi wa kitaifa wanaofanya ziara Tanzania walikuwa wakifika Zanzibar na kuonana na Rais wa Zanzibar, je kwa nini katika siku za hivi karibuni viongozi hao wamekuwa wakiishia Tanzania Bara?" alihoji.

Aidha alitaka kujua ni viongozi wangapi wa kimataifa ikiwemo marais ambao wamefanya ziara Tanzania katika kipindi cha 2016/17 na nchi wanazotoka na kati ya viongozi hao wangapi wamefika Zanzibar na wangapi hawakufikia na kwa sababu gani.

Akijibu, Ole Nasha alisema viongozi hao walitoka katika nchi za Afrika ya Kusini, Burundi, Chad, Cuba, Ethiopia, India, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Msumbiji.

Nyingine ni Morocco, Mauritius, Misri, Malawi, Rwanda, Uturuki, Uganda, Uganda, Vietnum, Sudan Kusini, Sri Lanka, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

Alieleza kuwa kati ya viongozi hao wa kimataifa waliotembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tisa walifika Zanzibar na 12 kati ya hao hawakufika Zanzibar.

Alieleza sababu zinazopelekea kutokufika kwao ni kutokana na aina ya ziara, ratiba ya ziara husika na ufinyu wa muda katika ziara, vipaumbele na malengo ya ziara za viongozi hao pamoja na utashi wa kiongozi husika.

"Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kushauri viongozi wa kitaifa kutoka nchi za kigeni wanaozuru nchini kutembelea Zanzibar katika ratiba zao," alisema.

Pia alisema wizara kupitia wazara ya mambo ya nje-Zanzibar imekuwa ikifanya maandalizi stahiki ili kurahisisha viongozi hao kutembelea Zanzibar.

Aidha, alisema kwa kawaida viongozi wa kitaifa wanapokuja nchini wanakuwa na ratiba ya maeneo ambayo wameyaainisha kuyatembelea kulingana na muda waliopanga kuwapo nchini.

Alieleza kuwa pamoja na hilo, wizara imekuwa ikiwashauri viongozi hao kuzuru maeneo mbalimbali ya nchi hususani Zanzibar ili pamoja na mambo mengine kukutana na kufanya mazungumzo rasmi na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutembelea vituo mbalimbali vya utalii vilivyopo huko.

# Mgodi wa Tanzanite kupandwa miche 1,200

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

ZAIDI ya miche 1,200 ya miti inatarajiwa kupandwa ndani ya ukuta na pembezoni mwa migodi ya madini ya Tanzanite katika Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, ili kuendeleza utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, aliyasema hayo wakati akizungumzia shughuli ya upangaji miti inavyoendelea kwenye machimbo hayo.

Ntalima alisema wamefanikisha shughuli hiyo kwa kuotesha miche 374 na wanaendelea kupanda zaidi hadi wafanikishe lengo la miche 1,200.

Alisema shughuli hiyo ya upandaji miti itakuwa endelevu na wamegawa kwenye kanda au maeneo mbalimbali ya machimbo hayo kwa kuanzia kwenye lango la ukuta unaozunguka migodi hiyo.

Alisema wameanza upandaji miche ya miti hiyo kwenye lango la ukuta unaozunguka migodi hiyo katika maeneo ya ndani na nje ya ukuta na pembeni ya barabara mbili zinazopanda migodini.

"Eneo lingine la upandaji miti ni kwenye sehemu za migodi na masoko mawili mapya kwa kuwa tunawahamisha wafanyabiashara katika migodi ili wakafanye biashara sokoni," alisema Ntalima.

Alisema ingawa kwenye maeneo hayo ni porini, wameona waongeze miti hiyo, na kuwa ndani ya wiki mbili wameshafikia lengo la robo ya idadi ya miche ya kupanda.

"Tumeshatoa agizo kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukata mti ndani ya ukuta wa madini ya Tanzanite na endapo yeyote akikiuka na kukata mti atachukuliwa hatua kali," alisema Ntalima.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini mkoani Manyara, (Marema) Tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi, aliwasihi wamiliki, mameneja na viongozi wa migodi kushiriki ipasavyo kwenye shughuli ya upandaji miti.

Mushi alisema kila mmoja akishiriki ipasavyo katika shughuli hiyo, watakuwa wamefanikisha utunzaji mazingira na kulinda uoto wa asili wa eneo hilo.

Alisema kama kila mgodi ukipanda miti miwili kwenye eneo hilo, watakuwa wamepiga hatua kubwa kwenye utunzaji wa mazingira kwenye machimbo ya Tanzanite.

**"Tumeshatoa agizo kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukata mti ndani ya ukuta wa madini ya Tanzanite na endapo yeyote akikiuka na kukata mti atachukuliwa hatua kali," alisema Ntalima.**

# Waziri Mkuu apokea watalii 343 kutoka China

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewakaribisha watalii 343 kutoka China na kuwaomba kutembelea vivutio vyote vilivyo nchini ili wajionee wanyama na rasilimali za asili zinazopatikana nchini pekee.

Akizungumza juzi jijini hapa katika hafla ya kuwakaribisha, Majaliwa alisema wamekuja nchi sahihi na watafurahia ujio wao kutokana na kuwapo vivutio vingi.

Alisema anaamini watatembelea Hifadhi ya Ngorongoro na kujionea shimo kubwa lenye kujaa wanyama.

Pia aliwasihi kupata fursa ya kutembelea Mlima Kilimanjaro ambao mrefu kuliko yote Afrika.

Aidha, alisema watakapotembelea Hifadhi ya Serengeti watajionea wanyama wa kila aina wanaofanya misafara kwenda nchi zingine na kurudi nchini.

Majaliwa alitaja hifadhi zingine watakazofurahia kwa wanyama wa kila aina ni Gombe, Katavi, Rubondo, Ruaha, Mkomazi, Mikumi, Pori la Akiba Selous na Zanzibar kwenye fukwe zenye mchanga mweupe na harufu nzuri zenye marashi ya karafuu na zingine.

Alisema vivutio hivyo hawawezi kuviona popote duniani ila ni Tanzania pekee. Alisema ujio huo ni matokeo ya mahusiano mazuri ya kirafiki yaliojengwa na waasisi wa nchi za China na Tanzania.

Alitoa wito kwa nchi yao kuendelea kufanya kazi na Tanzania na watadumisha ushirikiano zaidi.

Naye Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamisi Kigwangalla, alimshukuru Waziri Mkuu kuwapokea wageni hao na Serikali kuipa kipaumbele sekta ya utalii kwa kufanikisha ujio huo.

Alisema Tanzania imeweka nchi tano za kimkakati katika utalii ambazo ni Australia, Israel, Oman, Urusi, Cuba na China ikiwapa kipaumbele kuwekeza sekta ya utalii.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema wageni hao wametoka miji mikubwa miwili ya Zhejiang na Shangai.

Alimpongeza Rais John Magufuli, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Wizara ya Maliasili, Utalii Ubalozi wa China na wadau wote wa utalii kufanikisha ugeni huo.

Kundi la watalii hao 343 linajumuisha watu maarufu,wawekezaji wa kampuni 27 za China, waandishi wa habari 40, maafisa wa ngazi za juu kutoka serikali ya China na mawakala wa kampuni kubwa za utalii nchini humo.

Watalii hao wameletwa na kampuni ya Touchroard International Holdings Groups ya China ya kiwa ni makubaliano na TTB yaliyofikiwa Novemba mwaka jana walipofanya ziara ya kutangaza utalii katika miji ya Beijing, Shanghai, Chengdu,Guangzhou na Hong Kong.



Mfugaji wa Kijiji cha Irkushbor wilayani Kiteto mkoani Manyara, Yohana Lemunge, akielezea changamoto ya mgogoro wa ardhi wa pori la akiba la Mkungunero juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watumishi afya Monduli wanolewa

**Na Cynthia Mwilolezi,ARUSHA**

WATUMISHI 200 wa sekta ya afya wilayani Monduli, wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na magojwa ya mlipuko kama kimeta na kipindupindu yanayoiandama wilaya hiyo kutokana na mvua za mafuriko na kusababisha vifo.

Mafunzo hayo ya siku tisa yalifanyika Mto wa Mbu na kuendeshwa na wataalamu wa afya kutoka Taasisi ya Tandia yenye makao yake makuu Ujerumani.

Akizungumza na vyombo vya habari wakati wa kufunga mafunzo hayo juzi, Mratibu wa dharura na magonjwa ya mlipuko wilayani humo, Dk. Joel Nkika, alisema semina hiyo ililenga utayari kwa wauguzi na madaktari katika kupambana na magonjwa ya dharura na milipuko kwa Wilaya ya Monduli ili kupata mbinu za kukabiliana nayo.

"Magonjwa ya milipuko yamekuwa yakijitokeza sana wilayani kwetu na kusababisha vifo kwa mifugo na binadamu, kwa hiyo mafunzo haya ya kujiweka utayari yatatusaidia sana kupata elimu ya kukabiliana na magonjwa haya," alisema Dk. Nkika.


Mkurugenzi wa Taasisi ya Tandia, Regina Meissner inayofadhili mafunzo hayo, alisema taasisi yake imekuwa ikisaidia sekta ya afya na elimu wilayani humo, tangu mwaka 2015 na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto za afya kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Alisema pamoja na kufadhili mafunzo hayo pia taasisi yake imekuwa ikisaidia ujenzi wa zahanati kwa kujenga vyumba vya wajawazito kujifungulia katika eneo la Makuyuni na kujenga matenki ya maji katika zahanati mbalimbali zilizopo eneo la Mbuyuni.

"Tumejikita zaidi katika Wilaya ya Monduli baada ya kubaini familia nyingi za kifugaji zina changamoto kubwa ya kukumbwa na magonjwa ya milipuko na uhaba wa vyumba vya kujifungulia, ila tuna mpango wa kwenda katika wilaya zingine kusaidia sekta ya afya," Alisema Meissner.

"Kwa kweli kabla ya mafunzo haya uelewa wangu ulikuwa mdogo, ila nimepata uelewa zaidi juu ya matumizi ya dawa na vifaa na namna ya kujikinga wakati nikihudumia mgonjwa," alisema Dk. Emma Msofe.

Aliongeza kuwa katika ukanda wa Mto wa Mbu ambao wakazi wake wengi ni wafugaji umekuwa ukikumbwa zaidi na milipuko ya magonjwa ya mifugo hasa kimeta na baadae kuwaambukiza kwa binadamu.





# Wanafunzi waanzisha ushirika wa walaji

Na Mary Mosha, MOSHI

MAKALI ya maisha ambayo yamekuwa changamoto kubwa kwa baadhi ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini kikiwamo Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), yamewalazimisha wanafunzi wake kubuni njia ya kupunguza gharama za maisha kwa kuanzisha Chama cha Ushirika cha Walaji cha Wanafunzi.

Chama hicho cha kwanza nchini cha Ushirika cha Walaji cha Wanafunzi kilichoanzishwa na kuzinduliwa rasmi jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, kinajulikana kama Waccos.

Akitoa taarifa kuhusu majukumu na wajibu wa kikatiba kwa jumuiya ya wanafunzi wa chuo hicho, Katibu wa chama hicho, Njenduis Michael, alisema lengo kuu la kuanzisha chama cha ushirika cha walaji cha wanafunzi ni kusaidia kupunguza gharama za maisha ya wanafunzi wanapokuwa chuoni kwa wakati wote wa masomo yao. Kwa mujibu wa Michael, wazo la kuanzisha chama hicho lilitokana na mwitikio wa wanafunzi wa elimu ya juu chuoni hapo kushiriki mara kwa mara maonyesho ya ubunifu na vipaji na kwa mwaka 2019 waliona umuhimu wa kuja hadharani na mpango huo mahususi.

Hata hivyo, baadhi ya viongozi wa chama hicho akiwamo Mwenyekiti wa Bodi ya Waccos hiyo, Mashaka Laurent, ameeleza kuwa nia yao ni kuhakikisha kile kiasi cha matumizi anachopewa mwanafunzi na mzazi wake, kinakidhi mahitaji yake ya kila siku.

Kutokana na mafanikio hayo, Mwenyekiti huyo wa Bodi ya Waccos alisisitiza kuwa mpango wao wa baadae ni kufungua duka, stationary na sehemu ya chakula ambazo zitatoa huduma kwa bei nafuu ili mwanafunzi aweze kumudu gharama zake tofauti na wanavyotozwa na wadau wengine wanaofanya biashara ndani na nje ya chuo hicho. Aidha, wakati anafungua maonyesho hayo, Naibu Waziri wa Kilimo,

Innocent Bashungwa, aliwataka wanafunzi wanaohitimu vyuo vya elimu ya juu nchini kujikita zaidi katika kujiajiri na sio kusubiri kuajiriwa kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kilimo na ujasiriamali.

Kwa upande wake, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prof. Alfred Sife, alimweleza Naibu Waziri Bashungwa kuwa chuo hicho ni miongoni mwa Taasisi za Elimu ya Juu ambazo zinang'aa kimataifa na ambacho kinatambuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa ushindi wa kuwa Centres of Excellence (kituo cha umahiri) cha mafunzo ya ushirika na biashara ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

## Watoto wenye ulemavu 92 wafikiwa kupitia Vicoba Shirikishi

Na Paul William, MOSHI

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya kuwakwamua kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu (TUSONGE) mkoani Kilimanjaro, limefanikiwa kuwafikia watoto wenye ulemavu 92 kupitia Mradi wa Vicoba Shirikishi.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa mradi wa Vicoba shirikishi kupitia shirika la TUSONGE, Hellen Mushi, wakati alipokuwa akizungumza kwenye kongamano lililofanyika katika ofisi za kata Njia Panda mjini Moshi.

Mushi alisema, "watoto hao tunawafikia kupitia wazazi wao ambao ni wanachama wa vikundi vya Vicoba Shirikishi ambavyo viko chini ya shirika letu la TUSONGE."

Aidha, mratibu huyo alisema changamoto mbalimbali katika jamii ndizo zilizosababisha kuingia kwa kina katika kufuatilia baada ya wazazi wao ambao ni wanachama wa shirika hilo.

"Mila na desturi zinazowazunguka ndizo chanzo kikubwa kinachosababisha wimbi kubwa la watoto kufichwa ndani, lakini kupitia mradi wetu huu tumewafikia hao kwa kuwa nao ni binadamu ambao wana mahitaji sawa na wengine," alisema Mushi.

Alisema asilimia 40 ya watoto hao wameshafikisha umri wa kwenda shule, lakini hawajaweza kupelekwa na wazazi wao kwa kukosa huduma za afya na utengamao.

Mushi aliongeza kuwa kupitia mradi huo wamefanikiwa kuwaunganisha watoto hao na CCBRT ambao wamekuwa bega kwa bega katika kufuatilia watu wenye ulemavu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa umoja wa watu wenye ulemavu kata ya Njia Panda Tadei Mbuya, alisema, "wazazi tunapowafuata kuwahamasisha kutowaficha watoto wao wenye ulemavu, wanaona fedheha kwamba mtoto wangu ataonekana kwamba ana ulemavu jamii itanitenga."

Naye Ofisa wa CCBRT anayesimamia kata ya Njiapanda, Gladness Mushi, alitoa hamasa kwa wazazi na viongozi wa serikali kuwaleta watoto wenye ulemavu kliniki ili wapate huduma ya utengamao.

Mradi wa Vicoba shirikishi uliopo Kata ya Njia Panda Himo, Wilaya ya Moshi, unafadhiliwa na African Initiatives na National Community Lottery Fund kutoka nchini Uingereza, yakiwa na dhamira ya kuwaunganisha watu wenye ulemavu ili wajikwamue kiuchumi na kuachana na utegemezi.

**Kwa upande wake Mwenyekiti wa umoja wa watu wenye ulemavu kata ya Njia Panda Tadei Mbuya, alisema, "wazazi tunapowafuata kuwahamasisha kutowaficha watoto wao wenye ulemavu, wanaona fedheha kwamba mtoto wangu ataonekana kwamba ana ulemavu jamii itanitenga."**



Diwani wa Kata ya Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, akiwa kwenye 'winchi' pamoja na mafundi kwenda kushiriki kufunga taa za barabarani katika kata yake. **PICHA: JAMES LANKA**

## TAMPA yaomba serikali kupunguza mamlaka simamizi

Na Mary Mosha, MOSHI

CHAMA cha Usindikaji wa Maziwa nchini (TAMPA), kimeiomba serikali kupunguza mamlaka simamizi zilizoko katika sekta ya maziwa kutoka 31 hadi kufikia 13 ili gharama za uendeshaji wa biashara hiyo zipungue.

Katibu Mtendaji wa chama hicho, Yohana Kubini, alisema hayo katika jukwaa la uhamasishaji unywaji wa maziwa yaliyosindikwa mkoani Kilimanjaro na kuongeza kuwa mamlaka 18 kati ya 31 zimekuwa zikifanya kazi zinazojirudia. Alisema upo umuhimu wa serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza utitiri wa mamlaka hizo zinazofanya kazi za kujirudia rudia ili kumsaidia mzalishaji wa maziwa salama ambayo mwananchi wa kawaida anaweza kuyanunua.

"Zipo changamoto zinazotukabili kama TAMPA, ambazo ni uwapo wa tozo nyingi katika mamlaka simamizi zilizoko katika sekta ya maziwa zimekuwa zikiongeza gharama za uendeshaji wa sekta hiyo hali inayosababisha uuzwaji wa bei kubwa kwa bidhaa za maziwa," alisema.

Kwa upande wake Meneja mradi wa maziwa na uwajibikaji wa utetezi wa sera kutoka katika Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Tom Ole Sikar, alisema katika kuhamasisha unywaji wa maziwa zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo uelewa mdogo wa wananchi kuhusu unywaji wa maziwa yaliyosindikwa.

"Bado wazalishaji wa maziwa hawana elimu ya kutosha kuhusu usalama na utunzaji wa maziwa katika kuhakikisha wanazalisha kwa ubora ili kuwasaidia wasindikaji...tumejitahidi kutoa mafunzo kwa vijana na kinamama 650 namna bora ya kuandaa malisho, kukaamua na usafi wa mabanda," alisema.

Alisema wanaiomba serikali kuhakisha inaungana na sekta binafsi katika kuhakikisha inaendelea kutoa mafunzo kwa wafugaji ili waweze kuzalisha kwa tija kwa kuwa sekta hiyo inauwezo mkubwa wa kutoa ajira kwa vijana .

Mmoja wa wasindikaji wa maziwa Mkoa wa Kilimanjaro, Edmund Mariki, alisema kuwa suala la usafi wa mabanda ya wafugaji bado ni changamoto ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuzalisha maziwa yasiyo na ubora.

Naye mkurugenzi Msaidizi Mazingira ya Biashara Ofisi ya Waziri Mkuu, Christopher Mramba, alisema tayari suala hilo lipo mezani kwao na watalifanyia kazi katika kuhakikisha wanapungunza mamlaka hizo za usimamizi.

"Serikali ya awamu ya tano ni sikivu na inajipanga katika kuhakikisha inasaidia uanzishaji na ukuaji wa viwanda...lipo mezani na tutalifanyia kazi kwa muda mfupi na kutoa majibu kwa haraka," alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 14, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 19



**Ujenzi wa miundombinu wanyanyua taaluma Mlowa, Lyamkena Njombe**

Ukurasa 17



JIELIMISHE

Nyangumi na wanyama wengine walivyotumiwa kufanya ujasusi



Ukurasa 18

## Kwa nini India inachukulia ngono kwa ahadi ya kuoa ni ubakaji?




# Ukeketaji sasa wafanyika kwa siri kubwa Singida

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# FAHAMU UMUHIMU WA HATI YA TABIA NJEMA (POLICE CLEARANCE CERTIFICATE)



Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) nchini, Robert Boaz. **PICHA: MTANDAO**

NI Cheti/Hati ya uthibitisho ambayo hutolewa na Jeshi la Polisi ikithibitisha kuwa mtu aliyepewa hati hiyo hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama kwa makosa ya jinai.

**MATUMIZI YAKE**

Hati ya Tabia Njema hutumika kwa shughuli mbalimbali za uthibitisho kama ifuatavyo:-

Kuomba VISA katika Balozi mbalimbali za nchi za nje zilizopo hapa nchini kwa ajili ya mtu kusafiri kwenda katika nchi hizo kikazi, kimasomo, kibiashara au vinginevyo.

Pili, kuomba ajira ndani ya nchi au nje ya nchi.

Lakini kusajili kampuni na kumiliki bunduki.

Vilevile kuomba uraia wa Tanzania pamoja na Taasisi au mwajiri kumchunguza mtumishi wake.

Aidha, kuomba kibali cha ukaazi katika nchi ya kigeni (Residence permit).

Pia kuomba kibali cha kufanya kazi nchi ya kigeni (work permit) na hatimaye kuomba kibali cha kusoma nchi ya kigeni (study permit).

**KIGEZO CHA KUPEWA HATI YA TABIA NJEMA**

Ili mtu aweze kupewa Hati ya Tabia Njema, inampasa kufika Forensic Bureau Makao Makuu Dar es salaam, kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole ambazo zitachunguzwa kitaalamu ili kutambua kama alishawahi kutiwa hatiani au hapana.

Pia, mbali na Makao Makuu kwa watu walioko mikoani wanaweza kufika katika ofisi za wakuu wa Upelelezi wa Mikoa au Ofisi za Polisi za Wilaya waliko kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole ambazo zitatumwa Forensic Bureau Makao Makuu kwa ajili ya uchunguzi na utolewaji wa Hati ya Tabia Njema ambayo itatumwa kwa mhusika aliyeomba hati hiyo.

**UMUHIMU WA HATI YA TABIA NJEMA**

Katika dunia ya leo yenye shughuli nyingi na mwingiliano mpana na ulio wazi kwa kiasi kikubwa kati ya watu wa mataifa mbalimbali, hakuna nchi ambayo ingependa kupokea mtu ambaye haeleweki au mtu mwenye historia mbaya ya uhalifu.

Halikadhalika, hakuna kampuni au taasisi yeyote ambayo ingependa kumwajiri au kumpa jukumu lolote mtu ambaye ana historia chafu ya kiuhalifu. Nchi na kampuni au Taasisi mbalimbali zinahitaji watu wenye tabia na mwenendo mwema katika maisha ambao hawawezi kuwa chanzo cha matatizo katika nchi au taasisi zao.

Hivyo, ni jukumu la kila mtu kujitunza na kutojihusisha na uhalifu wa aina yoyote ili asije akakosa huduma hii muhimu kwa sasa ambayo ukiikosa ni dhahiri unaweza kushindwa kufikia malengo.

Hayo yaweza kuwa ni ya kielimu, ajira, biashara, safari za kikazi, kibiashara, kiutalii, kusajili kampuni n.k.

**MAMLAKA YA KUTOA HATI YA TABIA NJEMA**

Hati ya Tabia Njema hutolewa na Jeshi la Polisi kupitia kurugenzi ya Forensic Bureau ambayo ni Taasisi ya Uchunguzi wa kisayansi ndani ya Jeshi la Polisi. Mojawapo ya huduma muhimu zinazotolewa na Taasisi hii ni Hati ya Tabia Njema (Police Clearance Certificate) ambayo kwa kiasi kikubwa ni kwa matumizi ya kiraia.

**VIAMBATANISHO MUHIMU KATIKA MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA**

Pamoja na alama za vidole, viambatanisho muhimu katika maombi ya Hati ya Tabia Njema baadhi vinatofautiana kulingana na sababu ambayo mtu au Taasisi inaombea Hati ya Tabia Njema kama ifuatavyo:-

**VISA YA MASOMO NJE YA NCHI**

Kunahitajika Nakala ya hati ya kusafiria, Nakala ya barua ya kukubaliwa chuo (ADMISION LETTER).

Pia Picha Passport size 1 na Barua ya maombi.

**VISA YA MAKAZI/KUFANYA KAZI NJE.**

Kunahitajika Nakala ya hati ya kusafiria na Picha Passport size 1.

Aidha, Barua ya maombi na Nakala ya mkataba wa kazi.

**URAIA WA TANZANIA.**

Kunahitajika Barua kutoka ofisi ya uhamiaji, Nakala ya Hati ya kusafiria na Picha passport size 1.

**MAOMBI YA KAZI/AJIRA NDANI YA NCHI**

Kunahitajika Barua ya ofisi anayotarajia kuajiriwa k.m Benki, Kampuni za ulinzi n.k.

Nakala ya kitambulisho cha mhusika na Picha passport size moja pamoja na Barua ya maombi kama mhusika hatoki kwenye Taasisi.

**MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA KWA WAGENI WALIO NJE YA NCHI.**

Kunahitajika Nakala ya Hati ya kusafiria na Picha passport size 1.

Lakini Alama za vidole zilizochukuliwa kutoka Kituo chochote cha Polisi katika nchi ambapo mhusika anaishi na Barua ya maombi.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi***
***Dar es Salaam.***
***habariphq@gmail.com***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# BAKITA wanaridhia upotoshwaji huu?

WATAKA kujua upotoshaji wa Kiswahili unaosemwa kuwa ni 'Kiswahili cha kisasa?' Soma magazeti ya michezo.

Wataka kuchafua lugha azizi (-a thamani) ya Kiswahili? Usipitwe na magazeti yetu ya michezo. Wataka kujua mseto wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza (Kiswangereza)? Usipitwe na safu hii ya 'Tujifunze Kiswahili' kila Jumanne kwenye gazeti maarufu la Nipashe, Mwanga wa Jamii.

"Maneno hataki maneno mbofumbofu" ni kichwa cha habari kwenye moja ya magazeti yetu ya michezo. Nimejaribu kutafuta na kuuliza maana ya 'mbofumbofu' kutoka kwa watu mbalimbali nikapata jibu nisiloridhika nalo kwamba eti maana yake ni 'mbovumbovu.'

Kama ndivyo, ingeandikwa: "Maneno hataki ubabaishaji" yaani maneno ya kudanganya.

"Mavituz ya Mane yampagawisha Fowler." Kiswahili hakina neno 'mavituz' wala wingi wa vitu si 'mavituz' kama alivyoandika mwandishi wa gazeti la michezo. 'Kitu' ni umoja (kitu hiki) na 'vitu' ni wingi (vitu hivi). Hakuna 'mavitu' wala 'mavituz.'

'Kitu' ni chochote kinachoweza kubainishwa kwa kutumia milango ya fahamu: kuonekana, kushikika, kuonjwa n.k. Aidha jambo, mali au fedha; chochote ambacho si mtu wala mnyama. Pia ni mnyama mweusi wa jamii ya paka.

"Aliyewapa maujanja Simba aibukia AFCON" ni kichwa kingine cha habari kwenye gazeti la michezo. 'Ujanja' ni uwezo wa mtu wa kubuni mbinu za kufanya au kukwepa jambo kwa urahisi. Pia ni hali ya kuwa na hila, tabia ya kudanganya; ghiliba, akili, werevu. Neno hili halina wingi; hivyo ni kupotosha lugha isemwapo au iandikwapo 'maujanja.'

"Madogo 10 AFCON usiwapime, wanakinukisha majuu buana." Kichwa hiki cha habari hakieleweki ila kwa aliyekiandika! 'Madogo' latokana na 'dogodogo' yaani –sio na kiwango kikubwa: biashara ndogondogo yenye mtaji mdogo; viwanda vidogovidogo; –sio enye umuhimu mkubwa; mambo yasiyokuwa muhimu sana. Mambo madogomadogo.

'Usiwapime' ni kukataza kiumbe kupimwa kama vile kujua uzito, urefu au kuwachunguza damu ama choo. Pia kadiria au linganisha hoja ili kupata inayofaa. Hapa pia twapata neno 'pimajoto' yaani chombo chenye zebaki ndani ya kioo kinachotumiwa kupimia joto la mwili. Aidha 'pimamaji' ni chombo cha ujenzi au useremala chenye maji ndani ya kioo kitumikacho kupimia usawa wa kitu.

'Kinukisha' maana yake nini? 'Nuka' ni toa harufu mbaya, aghalabu kwa sababu ya kuoza. 'Nukia' ni toa harufu nzuri ya kupendeza kama ya marashi; firidi. Kitendo cha jambo kukaribia kutendeka au kutokea. 'Nukisha' ni kumfanya mtu anuse harufu nzuri au mbaya.

'Majuu' ni wapi? Ni nchi gani duniani yaitwa 'majuu'? Eti kwa Kiswahili cha kihuni 'majuu' ni Ulaya! Kumbe kuna siku Tanzania itaitwa 'Tanzia' yaani taarifa ya kifo inayopelekwa mahali pengine! Kweli ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni! Maana yake ukishangaa kutokana na miujiza ya Musa utashtuliwa na matendo ya Firauni.

Sielezi maana ya 'buana,' 'bhana' wala 'bana' kwani nimeeleza mara nyingi sana kwenye makala zangu lakini ni kama nawapigia mbuzi gitaa … hawachezi wala kujifunza ila kukodoa (toa macho pima, fumbua macho na kuyakaza sana)!

"Abdi Banda mambo ni fire." Ina maana mwandishi angeandika: "Abdi Banda mambo ni moto" isingeeleweka bila kuchanganya neno la Kiingereza (fire) lenye maana ya moto? 'lay a fire;' (koka moto). 'set on fire' (choma moto, tia moto, unguza) na 'catch fire' (shika moto).

"Meneja wa Samatta kuwapa shavu wachezaji kibao." 'Shavu' ni sehemu ya uso kati ya jicho na taya la mtu. Kiungo cha samaki atumiacho kuvutia hewa. Kichwa alichoandika mtangazaji maana yake ni kwamba meneja wa Samatta amewapa wachezaji wengi 'shavu.' Ina maana baadhi ya wachezaji hawakuwa na mashavu?

Kutokana na waandishi kutumia maneno ovyo na kuchanganya Kiingereza, baadhi yao wanashindwa hata kujua matumizi sahihi ya maneno ya Kiswahili! Soma hii: "Mwanamke auawa akitaka kubakwa." Nilipo-soma kichwa hicho cha habari, nilishangaa kuwa mwanamke ameuawa 'akitaka' kubakwa!

**Methali: Eleza haja upate haja.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

SAIKOLOJIA

NA NA MICHAEL ENEZA

# Tatizo la kujiua linavyotesa fikra, maadili tangu zamani

HAKUNA jambo ambalo linatesa fikra ya jamii kama tatizo la mtu kuamua kukatisha maisha yake mwenyewe, jambo ambalo katika sheria ni kosa la jinai, lakini sheria inachukua mkondo wake tu endapo jaribio hilo halikufanikiwa.

Mara nyingi zaidi dhamira ya kujiua inafanikiwa kwa hiyo inakuwa ni janga la kifamilia na kijamii kwa upande mwingine, kwani lawama hiyo ya kisheria na hata uvunjifu wa sheria siyo rahisi urudiwe katika ngazi ya familia na jamii, ila huzuni kwa yaliyotokea hadi mhusika au marehemu akashindwa kumudu maisha kiasi cha kuchukua uhai wake.

Kuna chembe ya kujiri kuonewa kwake, kupungua kimaadili kwa jamii.

Ina maana kuwa mtu anapojiua anaihukumu jamii kwa kilichotokea, kwani kwa kawaida kila mtu ana aina ya mzunguko wa watu ambao wanatazamiwa kumjali, na inapofikia hatua ambako mtu haoni faida ya kuonana na watu wengine, au kuendelea na kile kinachoitwa kwa kawaida ni kufurahia maisha, kuna tatizo kubwa mahali.

Huzuni na mkasa wa kimaadili katika suala hilo ni kuwa ni jambo linalotesa wahusika kijamii kimyakimya, kwani hapatakuwa na nafasi ya kuulizana kibagaubaga nani alikosea katika jambo gani, kama ingeweza kurekebishwa, na kimsingi hakuna anayetaka ahojiwe, na hakuna anayeweza kukubaliana na tukio. Pia hawezi kulaumiwa mfu.

Kuna tofauti kati ya kifo cha kujitakia na kile cha kutakiwa na wengine, lakini pale mhusika wa kifo cha kutakiwa na wengine anapokiruhusu, anaitia jamii husika katika majaribio makubwa kujitizama upya kimaadili, na mara nyingine mfumo mzima wa kimaadili wa jamii hiyo unaathirika.

Ndiyo ilivyokuwa katika historia, kwa watu wawili wanaofanana, na hata majina yao ni kama yanaendana, yaani mfikiriaji wa Kiyunani Socrates, na mhubiri wa Kiyahudi aitwaye Yesu, au yule Kristo.

Socrates alikuwa akipita maeneo mengi, siku hizi ingeitwa ni mihadhara, akifundisha watu jinsi ya kufikiri, hasa kujitambua na kutambua kinachokuzunguka, kwa usahihi.

Ni katika mazingira hayo ambako Socrates aliingia katika mzozo na wakuu wa mji wa Athens, zaidi kidogo ya miaka 300 kabla ya Kristo, na wakati mmoja akahukumiwa kifo kwani mafundisho yake yalikuwa yanapingana na maelezo ya makuhani katika mahekalu ya miungi ya Wayunani.



Msongo wa mawazo ni moja ya sababu ya watu kujiua kwa mujibu wa utafiti. **PICHA: MTANDAO**

> Sheria na dhana nzima ya uadilifu kisheria Uyunani ukatetemeka, mpangilio wa fikra ukaanza upya na alichosema Socrates kikawa ndiyo mwanzo wa fikra mpya.

Alipotupwa gerezani ili hukumu ya kifo itekelezwe, alipewa nafasi ya kutoka gerezani kana kwamba ametoroka, halafu aondoke katika mji huo aende kuishi kwingine.

Sababu ilikuwa kwamba wengi kati ya wanajamii na hata baadhi ya watawala na askari wa mji huo walikuwa wanafurahia mafundisho yake, huku wakiona bayana kuwa yanahatarisha uimara wa dini yao.

Jambo la kushangaza ni kuwa Socrates aliamua kubaki hapo gerezani hadi hukumu hiyo itekelezwe, au uamuzi mwingine ufikiwe kisheria kuwa atoke, lakini siyo atoroke kwani hapo atakuwa amevunja sheria, kwa mantiki kuwa kutekelezwa kwa hukumu hiyo ilikuwa ni sehemu ya kuitii sheria.

Ikafika siku ya kutekelezwa kwa hukumu na Socrates bado yuko hapo gerezani hivyo hukumu hiyo ikatekelezwa kwa yeye kupewa kikombe chenye sumu (kinywaji) naye akijua hivyo, akanywa na akafariki dunia.

Sheria na dhana nzima ya uadilifu kisheria Uyunani ukatetemeka, mpangilio wa fikra ukaanza upya na alichosema Socrates kikawa ndiyo mwanzo wa fikra mpya.

Cha msingi kilichobadilika ni kuwa mizimu (au wao wanasema miungu) wakaondolewa kama mojawapo ya nyenzo za uthibitisho wa chochote kile ila fikra, na ndiyo mwanzo wa kuondolewa kwa dhana ya kuthibitisha maadili au usahihi wa chochote kile kwa kunukuu maandiko ya dini au dhehebu.

Mazingira hayo yalishamiri kwa kipindi kifupi kama mapokeo ya wasomi, na baada ya miaka 300 mazingira hayo yakaathiri kukua kwa msukumo wa aina tofauti unaofanana na ule wa Socrates, yaani kifo cha mhubiri wa Kiyahudi ambaye wengi walimtazamia awe Masihi, ila hakuiendea njia au mwelekeo waliotazamia.

Alipohukumiwa kifo na kukataa kufanya ishara au muujiza wowote ili asiuawe kikatili kwa mtindo wa kumpigilia mtu msalabani, dini ikayumba.

Suala la kujiua ni moja ya maeneo yaliyowezesha kuanza kwa taaluma ya miingiliano ya kijamii (sociology), kwani kuanzia miaka ya 1850 nchini Ufaransa wimbi la wasomi wa masuala ya jamii wasiotaka kuendea fikra zinazoelekea katika 'mabadiliko, maendeleo na mapinduzi' lilijengeka.

Suala lilikuwa mshtuko wa usomi nchini humo kutokana na mkasa wa Mapinduzi ya Ufaransa mwaka 1789 ambayo yalitokana na mivutano ya karne nyingi kati ya tabaka la watwana wanaotoa kodi ya ardhi kwa mamwinyi wanaoimiliki, halafu na wafanyabiashara ambao wakati huo walitaka wawe huru wasitawaliwe na kodi maridhawa zinazowekwa na mamwinyi, wakisimamia na utawala wa kifalme.

Halafu kukawa na mageuzi ya kidini Ulaya nzima, yakaleta maafa mengi.

Dhana ya weledi bila ukinzani (positivism) ilifuta hulka ya kutaka kujua chanzo cha hiki au kile, na badala yake kutafuta kama kuna uhusiano kati ya kitu kimoja na kingine.

Kwa mfano badala ya kuyakinisha chanzo cha kujiua na kutaka kuunda kanuni ya maadili kutokana na chanzo kinachofikiriwa, ni rahisi zaidi kuyakinisha ni aina gani za watu wanajiua, na kama kuna mazingira maalum ya mtu kujiua, kutafuta kama kuna chembe au taswira za kimazingira zinazoashiria hali hiyo, halafu zipimwe kuona kama zinaoana, kuendana.

Kwa njia hiyo mtu anapata picha ya aina ya watu wanaoweza kujiua, lakini haingii katika mtego wa kuyakinisha sababu husika.

Hivi karibuni mjadala ulikuwa unasikika katika moja ya vituo vya redio ambako mchangiaji mmoja kutoka Arusha alisema kuwa walifundishwa katika darasa la theolojia Chuo Kikuu Makumira kwamba wanaojiua zaidi ni watu wenye wake au wenza, kwa maana kuwa wanaume wanajiua zaidi ya wanawake.

Kwa vile mchangiaji alisema walifundishwa darasani chuoni, ina maana kuwa tafiti zinaonyesha kuwa hali hiyo ina vielelezo vingi, lakini kuna suala la umri wa wanaojiua, hata kama ni wanandoa au wana unyumba, kuishi pamoja.

Pia kuna mazingira ya mahusiano ya vipato, umri wa kiuhusiano, kama ni wanandoa au wenza wenye umri unaofanana au kupishana kwa kiwango gani.

Vielelezo hivyo hutoa picha, hivyo mtu anaweza kutafakari mengine yaliyobaki.

Kutumiwa kwa vigezo vya mahusiano na idadi za watu wanaojiua ni njia ya kuondoa mkanganyiko wa kutoa sababu za watu kujiua, kila mtu akiongea ya kwake, na pia kutafuta kama kuna kanuni au mazingira ya jumla ambayo yakifikiwa huleta hatari ya mtu kukwama katika mahusiano, akwame pia kifikra, ajiue.

Unaweza pia kuangalia hisia za kijinsia katika mjadala huo, kwani watangazaji walianza kubishana ambako mtangazaji wa kike alijaribu kuainisha kuwa tatizo ni kuwa mtu huyo (aliyejiua) alichagua sura na hakumfahamu mwenza kwa ndani.

Waliobaki hawakuwa na uhakika huo, kwani unakutana na mtu umpende; mengine utajua hapo baadaye.

## ELIMU

**NA SALOME KITOMARI**

# Ukeketaji sasa wafanyika kwa siri kubwa Singida

• Ni kwa imani ya kutibu ugonjwa wa 'lawalawa' • Ni kupitia kucha ndefu iliyofugwa na ngariba • Kidonda hupakwa mkojo au masizi ili kipone

KWA mujibu wa Kamusi ya Kiswahili (Swahili Oxford Living Dictionaries), neno mila lina maana ya mambo yanayofanywa na jamii fulani ambayo yanalingana na asili, mazingira na nyendo za jamii hiyo.

Nimeanza kutoa maana ya neno hilo, kwa sababu makala zangu tatu zijazo kuanzia hii zinajikita zaidi katika eneo hili la mila kutoka mojawapo ya makabila yaliyoko Kanda ya Kati na Ziwa. Jamii nyingi katika maeneo mbalimbali nchini na kwa maana hiyo makabila tofauti yameweza kuwa yalivyo hivi leo pamoja na mambo mengine kwa sababu ya kutoa kipaumbele kwenye mila zao.

Hivyo mila ni eneo la thamani kubwa ambalo limechangia maendeleo ya jamii kwa upande mmoja, lakini pia kudumaa kwa baadhi ya jamii nchini na katika maeneo mengi Afrika na hata nje ya bara hili.

Pamoja na hayo kuna baadhi ya mila ambazo zimepitwa na wakati, ama kutokana na kuwa kandamizi au kwa sababu ya athari kubwa kwa baadhi ya wanajamii katika maisha yao yote. Na ndiyo maana athari zake zimekuwa zikipigiwa kelele na serikali pamoja na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali na wadau wenye mapenzi mema ili zitokomezwe kabisa.

Kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na wadau kuhakikisha mila zisizofaa haziendelei na wanaoziendeleza wanachukuliwa hatua za kisheria, mila hizi sasa zinafanyika kwa usiri mkubwa. Mojawapo ya Mila hizo ni ya ukeketaji (FGM), inayohusisha kuondolewa kwa sehemu au jumla ya sehemu za siri za msichana.



Baadhi ya wasichana walionusurika kukeketwa katika Kata ya Kang'ata, wilayani Handeni. **PICHA: MTANDAO**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, (kulia) akisalimiana na wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Ikungi, mkoani Singida. **NA MPIGA PICHA WETU**

> Tunatoa elimu kwenye jamii na shuleni kuelimisha wazazi na watoto wenyewe kukataa kufanyiwa ukeketaji.

#### TAKWIMU

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kwamba kati ya wasichana na wanawake milioni 100 na 140 wamefanyiwa ukeketaji, na wasichana milioni mbili zaidi wako katika hatari ya kukeketwa kila mwaka.

WHO inasema wengi ya wanawake na wasichana hawa wanaishi katika nchi 28 za Afrika, Tanzania ikiwamo, chache za Mashariki ya Kati na Asia, Jumuiya ya wahamiaji barani Ulaya, Australia, New Zealand, Marekani na Canada. Na ndiyo maana Umoja wa Mataifa (UN), ukaiweka Februari 6 ya kila mwaka kuwa siku ya kutokomeza aina zote za ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake duniani.

UN iliweka siku hii kwa kuzingatia kuwa kitendo hicho pamoja na kukiuka haki za binadamu kinakwamisha harakati za maendeleo ya kundi hilo wakati huu ambapo dunia inasaka si tu ulinzi wa kila binadamu, pia kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo, bado kuna makabila au baadhi ya watu ambao wanahama na mila hizo zisizofaa ikiwamo ya ukeketaji kila waendako.

#### KWA NINI?

Wanahama nayo kwa kuamini kuwa wasipofanya hivyo watapata laana au majanga mbalimbali.

Yapo makabila nchini yanayojulikana kwa kuendeleza mila hiyo ingawaje sasa kwa kujificha na hivyo kuja na mitindo tofauti ya ukeketaji.

Kuna makabila ambayo sasa yanakeketa watoto wa kike katika umri wa kati, moja kwa moja wakiandaliwa kuolewa.

Lakini wapo wanaolewa kwenye familia fulani wakiwa hawajakeketwa ambapo hulazimishwa kwanza kukeketwa ili wakubalike katika familia walizoolewa. Aidha, kuna wanaokeketwa wakiwa watoto na wengine kwenye madarasa ya awali.

Mikoa wa Kanda ya Kati kwa maana ya Dodoma na Singida ni miongoni mwa mikoa ambayo bado ukeketaji unaendelea kufanyika. Katika mikoa hii, ukeketaji unafanyika kwa watoto wachanga lakini kwa siri kubwa, kwa ushirikiano baina ya ngariba, wazazi wa mtoto na mama mkwe kwa madai ya kutimiza mila hiyo.

#### SHIRIKA LA ESTL

Mkurugenzi wa Shirika la Empower Society Transform lives (ESTL), Joshua Ntandu, ameueleza muungano wa Asasi zisizo za kiserikali zinazopinga ukeketaji zilipokutana jijini Dar es Salaam, kuunda umoja wa kupambana na suala hilo hivi karibuni, namna ukeketaji unavyofanyika mkoani Singida.

Anasema Mkoa wa Singida una makabila makubwa mawili ambayo ni Wanyaturu na Wanyiramba, yote yakitekeleza mila hiyo kwa usiri mkubwa.

Ntandu anabainisha kwamba ukeketaji katika mikoa hiyo hufanywa na wanawake wanaoamini kuwa ndiyo namna sahihi ya kutibu 'lawalawa'.

"Hiyo ni baada ya kuona serikali inafuatilia kwa karibu ili ichukulie hatua wanaoendeleza mila hii potofu," anasema.

Anasema utafiti uliofanywa na shirika hilo umebaini kuna usiri mkubwa kwa kuwa jamii hizo zinaamini ukeketaji unatibu ugonjwa wa lawalawa, ambao kihalisia unatokana na uchafu kwenye sehemu za siri za mtoto wa kike.

"Wazazi wengi wanaamini kwamba wakikata sehemu za siri za mtoto, wanatibu ugonjwa huo... hata hivyo kiuhalisia si kweli kwani huo ni ugonjwa wa njia ya haja ndogo unaosababishwa na uchafu kwenye sehemu hizo na tiba yake si kukeketa mtoto," anasema.

#### KINACHOFANYIKA

Ntandu anasema ukeketaji hufanywa na ngariba ambaye amefuga ukucha mrefu wenye makali kwa ajili ya kukata kinyama husika pale mtoto anapozaliwa.

Mkurugenzi huyo anabainisha kwamba wanakeketa watoto wakiwa wachanga kwa kuwa nyama yao inakuwa bado laini.

"Ngariba anafuga ukucha mdogo ambao ni kwa ajili ya kazi hiyo na wakati mwingine anatumia kisu maalum cha asili," anasema na kuongeza: "Kwa kutumia ukucha uliochongwa, hukata kidogo kidogo hadi kukimaliza kinyama kilichopo kwenye eneo la siri."

#### KISHA TUMBAKU AU MASIZI

Ntandu anasema baada ya ngariba kufanya kazi yake, kidonda hupakwa tumbaku au masizi kama namna ya kukiponya.

"Kutokana na jitihada za serikali kuingilia kati na kuwakagua watoto kila wanapopelekwa kliniki, sasa wamekuja na mbinu nyingine," anasema na kuongeza:

"Wazazi katika makabila haya huvizia na kuitekeleza mila hii nyakati ambazo watoto wamemaliza chanjo zote au wakati wanajiandaa kwenda shule ya awali ama nyakati za likizo, hasa ya mwezi Desemba, ambacho huwa ni kipindi cha baridi."

#### TIBA YA KIDONDA CHA UKEKETAJI

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, vidonda vya ukeketaji hutibiwa kwa usiri mkubwa nyumbani na kuwa wapo baadhi ya waathirika ambao hupoteza maisha kutokana na kuoza sehemu za siri.

#### MKOJO WA BIBI KIZEE

"Tiba inafanywa na bibi kizee ambaye ameshaacha kufanya mapenzi... hukojoa mkojo wake ambao huhifadhiwa kwenye kibuyu kwa muda wa siku saba... baada ya hapo mkojo huo hupakwa kwenye kidonda cha mtoto husika kila siku," anasema.

> Hiyo ni baada ya kuona serikali inafuatilia kwa karibu ili ichukulie hatua wanaoendeleza mila hii potofu.

Ntandu anabainisha kwamba wakati mwingine wazee wa kike saba (mabibi) hukojoa mikojo yao ambayo kwa pamoja huhifadhiwa kwenye kibuyu kwa siku saba.

"Hiyo ndiyo inakuwa tiba ya vidonda vitokanavyo na ukeketaji kwa watoto tofauti tofauti waliokeketwa wakati huo," anasema.

Mbali na madhara ya kuoza, Ntandu anabainisha kwamba watoto wengine hukumbana na maumivu makali.

#### MATIBABU HOSPITALINI

Anasema pamoja na madhara hayo, bado wazazi huwa hawawapeleki hospitali watoto wao walioathirika kwa hofu ya kukumbana na mkono wa sheria.

"Mbaya zaidi nyama zinazokatwa kutoka kwa watoto baada ya kukeketwa huhifadhiwa na nyingine hutupwa kwenye zizi la mifugo kwa imani ni chanzo cha kupata utajiri, jambo ambalo si kweli kwani familia husika huendelea kuwa maskini," anasema.

#### MKURUGENZI HALMASHAURI

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ikungi mkoani Singida, Justice Kijazi, anathibitisha kuwepo kwa vitendo hivyo.

Hata hivyo anabainisha kwamba serikali inachukua hatua mbalimbali kukomesha mila hiyo ikiwa ni pamoja na kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali kuelimisha jamii.

Kijazi anasema kuna mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuacha mila ya ukeketaji, na kwamba halmashauri kupitia idara ya maendeleo ya jamii inatoa elimu kuhusu madhara kwa watoto wa kike wanapokeketwa.

"Tunatoa elimu kwenye jamii na shuleni kuelimisha wazazi na watoto wenyewe kukataa kufanyiwa ukeketaji," anasema na kuongeza:

"Kwa kuanzia kuna kata za Puma, Ikungi, Isuna na Man'gonyi ambako kuna shirika linatoa elimu kwa wanawake, ngariba na familia mbalimbali juu ya madhara ya ukeketaji pamoja na kuunda kamati za ukeketaji na sasa wameacha," anasema.

Kijazi anasema wamelitaka shirika hilo kujitanua na kuzifikia kata zote 28 ili wapeleke elimu na kuwaeleza mangariba madhara ya ukeketaji.

"Lakini tunatoa pia kipaumbele kwa mangariba wapate shughuli za kufanya zitakazowaingizia kipato," anasema.

#### VIKUNDI

Mkurugenzi huyu anasema kwamba katika halmashauri hiyo kuna vikundi vimeundwa ambavyo vinapewa mikopo na miongoni ni vikundi vya mangariba ambao kupitia mikopo hiyo wanafanya miradi ya kuwaingizia kipato.

"Lakini tumeanzisha vilevile mpango wa kuwakagua watoto wanapozaliwa na wanapopelekwa kliniki na wanapobainika kukeketwa, wazazi huchukuliwa hatua za kisheria," anasema.

---

## JIELIMISHE

# Nyangumi na wanyama wengine walivyotumiwa kufanya ujasusi

SHERIA moja ya upelelezi ni kuwa "Usijionyeshe kuwa jasusi."

Nyangumi wa beluga, iwapo hilo ndio jina lake ambaye anapatikana katika bahari ya Norway, alitumika sana katika eneo hili lakini alionekana kufanya makosa mara nyingine.

Sababu ambayo amekuwa akisababisha tashwishi miongoni mwa wavuvi wa Norway na wanasayansi ni kwamba alikuwa akivalia kamba na lebo ilionyesha kwamba anatoka St. Petersburg nchini Urusi. Urusi imekana kufanya makosa hayo na kufikia sasa, nyangumi huyo amekataa kuzungumza.

Licha ya ukweli huo, ni wazi kwamba si mara ya kwanza wanyama kutumiwa kufanya upelelezi.



Ndege ni moja ya viumbe waliotumika katika ujasusi. **PICHA: MTANDAO**

#### PAKA

Iwapo kuna kitu kimoja tunachojua kuhusu paka, ni kwamba wao hufanya chochote wanachotaka na wakati wowote ule. Kwa hakika, wao huwezi kuwadhania kufanya jambo baya na ndipo sasa shirika la Ujasusi la Marekani (CIA), lilifikiria wanaweza kuwa wapelelezi wazuri sana.

Mwaka 1960, inakadiriwa takriban dola za Marekani milioni 14 zilitumika katika mradi wa kuweka vifaa vya kusikiliza ndani ya paka.

Lengo kuu lilikuwa kuingia kila mahali ili kuweza kukusanya ujasusi wa Urusi.

Lakini mpango huo haukufua dafu katika siku ya kwanza, wakati paka huyo alipogongwa na gari nje ya ubalozi wa Urusi mjini Washington na kufariki.

#### MABOMU YA POPO

Popo ni ndege watulivu na wao huendelea na opereshenі zao wakati wa usiku huku wakiishi katika maeneo fiche kama vile mapango. Ikiwa ni vigezo vizuri kwa mpelelezi yeyote na njia nzuri ambayo Marekani huitumia.

Wakati wa vita vya pili vya dunia, daktari mmoja wa meno alipendekeza kuwawekea vilipuzi vidogo wanyama hao.

Lengo lilikuwa kuviangusha katika miji ya Japan ili kuchoma nyumba kabla ya kulipuka na kusababisha moto mkubwa. Majaribio kadhaa yalifanywa, ikiwemo kuchoma anga la ndege, lakini wazo hilo halikufaulu.

#### VIFAA VYA KUSIKILIZIA

Juhudi zimefanywa kuunda nzi kuwa wapelelezi.

Mwaka 2008 jarida la new science liliripoti vile ambavyo idara ya ulinzi nchini Marekani, ilijaribu kutengeneza nzi bandia wenye nyaya ndani yake ili kudhibitiwa.

Uwezekano huo ulikuwa unafurahisha, ilikuwa fursa ya kurusha vifaa vidogo vya kusikiliza katika eneo la adui yako. Miradi kama hiyo imejaribiwa, huku ikiwa na ufanisi tofauti, kwa kushirikisha papa, panya na njiwa.

Huku teknolojia ikizidi kupiga hatua, lengo sasa ni kuunda vifaa vinavyosikiliza na vinavyofanana na wadudu wadogo.

#### NJIWA NA POMBOO

Matumizi ya wanyama katika ujasusi yamefanyika kwa miaka kadhaa kupitia njiwa waliotumwa kuwasilisha ujumbe katika vita vya dunia vya kwanza ama hata kupitia matumizi ya pomboo waliotumiwa na mataifa kama vile Marekani, Urusi na Israel ili kufanya upelelezi chini ya maji.

Lakini unaweza kufikiria wanyama ambao wamekamatwa kwa bahati mbaya na adui.

Mwaka 2007, Jeshi la Iran lilikamata kundi moja la chindi 14 waliokutwa katika kinu cha kutengeneza nyuklia.

UTAFITI

# Kwa nini India inachukulia ngono kwa ahadi ya kuoa ni ubakaji?



Wapenzi nchini India. **PICHA: MTANDAO.**

IWAPO mwanamume atashindwa kutimiza ahadi ya kumuoa mwanamke, ngono baina ya wapenzi wawili walioelewana inaweza kuchukuliwa kama ubakaji?

Mahakama ya ngazi ya juu zaidi nchini India, imetoa jibu la swali hilo na kusema kuwa ni "ndio."

Katika uamuzi muhimu, Mahakama imepitisha uamuzi wa Mahakama ya Awali na kumtia hatiani daktari mmoja kwa kosa la ubakaji katika Jimbo la Kati la India la Chhattisgarh.

Hiyo ni kwasababu alikuwa na makubaliano ya uhusiano wa kingono na mwanamke baada ya kumuahidi kuwa atamuoa, lakini hakutimiza baadaye ahadi hiyo na kumuoa mtu mwingine.

Majaji L Nageswara Rao na MR Shah walisema mwanamke alimruhusu daktari kufanya naye ngono kwasababu aliamini kwamba alikuwa na lengo la kumuoa kwa hiyo haiwezi kuchukuliwa kuwa alimruhusu kufanya tendo la ngono kwa hiari.

Bado India ni taifa lenye itikadi za kihafidhina linapokuja katika suala la ngono na mambo yanayohusu jinsia kwa ujumla. Mabikra huzawadiwa na mwanamke anayejulikana kuwa aliwahi kufanya tendo la ngono nje ya ndoa, huwa inakuwa vigumu kwake kuolewa.

Majaji walisema kwamba mshtakiwa alikuwa na "lengo la wazi" la kutomuoa, na kuongeza kuwa "tendo la ngono linalofanyika bila dhana halisi, haliwezi kuchukuliwa kama hiari."

Hata hivyo, Mahakama ilipunguza kifungo cha miaka 10 alichokuwa amefungwa na Mahakama ya Mwanzo na kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 7 jela.

Majaji wamesema kwamba "ni lazima akabiliwe na athari za uhalifu alioutekeleza."

Hii si kesi ya kwanza kwa mujibu wa data za serikali za mwaka 2016.

Polisi walirekodi kesi 10,068 za aina hiyo za ubakaji "zinazofahamika kama za waathiriwa wa ahadi ya kuolewa." Mwaka 2015, idadi ya kesi hizo zilikuwa ni 7,655.

Majaji wa Mahakama ya Juu zaidi ilishauri Mahakama za Mwanzo "kuchunguza kwa makini ikiwa kweli mwanamume aliahidi kumuoa muathiriwa au kulikuwa na njama nyingine tangu mwanzo na kwamba alifanya tendo la ngono kwa lengo tu la kuridhisha nafsi yake."

Hii ina maana kuwa kama mwanamume atathibitisha kuwa kweli alitaka kumuoa mwanamke lakini akabadili nia hiyo baadaye, bado haitakuwa ubakaji.

Haichukuliwi kama ubakaji ikiwa itabainika kuwa alikuwa na njama mbaya tangu mwanzoni mwa mahusiano yao.wLakini kama kweli tendo hilo lilifanyika kwa "lengo fulani" si rahisi kuthibitisha, na uamuzi huachiwa majaji na pia kuna hofu kuwa sheria hiyo inaweza kutumiwa isivyotarajiwa.

Na ukweli ni kwamba, kutokana na idadi kubwa ya kesi hizo, Jaji Pratibha wa Mahakama ya Juu ya Delhi, alisema mwaka 2017 kuwa wanawake hutumia sheria za ubakaji wakati wanapokuwa na mahusiano mabaya ya ndoa.

Jaji anasema hii inahitaji kuwapo na mipaka ya wazi kati ya ubakaji na ngono ya makubaliano, hususan wakati ambapo malalamiko ni kwamba mwanamke aliahidiwa kuwa ataolewa.

Wahindi wengi wanaamini kwamba sheria za ubakaji, hazipaswi kutumika kudhibiti mahusiano ya kujamiiana, hususan katika matukio ambapo wanawake wana wakala na wanaingia katika mahusiano kwa utashi wao.

Wengi katika Mahakama pia wanaonekana kuwa na maoni sawa na haya na kwa kiasi fulani inaelezea ni kwanini idadi ya watu wanaopatikana na hatia kwa kosa hili huwa ndogo na katika kesi nyingi mshtakiwa huondolewa mashtaka.

Mengi kati ya malalamiko ya ubakaji wa kutelekezwa na wapenzi wanaowaahidi kuwaoa hutoka katika familia maskini katika maeneo ya vijijini

Mnamo mwaka 2016, Mahakama Kuu ya Bombay ilisema kuwa mwanamke msomi mtu mzima ambaye alikuwa na mahusiano ya ngono ya kukubaliana, baadaye hawezi kudai amebakwa uhusiano unapokuwa mbaya.

Wakili wa ngazi ya juu na mwanaharakati mwenye makao yake Mumbai, Flavia Agnes, hata hivyo anadai kuwa kile tunachopaswa kukikumbuka ni kwamba mengi kati ya malalamiko haya hutoka katika familia maskini na wanawake kutoka jamii zenye matatizo katika maeneo ya vijijini.

Anasema wanawake hao mara nyingi hulaghaiwa kuingia katika mahusiano ya ngono na wanaume wanaowapa ahadi za uongo za kuwaoa na baadaye kuwatelekeza mara wapatapo ujauzito.

Aliongeza kuwa chini ya mfumo wa sasa wa sheria, sheria ya ubakaji huenda ndio inayoweza kuwasaidia kudai uharibifu au hata kupewa haki yao.

Ndio maana anapendekeza kuwa kipengele cha kutengana chini ya sheria ya ubakaji cha kukabiliana na kesi hizi kitumike badala ya adhabu kali za jela ambapo mwanamume anayepatikana na hatia ya kumlaghai mwanamke anaweza kulipa faini, na kuwajibishwa kwa malezi ya mtoto atakayezaliwa. **BBC**

## JE, WAJUA?

## Maisha ya kasuku asiye wa kawaida



Kasuku ajulikanaye kwa jina la Freddy Krueger, ambaye si wa kawaida kutokana na matendo yake. **PICHA: MTANDAO.**

ANAJULIKANA kwa jina la Freddy Krueger na kimsingi si kasuku wa kawaida.

Na sio kwasababu alifanikiwa kurudi nyumbani katika bustani ya wanyama Cascavel huko Kusini mwa Brazil, siku tatu baada ya kuibwa na wezi waliojihami kwa bunduki. Lakini pia kwa sababu alikutwa katika kizimba alimokuwa akiishi miaka minne iliyopita.

Kasuku huyu aliibwa wakati akipata matibabu kutokana na kile wahudumu katika bustani hiyo wanasema baada ya kuumwa na nyoka ambapo alivuja damu nyingi nusura ya kufa.

Usishangae kuna mengi zaidi ya hayo kama inavyobainishwa hapa chini:

Kwamba kabla ya kuanza kuishi katika bustani hiyo, aliishi katika ngome ya walanguzi wa dawa za kulevya.

Alipewa jina la Freddie Krueger ambalo ni la muigizaji katika filamu ya kutisha na pia kutokana na sura yake kuharibika mnamo mwaka 2015, baada ya kupigwa risasi usoni wakati wa operesheni ya polisi.

Kasuku huyo alipoteza uwezo wa kuona kupitia jicho lake la kulia na sehemu ya mdomo wake ilivunjika kutokana na jeraha hilo.

Aidha, huenda si jambo la kushangaza kwamba kasuku huyo hakuwa na urafiki pale alipoibiwa.

Pamoja na hayo, majeraha yake hayakumzuia kuishi maisha kama ya kasuku mwingine.

Kwa mfano licha ya sehemu ya mdomo wake kuharibika, bado alikuwa anaweza kuchambua magamba ya njugu na kula matunda. Polisi wanaamini kwamba huenda Freddy aliachwa huru na wezi baada ya kugundua majeraha yake.

"Huenda ingekuwa ngumu kumuuza, na pengine angetambulika kwa urahisi kwasababu ni rahisi kumtambua Freddy," anasema Ilair Dettoni, msimamizi mkuu wa bustani hiyo ya wanyama kwa BBC.

### BIASHARA YA WANYAMA

Usafirishaji haramu wa wanyama ni mojawapo ya biashara haramu zenye faida kubwa nchini Brazil.

Wataalamu kutoka shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na masuala ya biashara haramu ya wanyama (Renctas), wanakadiria kwamba biashara hiyo ina thamani ya dola za Marekani bilioni tatu kwa mwaka nchini humo

Msimamizi huyo anasema wamegundua damu ya binadamu karibu na kituo cha afya alichokuwa akipokea matibabu kasuku huyo anayoamini ni ushahidi kwamba aliwashambulia wezi hao.

### MATUMAINI YA KUPATA WAGENI ZAIDI

Kutekwa kwa Freddy si tukio la kwanza linalohusisha wanyama katika mji huo wa Cascavel.

Mamba na kasuku wengine pia wamewahi kuibwa kutoka katika bustani hiyo kwasababu ya kutokuwa na fedha za kutosha za kuweka mfumo thabiti wa ulinzi.

"Pengine masaibu ya Freddy yatawafanya watu watake kufahamu zaidi kuhusu shughuli za bustani hiyo ya wanyama na tunakaribisha wageni zaidi," anakiri Dettoni. **BBC**

TEKNOLOJIA

NA ELIZABETH ZAYA

# Ujenzi miundombinu wanyanyua taaluma Mlowa, Lyamkena Njombe

• Mchango wa TASAF wazisaidia sekondari hizo

UPUNGUFU wa vyumba vya madarasa pamoja na mabweni ya kulala wanafunzi ni miongoni mwa changamoto zinazozikabili shule nyingi nchini.

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutatua changamoto hizo kwa mustakhabali mzima wa ubora wa elimu inayotolewa kwa watoto wa Kitanzania na hivyo ustawi wa jumla wa taifa.

Kama ilivyo kwa mikoa mingine, mkoa wa Njombe una baadhi ya shule zinazokabiliwa na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa, ukosefu wa mabweni na nyumba za walimu, hivyo kuathiri wanafunzi na walimu kwa kiasi kikubwa.

Shule za Sekondari za Mlowa na Lyamkena zilizopo katika Kata ya Mlowa, Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe ni miongoni mwa shule zinazokabiliwa na changamoto hizo pia.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mlowa, Raymond Kyando, anasema shule hiyo ilianzishwa mwaka 2014 ikiwa na wanafunzi 52 na madarasa matatu.

Hata hivyo, anasema ilipofika mwaka 2015 walibaini maendeleo ya wanafunzi kitaaluma hayakuwa ya kuridhisha, mojawapo ya sababu ikiwa ni baadhi yao kuishi katika makazi ya kupanga nje ya shule yaliyokuwa mabovu.

"Tulilazimika kufanya ukaguzi katika makazi yao mwaka 2015 kwa kushirikiana na kamati ya shule, ndipo tuligundua wana changamoto kubwa ya usomaji," anasema na kuongeza:

"Makazi yao hayakuwa rafiki kwa maana mazingira waliyokuwa wakiishi kwa usomaji na tulipata kesi ya watoto wanne kupata ujauzito."

Kyando anasema walichukua hatua ya kuwashirikisha wazazi wa wanafunzi wakiwa kidato cha pili na wakakubaliana kuanzisha kambi ya kuishi wanafunzi.

"Walikuwa wanaishi shuleni wakilala katika madarasa, huku wakisimamiwa na viongozi wa shule," anasema na kuongeza:

"Mwaka huo tulipata matokeo mazuri ya ufaulu na kesi za utoro zilipungua tofauti na ilivyokuwa wakati wanafunzi wakitokea nyumbani."

## HOSTELI

Anasema mwaka 2016 kupitia bodi ya shule walianzisha hoja ya kufanya harambee ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi baada ya kugundua kwamba wakiwa katika mazingira ya shule, muda mwingi walikuwa wanafanya vizuri kitaaluma.

Mwalimu Mkuu anasema walifanikiwa kufanya harambee na kupata kiasi cha fedha ambacho walianza kuchimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo.

Hata hivyo, anasema waliishia njiani kwa sababu wazazi hawakuchangia tena pesa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi waliouanzisha.

## TASAF

Kyando anabainisha kuwa mwaka 2016 kuelekea 2017, TASAF iliwatembelea na kujionea mazingira ya miundombinu ya shule hiyo yasivyoridhisha.

Anasema kwa maombi ya uongozi wa shule pamoja na wazazi, TASAF ilikubali kuwasaidia kuwajengea madarasa, nyumba za walimu, mabweni na vyoo kupitia miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Anabainisha mwaka huo huo wa 2017 ndipo TASAF ilipoanza ujenzi huo na kuukamilisha mwaka 2018.

"Kufikia Oktoba Mosi 2018, wanafunzi wa kidato cha nne walianza kutumia hosteli hizo, kwa sababu walikuwa wanajiandaa na mitihani ya Taifa," anasema na kuongeza:

"Ilikuwa msaada mkubwa kwetu kwani ulitusaidia kuwaweka wanafunzi katika mazingira salama hasa katika kipindi hicho muhimu cha mitihani ya taifa kwao."

Kyando anasema baada ya kidato cha nne kumaliza mitihani, waliwahamishia wanafunzi wa vidato vingine katika hosteli hizo.

"Kwa hiyo tangu wanafunzi wahamie hosteli, hatuna kesi za utoro wala mimba... hivyo hosteli kwetu sisi ni msaada mkubwa wa kujenga mazingira bora ya kitaaluma kwa kuzingatia mazingira wanayotoka wanafunzi," anasema.

## NYUMBA ZA WALIMU

Anabainisha mbali na changamoto ya hosteli, pia shule hiyo ilikuwa na changamoto ya uhaba wa nyumba za walimu na kwamba TASAF imesaidia kujenga nyumba tatu za walimu pamoja na jengo la utawala na ofisi za walimu.

"Nimezungumzia hosteli kwa upande wa wanafunzi, lakini pia katika hii shule kuna jumla ya walimu 20, wa kiume 14 na wa kike sita... hakuna nyumba shuleni, tunapanga mtaani tena ni mbali na maeneo ya shule, zaidi ya kilomita 15," anasema na kuongeza:

"Kwa hiyo tulipokaa katika vikao vya wazazi, tuliona kwamba kunahitajika nyumba za walimu lakini pia na jengo la utawala kwa sababu tulikuwa tunatumia darasa kwa ajili ya ofisi ya walimu... kwa hiyo tuliwaomba pia TASAF wasaidie kwa hili na wakakubali."

Kyando anasema kuna uhitaji wa nyumba 20 za walimu katika shule hiyo na kwamba katika kipindi ambacho wanasubiri kupata nyumba zote zinazohitajika, watazitumia vizuri walizojengewa na TASAF.

"Kwa sababu nyumba ziko tatu na kila moja ikiwa na vyumba vitatu vya kulala, hivyo nimepanga nyumba moja kuweka walimu ambao hawajaoa ili walau kila mmoja apate chumba kimoja cha kulala," anasema na kuongeza:

"Na nyumba moja nzima moja miongoni mwa hizo, nitaweka mwalimu mmoja mwenye familia... kwa hali hiyo walimu kama saba watakuwa wamepata mahali pa kukaa... nitabaki nahangaikia walimu waliobaki." anasema.

## TASAF

Kwa upande wake, Ofisa Mfuatiliaji wa Miradi ya TASAF katika Halmashauri ya Mji wa Makambako na Wanging`ombe, Edwin Mlowe, anasema mbali na kuwa na miradi inayolenga kaya maskini, pia wamekuwa wakiboresha miundombinu ya shule.

"Kwa hiyo tukipata fursa ya kifedha huwa tunajenga vyumba vya madarasa, majengo ya utawala, mabweni ya wanafunzi pamoja na kuboresha vyoo," anasema.

Mlowe anabainisha kuwa majengo yanayojengwa na TASAF huwekewa kila kitu cha ndani ikiwamo samani, mfumo wa maji na umeme katika kila darasa.

## SEKONDARI YA LYAMKANA

Mbali na shule ya Sekondari Mlowa, Mlowe anasema pia TASAF wamejenga madarasa mawili, ofisi ya walimu pamoja na matundu nane ya vyoo kwenye Shule ya Sekondari ya Lyamkana.

Mkuu wa Shule hiyo, Sebastian Simtitu, anasema kwa kipindi kirefu wamekuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na kwamba wamekuwa wakishirikisha kamati za shule mara kwa mara kutafuta mbinu za kutatua changamoto hiyo.

"Tumekaa vikao vingi na wazazi pamoja na kamati ya shule kwa ajili ya kutafuta mbinu mbadala za kutatua changamoto hii... tuliendesha harambee na kufanikiwa kupata pesa ambayo ilituwezesha kujenga madarasa mawili, lakini hayakuwa yakitosheleza," anasema na kuongeza:

"Mwaka 2016 tulitembelewa na TASAF na tukawaomba watusaidie kujenga madarasa na baada ya tathmini yao waligundua kweli tulikuwa na uhitaji...mbali na madarasa, wametujengea ofisi ya walimu na vyoo, wakiweka kila kitu ndani yake."



Baadhi ya nyumba za walimu zilizojengwa kwa msaada wa TASAF, Shule ya Sekondari Mlowa.
**PICHA: ELIZABETH ZAYA**

> Kwa hiyo tukipata fursa ya kifedha huwa tunajenga vyumba vya madarasa, majengo ya utawala, mabweni ya wanafunzi pamoja na kuboresha vyoo.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Wadau wanajadili

WAKATI wanafunzi wakielekea kwenye Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita, nini kifanyike kuwajengea moyo wa kujiamini ili wasikubali kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo?



**LEONARD MBANGILE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

WENGI wetu tumepitia shule ingawa pia inawezekana wapo wachache ambao kwa sababu moja au nyingine hawakubahatika kusoma. Kuhusu udanganyifu wa mitihani, huu umekuwa ni kama jambo la kawaida kutokana na ukweli kwamba umekuwa ikiripotiwa kutokea katika shule mbalimbali na kusababisha baadhi ya wanafunzi kufutiwa matokeo.

Kimsingi kuna mbinu nyingi za udanganyifu zinazotumika kwa lengo la kusaidia wanafunzi kufaulu au kuzifanya shule husika kuwa na sifa ya kufaulisha wanafunzi wengi na kumbe nyuma ya pazia kuna udanganyifu unafanyika, ukiwamo wa kuiba mitihani na kuwapa majibu wanafunzi. Kwa kifupi kuhusu swali lako kuwa nini kifanyike kuwajengea wanafunzi moyo wa kujiamini ili wasikubali kufanya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa wanapoelekea kwenye mtihani wa kumaliza kidato cha sita, jibu ni kwamba wasitegemee njia ya mkato kwa ajili ya mafanikio.

Wanatakiwa kuzingatia kile ambacho wamefundishwa na kukifanyia kazi kwa vitendo, si kutafuta njia ya mkato kama hiyo ya kufanya udanganyifu ili kupata mafanikio. Wakumbuke kuwa maisha ya shule ni safari ndefu yenye changamoto nyingi. Ninaamini kwamba kwa mwanafunzi ambaye anatambua wajibu wake shuleni, hawezi kukubali kufanya upuuzi huo.

Vilevile watumishi wa umma, walimu na wamiliki wa shule ambao wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na mchezo huo mchafu, waache kuharibu wanafunzi kwa tamaa yao ya kutaka pesa au shule zao zionekane zinafundisha vizuri na kumbe hakuna lolote.



**JOSEPH MAUMA (MKAZI WA ARUSHA)**

KUHUSU swali lako kuwa nini kifanyike kwa lengo la kuwajengea wanafunzi moyo wa kujiamini na kukataa kufanya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa wanapoelekea kwenye mtihani wa kumaliza kidato cha sita, mimi ninasema kuwa waumize vichwa kwa kusoma sana vitabu.

Watumie muda mwingi kusoma sana, siyo kubuni mbinu za kufanya udanganyifu kwani hazitaweza kuwasaidia katika maendeleo yao kwenye elimu. Najua kwamba ukuaji wa teknolojia kwenye zama hizi umekuwa ni tatizo linaloendelea kupanuka siku hadi siku likihusisha vitu mbalimbali kama vile saa, miwani, vitu vya kuchomeka kwenye masikio ili kuwasiliana na mtu wa nje ya chumba cha mtihani na kadhalika.

Binafsi ninaamini kwamba bado kuna uwezekano mkubwa wa kukomesha udanganyifu kwenye mitihani. Hivyo mamlaka ziendelee kubuni mbinu mbalimbali zitakazosaidia kumaliza kabisa tatizo hili kwenye elimu. Baadhi ya shule zimekuwa na mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani ikiwamo kuanzisha kambi za taaluma, matokeo tumekuwa tukiyasikia kuwa wanafanya vizuri.

Siyo vibaya shule zote kuiga mbinu hiyo kuliko kutegemea udanganyifu. Mtindo huo wa kufanya udanganyifu umekuwa ukiharibia wanafunzi wanaojitahidi katika masomo na kujikuta wakifutiwa matokeo kwa pamoja kwasababu ya watu wachache walioshiriki udanganyifu. Umefika wakati sasa wa kutafuta mbinu za kudumu za kumaliza tatizo hilo kwa kuelimisha wanafunzi juu ya madhara ya udanganyifu na siyo kusubiri hadi ufanyike.



**JUMA HAMIS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SEKTA ya elimu inakabiliwa na changamoto nyingi sana, labda nigusie hili la uhaba wa walimu ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kusababisha kuwepo kwa hayo mambo ya udanganyifu wa mitihani, lakini kabla ya kuendelea, niseme kuwa sina maana ya kuhalalisha vitendo hivyo.

Nikirejea katika kile ninachotaka kuzungumza, ni kwamba inawezekana uhaba wa walimu unachangia wanafunzi kutofundishwa masomo yote vya kutosha na hivyo kusababisha waingie kirahisi katika mtego wa kufanya udanganyifu kwenye mitihani ili wafaulu.

Kama hilo lina ukweli ndani yake, basi serikali ijitahidi kuajiri walimu wa kutosha, kuongeza vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuboresha miundombinu ya shule na pia kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa masomo yote na tena kwa uhakika, lakini kikubwa zaidi ikiwa ni upatikanaji wa chakula shuleni, ili kuongeza ujifunzaji na ufaulu.

Hata hivyo, masuala hayo yasiwe ya serikali tu bali wadau wote wa elimu washirikishwe na pia jamii ielimishwe kuhusu umuhimu wa kuwajenga watoto katika maadili mema kwani ndio wanaotarajiwa kuwa viongozi wa baadaye. Hivyo ni jambo muhimu kuwajenga katika misingi ya kweli, uwajibikaji na kujituma kuliko kutegemea wizi wa mitihani ndipo wafaulu.



**SIMEO MATIKO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SERIKALI imekuwa ikifanya jitihada kubwa na kuwekeza fedha nyingi kuhakikisha mitihani inafanyika kama ilivyopangwa.

Lakini pamoja na jitihada hizo, bado mitihani hii imekuwa ikigubikwa na changamoto mbalimbali ikiwamo udanganyifu au wizi wa mitihani.

Hali hiyo ya kujirudia mara kwa mara kwa udanganyifu huo ni dalili tosha kwamba huenda ufumbuzi wa tatizo hilo bado haujapatikana. Matukio ya aina hii siyo mazuri kwa mustakabali wa elimu yetu, kwani wanafunzi wanaofaulu kwa kuiba mitihani hawafai kwa maendeleo ya taifa.

Hivi watendaji wanaojihusisha na udanganyifu huo wanapata wapi ujasiri huu? Ninaweza kusema kuwa udanganyifu wa mitihani ni ishara kwamba wanafunzi hawaandaliwi vyema shuleni hali inayosababisha walimu na watendaji kutafuta njia mbadala ili wanafunzi wafaulu.

Kufaulu kwa njia hizo siyo sahihi kabisa, waliozoea mtindo huo watafakari kisha wachukue hatua za kuwanusuru wanafunzi. Inashangaza kwamba baadhi ya shule ambazo watendaji wake wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na udanganyifu huo ni miongoni mwa zile zinazofanya vizuri katika mitihani ya taifa.

Hatua hiyo inatia shaka kama shule hizo zimekuwa katika nafasi hiyo kihalali au kwa kutumia udanganyifu.



**MWANAHAMISI ABADANI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KABLA ya yote ni muhimu kujua chanzo cha udanganyifu huo na ndipo tunaweza kupata jibu sahihi la kuwapa wanafunzi cha kufanya.

Kwanza kabisa kwa maana yangu, mtindo wa kutozingatia kile kinachofundishwa shuleni ndio unawafanya wanafunzi kujikuta wakiingia kwenye mtego wa kufanya udanganyifu kwenye mitihani ili waonekane wamefaulu vizuri na kumbe ni kwa njia ya wizi.

Mtindo huu ninaamini wapo baadhi ya wazazi na walezi wanachangia kuuendekeza kwa kuamini kuwa wanawasaidia watoto wao na kumbe wanawaharibu kitaaluma.

Hatua ambazo zimekuwa zinachukuliwa na serikali za kufuta matokeo ya mitihani na kuwachukulia hatua wahusika wote ni za kungwa mkono na zingetosha kuwa fundisho kwa wahusika za kuwafanya wazingatie masomo na kufaulu kihalali, kwani kurudia mitihani huna ninaona kwamba kunaweza kuwaathiri kisaikolojia wanafunzi.

Hivyo wale wanaojiandaa kufanya mtihani wa kidato cha sita wajiandae kwa njia halali na siyo kutegemea kuonyeshwa majibu ya mitihani, wasije kujikuta kwenye mkondo uleule wa kufutiwa matokeo.

Wanafunzi wazingatie kile ambacho wamekuwa wakifundishwa katika kipindi chote ambacho wamekuwa shuleni kuliko kusubiri kufaulu kimiujiuza.



HABARI MBEYA

# Washauriwa kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VITUO vya taarifa na maarifa vinavyotoa elimu ya jinsia kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia nchini (TGNP), vimeshauriwa kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia, uwajibikaji na utawala bora kwenye kata ambazo hazijanufaika na elimu hiyo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alipokuwa anazungumza na Nipashe kuhusu namna halmashauri yake inavyoshirikiana na TGNP kutekeleza bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

Alisema elimu ya ukatili wa kijinsia bado inahitajika kwenye jamii na kwamba kata ambazo hazijanufaika na elimu hiyo katika wilaya hiyo zinatakiwa zifikiwe na vituo kwa wahusika kuandaa utaratibu mzuri wa namna ya kuwasaidia wananchi.

Alisema kata zilizonufaika na elimu hiyo kama vile, Mshewe, Ijombe, Maendeleo, Itewe na Ifiga zimekuwa na mchango mkubwa katika kupiga vita ukatili wa kijinsia, lakini pia zimefanya jitihada za kujiletea maendeleo.

Alisema kata hizo zimejitahidi kuhamasisha shughuli za maendeleo hasa kuhimiza ukombozi wa mwanamke kiuchumi kwa kuhimiza na kujitolea katika ujenzi wa shule, zahanati na vituo vya afya.

"Sisi halmashauri tumeridhishwa na utendaji kazi wa vituo vya taarifa na maarifa hasa kwenye kata ambazo zimefikiwa, tumekuwa tukipokea taarifa mbalimbali za maendeleo na hata za wale wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia, tunahitaji kata zote katika halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zipate elimu hiyo ili kurahisisha shughuli za maendeleo," alisema Kisemba.

Aidha, Kisemba alisema katika kufanikisha suala hilo, halmashauri kupitia vikao vyake vya Baraza la Madiwani vitajadili na kupitisha azimio la kuviruhusu vituo hivyo kutoa elimu kwa kupewa kibali maalum.

Mwenyekiti wa vituo vya taarifa na maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, aliishukuru halmashauri kwa kutambua mchango wao na kuahidi kutoa elimu hiyo kwenye kata ambazo bado hazijanufaika.

**"Sisi halmashauri tumeridhishwa na utendaji kazi wa vituo vya taarifa na maarifa hasa kwenye kata ambazo zimefikiwa, tumekuwa tukipokea taarifa mbalimbali za maendeleo na hata za wale wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia, tunahitaji kata zote katika halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zipate elimu hiyo ili kurahisisha shughuli za maendeleo," alisema Kisemba.**

# Shahidi aeleza mahakama alivyoitwa kutambua mbegu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, imeendelea kusikiliza mashahidi upande wa mashtaka katika kesi ya kuzalisha na kuuza mbegu kinyume cha sheria, inayomkabili mfanyabiashara wa pembejeo za kilimo jijini Mbeya, Fortunatus Lutekinikwa.

Hakimu Mkazi, Paul Ntumo anaendelea kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka, shahidi wa kwanza, Naomi Mlowe ambaye ni Ofisa Masoko wa kampuni inayozalisha Mbegu ya Beula.

Aliiambia mahakama kuwa alipigiwa simu Januari 31, mwaka huu na Ofisa wa Polisi kutoka Kituo Kikuu cha Kati kuwa anahitajika kufika Uyole kwenye duka la Fortunatus Lutekinikwa ili kuzitambua mbegu ambazo zinatiliwa shaka baadhi zikiwa na vifungashio vya kampuni yao.

"Baada ya kufika dukani kwa Mfanyabiashara huyo niliwakuta askari, maofisa wa TOSCI na mtuhumiwa na katika upekuzi wa duka lake walibaini kuwapo kwa mbegu zenye vifungashio vya kampuni ya beula," Naomi aliiambia mahakama.

Alidai alibaini Mfuko wa Mbegu ambazo hazikuzalishwa na kampuni yao, licha ya vifungashio kuwa vyao, lakini pia mbegu hizo zilikuwa hazina sifa za kuuzwa.

Shahidi mwingine kwa upande wa mashitaka ambaye ni askari mpelelezi wa Polisi Kituo Kikuu cha Kati jijini Mbeya, Allan Kivamba, aliiambia mahakama kuwa aliletewa jalada na mkuu wake Januari 31, mwaka huu ili kumhoji Fortunatus Lutanikwa ambaye anatuhumiwa kuzalisha na kuuza mbegu bila kibali cha mamlaka husika.

"Kabla ya kuchukua maelezo ya mtuhumiwa nilimweleza haki zake ikiwa ni pamoja na kuwapo mtu au wakili wakati wa kuchuliwa maelezo, mtuhumiwa alisema hakuna ulazima atatoa maelezo yeye mwenyewe bila kuwapo watu na alitoa maelezo yake na yalipokelewa kama kielezo cha nne katika kesi hiyo," alisema Afande Kivamba.

Akisoma mashtaka katika kesi hiyo, Mwanasheria wa Serikali, Mwajabu Tengeneza alisema mshtakiwa alikamatwa akiuza mbegu kinyume cha sheria ya mbegu namba 18 kifungu cha 13(1) na kifungu cha 26(1) na (2).

Mwajabu alisema mshtakiwa alikamatwa na maofisa wa ukaguzi wa mbegu kutoka TOSCI Januari 31, mwaka huu dukani kwake, akiwa na mbegu zisizoruhusiwa na kughushi vifungashio mbalimbali kinyume cha sheria kama DKS 80-33(1), Kenya seed H 628(14), Kibo H 614D(30),Pioneer B 30919 na, HYGENE Ashley(38),HYGENE(99) na HY-GENE OKRA(7).

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Mei 15, mwaka huu na upande wa mashtaka bado unaendelea kutoa ushahidi huku mshtakiwa akiwa nje kwa dhamana.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika migodi ya wachimbaji wadogo iliyo katika Kijiji cha Nyakafuru wilayani Mbogwe mkoani Geita. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na viongozi wa wachimbaji wadogo katika eneo hilo.

# Kodi mashine za EFD zawaliza wafanyabiashara

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAFANYABIASHARA mkoani Mbeya, wameishauri serikali kupunguza tozo za kodi kwenye mashine za kielekroniki EFD's ili watu wengi waweze kuagiza mashine hizo kutoka nje ya nchi na hivyo kurahisisha ulipaji wa kodi.

Ushauri huo ulitolewa jana na mfanyabiashara, Ally Richard, kutoka kampuni ya Ally Rich Sanaa Group, jijini Mbeya ikiwa ni Wiki ya Elimu kwa Mlipakodi.

Alisema ili kufikia azma ya serikali ya uchumi wa kati lazima iangalie kodi ambazo ni rafiki kwa wafanyabiashara.

Alisema baadhi ya tozo kwenye mashine za kielekroniki zimekuwa zikiwaumiza wafanyabiashara hali inayosababisha kukwepa kulipa kodi.

"Kumekuwa na utitiri wa kodi kwenye mashine za kielekroniki tunaomba TRA iliangalie upya suala hilo, wapo baadhi ya wafanyabiashara wana mitaji midogo wanashindwa kumudu gharama hizo, baadhi ya sheria ziangaliwe upya ili kila mmoja anufaike," alisema Richard.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha mfanyabiashara anakuwa mzalendo kwa kulipa kodi kwa wakati, TRA ijenge mazingira rafiki yenye ushawishi wa kulipa kodi.

Msaidizi Maalum wa Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Salum, aliwahakikisha wafanyabiashara kuwa wanaendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Alisema kwa umuhimu huo TRA walianza kuadhimisha Wiki ya Elimu ya mlipakodi ambayo ina lengo la kupata mrejesho wa masuala mbalimbali waliyoyaboresha na kusikiliza changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na kuzitafutia ufumbuzi.

Salum alisema elimu hiyo mkoani Mbeya itakuwa na tija kwa kuwa wafanyabiashara wote watapata elimu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa.

"Katika wiki hii ya elimu ya mlipakodi mamlaka tumedhamiria masuala kadhaa kutimia ikiwamo kuhakikisha kila mfanyabiashara nchini anapata elimu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari yake mwenyewe, lakini pia tunasisitiza kutanguliza uzalendo kwa manufaa ya kulijenga taifa letu," alisema Salum.

Aidha, Salum alisema mamlaka ya ukusanyaji mapato Tanzania imefanikiwa kuboresha miundombinu ya ulipaji kodi kupitia teknolojia ya mitandao ya simu ambayo imesaidia kuondoa ukiritimba na kodi kulipwa kwa wakati.





## Wamachinga wapewa angalizo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

AFISA masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabishara wadogo kuacha tabia ya kupanga biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi, ikiwamo kandokando na barabarani ili waweze kuepukana na ajali.

Tahadhari hiyo aliitoa wakati akizungumza na wafanyabiashara wanaopanga biashara zao kandokando ya barabara katika mitaa ya Uhindini kufuatia ajali ya gari na kusababisha kugongwa na kujehuriwa kwa wafanyabiashara wawili, waliokuwa wameweka biashara zao kandokando na barabarani.

Alisema biashara hizo sasa ni bora zikahamishiwa kwenye maeneo yalio rasmi kwa ajili yao ambayo Halmashauri ya Jiji iliwatengea.

'Upangaji huo wa biashara usio rasmi unaofanywa na wafanyabiashara hao (wamachinga) katika maeneo yasiyo rasmi umekiukwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za halmashauri ya jiji, ikizingatia kuwa wanahatarisha maisha yao na hata kwa wateja," alisema.

Alisema kuwa kwa mujibu wa mipango ya Halmashauri ya Jiji, yapo maeneo rasmi yaliyopangwa kwa ajili ya biashara na siyo barabarani.

"Kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Halmashauri ya Jiji, hivi sasa yapo maeneo mengi rafiki kwa shughuli za kufanya bishara ikiwamo kwenye masoko kama Bonanza, Soko Kuu la Majengo, Sabasaba, Chang'ombe na soko maalum la jioni Nyerere Square," alisema.

Alisema ni vema masoko hayo yakatumiwa kwa wafanyabiashara hao badala ya kuzagaa mitaani na barabarani ambako wanaweza kusababisha majanga ya ajali kwa watembea kwa miguu na wateja, hali ambayo inaweza kusababisha hasara kwa upande wao na serikali.

**"Kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Halmashauri ya Jiji, hivi sasa yapo maeneo mengi rafiki kwa shughuli za kufanya bishara ikiwamo kwenye masoko kama Bonanza, Soko Kuu la Majengo, Sabasaba, Chang'ombe na soko maalum la jioni Nyerere Square," alisema.**

# Jafo aja na mwarobaini ugonjwa pumu mashuleni

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Selemani Jafo, amezitaka halmashauri kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya visanduku vya huduma ya kwanza kwa ugonjwa wa pumu katika shule za msingi na sekondari nchini.

Jafo alitoa maagizo hayo baada ya maandamano ya kuadhimisha Siku ya Pumu Duniani.

Alisema tatizo la pumu ni kubwa na takwimu zinaonyesha nusu ya watu wenye pumu ni watoto ambao wengi wako mashuleni na hawana uwezo wa kujisaidia.

"Ukiangalia takwimu za Shirika la Afya Duniani zinasema vifo vinavyotokana na pumu nchini ni zaidi ya 2,000, sasa kama nusu ya hao ni watoto, hii inamaanisha tunapoteza shule mbili nzima," alisema na kuongeza:

"Yaani wanafunzi wa shule iliyokamili kutoka darasa la kwanza hadi la saba hii inaonesha tatizo hili ni kubwa na tunahaja ya kutathmini kama taifa."

Kutokana na hali hiyo, Jafo aliagiza halmashauri katika bajeti ya mwaka 2020/ 2021, zitenge Sh. 100,000 kwa kila shule katika eneo lake ili kununua visanduku viwili vya huduma ya kwanza kwa ugonjwa wa pumu.

"Ghamara ya first aid kit moja ya huduma ya kwanza kwa ugonjwa wa pumu ni Sh. 50,000, hivyo kila shule ikitengewa kits mbili haitakuwa fedha nyingi, hivyo kwa shule zote zaidi ya 17,000 kutenga Sh. bilioni 1.7 kwa hili sio fedha nyingi," alisema.

Jafo alisema jamii kubwa ya Watanzania haina ufahamu wa tatizo la ugonjwa wa pumu, dalili na namna ya kutoa huduma ya kwanza kwa mgonjwa wa aina hii, hivyo alitaka maadhimisho hayo kupewa kipaumbele na waganga wakuu wa mikoa na wilaya katika maeneo yao kuadhimisha siku hii kwa kutoa elimu katika jamii na mashuleni. Pia aliziagiza halmashauri na mipango miji kutenga maeneo kwaajili ya mazoezi ili kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Magonjwa ya Mfumo wa Hewa (TARD), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (Tancida), Dk. Digina Riwa, alisema takwimu za WHO zinaonesha dunia ina wagonjwa zaidi ya milioni 3, huku nusu ya wagonjwa hao ni watoto.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akikata utepe kuzindua ofisi mpya za kanda ya kati na duka la kisasa la Vodacom Tanzania jijini Dodoma. Kampuni hiyo imezindua makao yake makuu ya Kanda ya Kati ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Serikali kuhamishia shughuli zake mji mkuu. Wa pili kulia ni Naibu Waziri, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Anthony Mavunde na Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Kati wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Grace Chambua. **MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wawashtaki watendaji mafisadi

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

MADIWANI wa Halmashauri ya wilaya ya Chamwino, wamemwomba Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Athumani Masasi, kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wanaoiba mapato ya ushuru wa mazao walioopo kwenye vizuizi vilivyopo vijijini.

Ombi hilo lilitolewa na madiwani hao walipokuwa wakichangia kwenye kikao cha baraza la madiwani cha kujadili taarifa za utekeleaji za kamati za kudumu.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani wengine Mwenyekiti wa kamati ya fedha, uongozi na mipango, Samwel, alisema baadhi ya watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya ushuru wa mazao siyo waaminifu na hawana uchungu wa halmashauri hiyo.

"Tunakuomba Mkurugenzi wetu kuwa macho kwa watumishi hao wanaofanya kazi kwenye vizuizi ambao walipewa dhamana ya kukusanya ushuru, baadhi yao siyo waaminifu kwa upande wa fedha, na pia wanatuangusha hawa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Masasi amewataka watumishi wake kusimamia kwa uaminifu na uledi katika ukusanyaji wa vyanzo vya mapato kwa vitendo. Ili kuiongezea halmashauri mapato.

Alisema ili kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato, watendaji waliopewa dhamana wakasimamia kwa uaminifu vyanzo vyote vinavyoiingizia Halmashauri mapato ikiwamo kwenye ushuru wa mazao.

"Madiwani na watendaji inatubidi kuongeza kasi katika ukusanyaji wote wa vyanzo vya mapato, ili kufikia malengo ya juu zaidi. Hii inawezekana pale ambapo kila mtumishi atasimama kwenye sehemu yake kwa uaminifu," alisema.

Katika kikao hicho kamati mbalimbali zilipitisha bajeti zake za robo mwaka wa pili ya 2018/2019 Oktoba hadi Desemba ikiwamo ya fedha na mipango, ambayo ilikusanya jumla ya Sh. 16,705,663,412 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ambayo ni sawa na asilimia 43 ya makisio ya mwaka wa fedha.





# Ofisi ya Mufti yaanzisha chuo cha ndoa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Mufti Zanzibar, imeanzisha Chuo cha ndoa ambacho kitawawezesha wanandoa watarajiwa kupata elimu ya ndoa na kuzifahamu sheria zake ikiwamo haki za watoto, mke aliyeachwa kama kupewa kianzio cha maisha.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalim, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, Suleiman Sarhani, aliyetaka kujua maendeleo ya Chuo cha ndoa yamefikia wapi hadi sasa.

Akijibu waziri alisema Chuo cha ndoa kipo chini ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na malengo makuu ya kuanzishwa kwa chuo ni kutoa elimu ya ndoa kwa wanandoa watarajiwa kufunga ndoa na wale waliopo katika ndoa. Alisema tayari chuo kimeshapokea wanafunzi wanandoa watarajiwa katika kipindi cha muhula mitatu hivi sasa na wanafunzi hao wamehitimu mafunzo yanayotolewa na kukabidhiwa vyeti.

Alieleza kwamba serikali imeanzisha chuo hicho baada ya kujitokeza kwa tatizo la kuvunjika kwa ndoa ambalo limekuja kutokana na wingi wa talaka.

Alisema talaka zimekuwa zikitolewa kiholela na wanandoa kwa sababu wengi wao hawajui na hawafahamu maana ya ndoa, haki zinazopatikana kwa wanandoa katika kipindi cha maisha yao.

''Tumefahamu kwamba watu wengi wanaingia katika ndoa bila ya kujua nini ndoa, haki zinazopatikana kwa wanandoa katika kipindi chote ikiwamo ndoa inapovunjika,'' alisema.

Hata hivyo, aliitaka jamii kujenga tabia ya ustahamilivu na kuvumiliana ili kuweza kudumisha ndoa zao.

Akijibu swali la nyongeza kuhusu tatizo la kuvunjika kwa ndoa, alisema kuna baadhi ya wanaume kunapotokea migogoro katika ndoa hukosa uvumilivu na kusababisha ndoa kuvunjika.

"Katika maisha ya ndoa kunahitajika ustahamilivu ...tusipokuwa wastahamilivu ndoa zetu hazitodumu, serikali inajitahidi kutoa elimu ili kuzinusuru ndoa kutovunjika," alisema.



Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif (kushoto), akibadilishana mawazo na Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, Shekhe Hamad Mantar, nje ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yasema watalii wa Israel wamepungua

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, imesema kuna upungufu mkubwa wa idadi ya wageni kutoka nchini Israel ambao huja kufanya utalii Zanzibar.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo Chum Kombo Khamis, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid.

Alitaka kujua kamisheni ya utalii imeweza kubaini sababu gani hasa za watalii kutoka Israel wasije kwa wingi Zanzibar, Naibu waziri huyo alisema kamisheni ya utalii haijabaini sababu gani hasa iliyofanya watalii kutoka Israel wasije kwa wingi Zanzibar.

Naibu waziri Chum alisema kuwa kwa sasa wizara yake imeshaanza kufanya mazungumzo na Balozi wa Israel kuhakikisha uingiaji wa wageni hao unarudi kama ilivyokuwa awali.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alisema mwaka 2018 wamevuka lengo lililopangwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lengo lilikuwa kupokea watalii 50,0000 na wameweza kupokea watalii 5,20389 lengo hilo liliwekwa hadi kufikia mwaka 2020.

Waziri huyo alilazimika kujibu swali hilo baada ya Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Yahya Ahmada Abdullwakil, alipouliza swali la nyongeza na kutaka kujua kupungua kwa idadi ya watalii kutoka Israel hakutoathiri lengo la serikali la kupokea watalii 50,000 kwa mwaka.

Alieleza kuwa licha ya kwamba watalii kutoka Israel kupungua, lakini watalii kutoka nchi zingine wameongezeka na kufidia kuanguka kwa watalii kutoka Israel kutokana na ulinzi na usalama wa kimataifa.

"Tunaamini kuwa na mwaka huu pia tutavuka lengo la kupokea watalii wengi zaidi, kutokana na uimarishaji wa ukusanyaji wa takwimu za watalii," alisema.

# Sababu ya minazi kupungua yaelezwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imesema kuwa minazi mingi imetoweka Zanzibar kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi ikiwamo ujenzi na utengenezaji wa vitu vya samani.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ali Ussi, alisema kwa mujibu wa sensa ya miti ya mwaka 2013 imeonyesha kuwa kutoka mwaka 1997 hadi 2013 minazi imepungua kutoka 3,317,600 hadi 1,255,000 kwa Unguja na Pemba kutoka 1,888,000 hadi 1,044,000.

Aliyaeleza hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, Ali Suleiman Shihata, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kutoa miche ya minazi kwa wakulima ili kurudisha kwa wingi zao hilo kutokana na minazi mingi kukatwa.

Dk. Makame alisema hali hiyo ya kutoweka kwa minazi inatisha kwa kuwa kiwango cha upunguaji kinaathiri sekta nyingi ikiwamo uchumi wa nchi.

Alisema wizara yake kwa kuzingatia hilo kwa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 ilijipangia kuotesha jumla ya miche ya minazi 200,000 na imeweza kuotesha miche 86,631 Unguja na Pemba katika vitalu vya serikali kwa lengo la kuitoa kwa wakulima bila ya malipo ili kurejesha miti hiyo ambayo ni muhimili mkubwa wa kiuchumi na kijamii kwa Zanzibar.

Aidha, alisema kuwa uzalishaji huo utakuwa unaongezeka mwaka hadi mwaka na utakwenda sambamba na uhamasishaji wa wananchi ili kukidhi haja ya uboreshaji wa zao hilo.

Akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na mwakilishi huyo wa Jimbo la Kijitoupele, aliyetaka kujua ni sababu gani zilizokwamisha kushindwa kuotesha miche 200,000 kama lengo lilivyokusudiwa, Naibu waziri huyo alisema, sababu za kutofikia lengo ni kuchagua miche ya kuotesha na waliotesha miche ya minazi iliyobora ili nazi zitakazozaliwa kuwa nazi bora na nzuri.

"Ukiotesha miche ya minazi mibovu na mibaya hutoweza kupata minazi mizuri kwa hivyo moja ya tatizo lililojitokeza tulikuwa tukichagua sana nazi tunataka nazi kubwa sio vinazi vidogo vidogo," alisema.

Hata hivyo, alisema wanamkakati wa kusaka misumeno ya moto nyumba kwa nyumba ambayo imekua ikiathiri sana kwa kukata minazi.

# Wakurugenzi waonywa fedha za mfuko wa jimbo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imewaonya wakurugenzi wanaotumia fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), bila ridhaa ya mbunge ilhali mbunge ndio mwenyekiti wa mfuko huo.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alitoa onyo hilo bungeji wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Konde (CUF), Khatib Said Haji.

Mbunge huyo alisema kuna baadhi ya halmashauri hufanya matumizi ya fedha hizo bila ya kumshirikisha mbunge na mambo hayo hasa yapo upande wa Zanzibar, na kuhoji serikali inatoa kauli gani ili waache tabia hiyo.

Aidha alisema kwa upande wa Zanzibar mbunge baada ya kupitisha fedha hizo halmashauri hamshirikishi mbunge katika suala lolote tena. Alisema wajumbe wengine wa mfuko huo ni Madiwani wawili kwa kuzingatia jinsia, watendaji wawili wa kata au viti maalum, lakini na mtu mmoja anayetoka jimbo husika na katibu ni mchumi katika halmashauri husika.

Waitara alisema kama kuna fedha zinazotaka kutumika kwa vyovyote vile hata kama ni Mkurugenzi lazima afanye mawasiliano na mbunge kama mwenyekiti na kama hakuwapo maana yake mbunge ataridhia labda miongoni mwa wale madiwani ili aweze kufanya kazi hiyo.

"Miradi inapopitishwa mkurugenzi kazi yake ni kwenda kupitisha fedha ikatumike na sio kupanga kwamba ongeza au punguza hiyo haruhusiwi kabisa," alisisitiza Waitara. Alisema wamepata malalamiko karibu kwa wabunge wote, hivyo wakurugenzi wa halmashauri hawana maamuzi katika fedha hizo na fedha hizo zinaenda kwenye mgawo na wabunge ambao ni wenyeviti wenyewe wanajadili.

Alifafanua kuwa Mbunge anaweza akasema napeleka Sh. 500,000 hapa, hivyo mkurugenzi hawezi kubadilisha maamuzi hayo kwa kuwa ndio uwezo wake na ndio maana inaitwa fedha ya kuchochea maendeleo ya jimbo.

"Kwa wale wakurugenzi ambao wana tabia ya kutumia fedha bila mbunge tunaomba majina yao tutawashughulikia maana sheria imetaja vizuri namna ambavyo wanapaswa kufanya,"alisema Waitara. Alisema pia wameelekeza kuwa fedha zikipita kwenda kutumika ni lazima kamati ya mfuko wa jimbo iende kufanya ziara ikakague miradi hiyo kama imetekelezwa kwa kuwa hiyo fedha ni ya serikali ni lazima isimamiwe vizuri na sheria imeleekeza.

Baada ya majibu hayo wabunge walipiga makofi mengi, hali iliyomlazimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu Jenista Mhagama kusimama na kusema kuwa makofi hayo mengi yaanaashiria kuwa yapo matatizo kwenye uwezeshaji wa matumizi na mfuko wa jimbo kwenye majimbo yao.

"Nikuombe Mheshimiwa Spika, kuwa wabunge waiache serikali ikashauriane na waziri mwenye dhamana ikiwezekana itoe waraka wa maelekezo tena kusudi kila Halmashauri iweze kusimamia utekelezaji wa sheria ya mfuko huo pia wabunge wahakikishe matumizi yanafanyika kwa mujibu wa sheria," alisema Mhagama.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali kuwa haioni umuhimu wa kuongeza viwango vya fedha hizi ili kuleta ufanisi zaidi. Akijibu, Waitara alisema kuwa mfuko huo ulianzishwa kwa sheria ya bunge Na. 16 ya mwaka 2009 na kwamba lengo ni kuhakikisha miradi ambayo ni vipaumbele vya wananchi katika jimbo husika ambayo haikupata fedha katika bajeti inapata fedha za utekelezaji.

Alifafanua kuwa kwa tafsiri ya sheria iliyoanzisha mfuko, fedha za jimbo ni kwa ajili ya majimbo ya uchaguzi ambayo yameanzishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuzingatia ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waitara alisema kuwa Vigezo vinavyotumika kugawa fedha hizi ni ukubwa wa eneo, idadi ya watu, na kiwango cha umaskini. "Serikali imekuwa ikiongeza fedha hizi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ambapo mwaka wa fedha 2018/2019 iliongeza kiasi kinachotolewa kutoka Sh. bilioni 10 zilizokuwa zinatolewa kipindi cha nyuma mpaka Sh. bilioni 12.5 na itaendelea kuongeza kadiri ya upatikanaji wa fedha,"alisema Waitara.



Mchuuzi wa viazi, mihogo na magimbi akipanga bidhaa zake pembezoni mwa barabara eneo la Tandale jijini Dar es Salaam jana.Vyakula vya aina hii vimeshamiri katika masoko mengi, kutokana na mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Vijiji sasa kupata umeme

**Na Steven William, MUHEZA**

NGUZO mpya za umeme zimewasili wilayani Muheza kutoka katika kiwanda cha Mkumbara kilichopo wilayani Korogwe kwa ajili ya kusambaza Mradi wa Umeme Vijiji (REA) katika vijiji vitatu wilayani Muheza.

Hayo yalisemwa juzi na Injinia wa REA, Peter Komele, wakati akipokea nguzo hizo mpya katika eneo la mji wa Hale, wilayani Korogwe.

Komele alisema wamepokea nguzo 120 ambazo watazisambaza katika vijiji vya Mto wa Mbuzi, Songa Batini na Songa Kibaoni, wilayani Muheza.

Alisema nguzo hizo ni jitihada za Mbunge wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi Rajabu kuhakikisha zinapatikana ili vijiji 19 wilayani Muheza viweze kupata umeme na watu wapate maisha bora vijijini.

Komele alisema kuwa kazi ya kusambaza umeme vijijini wilayani Muheza ilichelewa kutokana na kampuni iliyopewa tenda ya kusambaza nguzo kuchelewa kupeleka kwa mkandarasi wa kampuni ya RADI.

Kwa upande wake diwani wa kata ya Mhamba, wilayani Muheza, Jofrey Kapiki, alisema anamshukuru mbunge huyo kwa kupigania kijiji chake cha Mto wa Mbuzi kufanikisha kupata umeme.

Alisema kijiji hicho kipo karibu na mtambo wa kuzalisha umeme wa Hale Power na wananchi wanalinda mitambo hiyo, lakini kijiji hicho kilikuwa hakina umeme.

Kapiki alisema alipofika Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, wilayani Muheza alitoa maagizo kuwa lazima kijiji hicho kipate umeme.

Naye Mbunge wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi aliwataka wananchi wasiwe na wasiwasi ya kupata umeme kwa kuwa vijiji na vitongoji vyote ambavyo havina umeme katika wilaya ya Muheza vitapata.

**Alisema kijiji hicho kipo karibu na mtambo wa kuzalisha umeme wa Hale Power na wananchi wanalinda mitambo hiyo, lakini kijiji hicho kilikuwa hakina umeme.**

# Wasiojiweza zaidi ya 500 wasaidiwa chakula

**Christina Haule, MOROGORO**

WATU wasiojiweza zaidi ya 500 wamepatiwa msaada wa vyakula vya futari kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE (AID) ukiwa ni muendelezo wa programu ya taasisi hiyo kusaidia jamii katika nchi mbalimbali ikiwamo ya Tanzania.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Amina Rashidi, mmoja wa wanufaika wa msaada huo, aliishukuru na kusema utamsaidia chakula na futari nyumbani kwa kuwa awali hakuwa na chakula chochote.

Awali akikabidhi msaada huo kwenye makao makuu ya Taasisi ya The Islamic Foundation, Kaimu Balozi wa UAE nchini, Mohamed Ibrahimu Albahry, alisema programu ya kutoa msaada wa futari itatekelezwa katika mikoa mingine ya Tanzania Bara na Visiwani, lengo likiwa ni kuwasaidia watu wasiojiweza wakiwamo wazee, walemavu, wajane na wenye mahitaji maalum.

Balozi Albahry alisema mbali na kutoa misaada ya vyakula, UAE AID imechimba visima vitano katika taasisi mbalimbali mkoani Morogoro ikiwamo Magereza, kwenye kituo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na kwenye misikiti ambayo ilikuwa na shida ya maji.

Balozi Albahry alisema kuwa UAE AID pia inasaidia kuwasomesha watoto zaidi ya 500 wanaotoka kwenye familia duni kwa kuwagharamia karo, sare za shule na vifaa.

Mwenyekiti wa taasisi ya the Islamic Foundation, Aref Nahdi, alisema taasisi hiyo imekuwa ikisimamia na kuratibu miradi mbalimbali inayotolewa na UEA.

Nahdi alitaja vyakula walivyotoa msaada kuwa ni unga wa ngano, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na maharage ambavyo vyote vina jumla ya tani 29.

## Ndege yatua kwa dharura bila matairi

**NAYPYIDAW,** Myanmar

RUBANI mmoja raia wa Myanmar alilazimika kutua bila gurudumu la mbele baada ya ndege kupata hitilafu ya kiufundi wakati wa kutua.

Ndege hiyo ya shirika la ndege la Myanmar iliteleza kwa muda katika barabara ya ndege kabla ya kusimama katika uwanja wa ndege wa Mandalay.

Rubani wa ndege hiyo aina ya Embraer 190 alisifiwa kwa kutua salama na abiria wote 89 bila hata mmoja wao kujeruhiwa. Kapteni Myat Moe Aung alizunguka uwanja wa ndege mara mbili ili kuwapa muda waelekezaji wa ndege kubaini ikiwa kifaa hicho kingeliweza kufanya kazi, ilisema shirika hilo la ndege.

Ndege hiyo iliyokuwa safarini kutoka Yangon na ilitakiwa kutua katika uwanja wa ndege wa Mandalay, lakini rubani alipojaribu kutua alishindwa kufanya hivyo kutokana na sababu za kiufundi. Rubani alifuata taratibu zote za kiusalama ikiwa ni pamoja na kumwaga mafuta zaidi ili kupunguza uzani wa ndege, ilisema shirika hilo la ndege.

Kanda ya video ilionesha ndege hiyo ilivyotua kwa matairi ya nyuma kabla ya pua kugonga chini. Ndege hiyo iliteleza katika barabara ya ndege kwa sekunde 25 kabla ya kusimama. **BBC**

# Wakenya wamtafuta rais wao mtandaoni

**NAIROBI,** Kenya

KATIKA hali isiyo ya kawaida, idadi kubwa ya wananchi wa Kenya wametumia mtandao wa kijamii wa Twitter kuuliza maswali kuhusu mahali aliko Rais wao, Uhuru Kenyatta, baada ya kutoonekana hadharani tangu Aprili 23.

Rais Kenyatta aliondoka nchini humo Aprili 23, mwaka huu kwenda China kukutana na Rais mwenzake, Xi Jinping na inasadikiwa kuwa alirejea nyumbani kimya kimya Mei 3. Kwa mujibu wa gazeti la The Standard.

Kutoonekana hadharani kwa Rais Kenyatta kumezua gumzo katika mitandao ya kijamii, huku wanasiasa wakitoa sababu tofauti kwa nini wanadhani rais ameamua kuwa kimya.

Msemaji wa Ikulu ya Kenya, Kanze Dena aliwajibu Wakenya wanaomuulizia Rais Kenyatta kwamba kiongozi wa nchi yuko ofisini na kuongeza kuwa yuko ana majukumu mengi ya kikazi.

Dena aliwajibu Wakenya waliyoanzisha kampeni ya kumtafuta rais Kenyatta, kwa kusema kuwa kutoonekana hadharani kwa rais hakumaanishi hajulikani aliko.

**Nashagaa kusikia kuwa watu wanasema hawajamuona rais tangu arejee nchini kutoka China, wakati rais amefanya mkutano na wakuu wa hazina ya Global Fund na kumekuwa na taarifa kuhusiana na mkutano huo.**

"Nashagaa kusikia kuwa watu wanasema hawajamuona rais tangu arejee nchini kutoka China, wakati rais amefanya mkutano na wakuu wa hazina ya Global Fund na kumekuwa na taarifa kuhusiana na mkutano huo," alisema Dena.

Akizungumza na kituo kimoja cha radio nchini humo, Dena alithibitisha kuwa Rais Kenyatta ni mzima wa afya na kwamba hakuna haja ya watu kuwa na hofu kwa sababu amepunguza mikutano yake ya hadhara.

Hata hivyo, kupitia 'hashtag' ya #FindPresidentUhuru, Wakenya katika mtando wa kijamii wa Twitter maarufu KOT walituma ujumbe wa kutaka kujua Rais Kenyatta yuko wapi.

Gavana wa jimbo la Machakos lililopo nje kidogo ya mji mkuu wa Nairobi, Dk. Alfred Mutua alinukuliwa na vyombo vya habari akimtetea rais kwa kutoonekana hadharani kwa mda.

"Rais ni meneja mwenye shughuli nyingi kwa hiyo anahitaji muda wa kufanya mikutano, kupokea taarifa muhimu za serikali na kushughulikia masuala ya uchumi wa nchi" alisema Mutua.

Aliongeza kuwa anashangaa kusikia watu wakiulizia kwa nini rais hajaonekana hadharani tangu arejee kutoka ziara ya China.

Baadhi ya wananchi waliandika: "Rais Kenyatta alifuta akaunti zake rasmi za mitandao ya kijamii na kisha akaelekea ziara ya China kutafuta mkopo. Hivyo ndivyo rais wetu alivyotoweka! Yuko wapi Uhuru Kenyatta?" walimalizia kwa kuuliza swali hilo.

Licha ya hashtag ya #FindPresidentUhuru, kusambaa katika mitandao ya kijamii kuanzia siku ya Jumamosi, kitengo cha mawasiliano cha Rais Kenyatta hakijatoa tamko lolote.

Hashtag zinazohusiana na masuala ya kisiasa sio maarufu kuliko masuala mengine ya kijamii, lakini hashtag ya #Kenya@50 ilitajwa kuwa miongoni mwa hashatag maarufu za kisiasa barani Afrika. **BBC**



Wanachama wa chama cha ANC Afrika Kusini, wakishangilia ushindi baada ya chama chao kutangazwa mshindi kwa kupata asilimia 57 ya kura zilizopigwa. **PICHA: ANC**

# ANC yasheherekea ushindi, yapata viti vichache bungeni

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MAELFU ya wafuasi wa chama tawala cha Afrika Kusini cha ANC wamekuwa wakisherehekea ushindi wa chama chao katika mji wa Johannesburg, licha ya kwamba chama hicho kimepata idadi ndogo ya viti katika bunge la taifa.

Kwenye uchaguzi huo, ANC kimepata ushindi kwa asilimia 57 za kura zilizopigwa. Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wamesema kutokana na hali hiyo inabidi chama hicho kikongwe cha Afrika kutafakari mikakati na majukumu yake ya siku zijazo, hasa kutokana na kuongezeka kwa ushindani mkubwa kutoka kwa vyama vya upinzani.

"Ni mchanganyiko wa ujumbe, lakini tukiangalia kwa usawa kwa haki ANC imepata asilimia 58 baada ya miaka 25 madarakani, marais watano na uchaguzi wa sita. Sio mbaya sana lakini pengine ingekuwa mbaya zaidi,"

"Lakini kwa ujumla ninadhani ukweli ni kwamba chama cha upinzani EFF kimeongeza karibu nusu ya kura zake na ni chama ambacho wapiga kura wake wengi wametoka ANC, kwa maoni yangu ninadhani huo ndio ujumbe muhimu kwa ANC, kwamba inahitaji kujipanga upya, kujitathmini na kushughulikia maslahi na mahitaji ya wa Afrika Kusini wote kwa ujumla". Alisema Otieno mmoja wa wachambuzi wa masuala ya kisiasa nchini Afrika Kusini.

Viti vya ANC bungeni vimepungua kutoka 249 mpaka 230. Chama cha upinzani cha Democratic Alliance nacho kimeshuhudia viti vyake vikipungua kutoka 89 mpaka 84 huku chama kingine cha upinzani EFF kinachoongozwa na Julius Malema kikiongeza viti vyake kutoka 19 mpaka 44. **VOA**

# Serikali yabanwa usajili laini za simu kwa vidole

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imeliomba Bunge liipe kipindi cha mwezi mmoja kuangalia uwezekano wa kuruhusu vitambulisho vingine, tofauti na kitambulisho cha uraia, kutumika katika usajili mpya wa laini za simu.

Waziri katika wizara hiyo Isack Kamwelwe, jana jioni alimwomba Spika Job Ndugai ampe kipindi cha mwezi mmoja kujadiliana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) kuangalia uwezekano wa kuruhusu wananchi kusajili laini kwa vitambulisho tofauti na cha uraia.

Kamwelwe aliomba muda huo baada ya Mbunge wa Welezo, Saada Mkuya Salum (CCM), kushika shilingi yake wakati wa kupitisha mafungu ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, akieleza kuwa jana mchana alikwenda kusajili laini kwa utaratibu mpya kwenye viunga vya Bunge lakini kazuiwa kutumia kitambulisho cha mkaazi wa Zanzibar.

Mbunge huyo aliliambia Bunge kuwa alielezwa na wanaosajili laini bungeni kuwa kitambulisho kinachohitajika ni cha uraia wa Tanzania kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (Nida).

**LAINI MOJA KWA MTANDAO**

Awali wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo jana asubuhi, Mbunge wa Mpendae, Salimu Hassan Turky (CCM), alitahadharisha kuwa masharti ya kutaka kila mtu amiliki laini moja ya simu, yatafifisha uchumi wa nchi.

Mbunge huyo alisema: "Mheshimiwa Spika, Rais wetu John Magufuli anataka nchi ikue kiuchumi, lakini mnakuja na mawazo ya kudumaza uchumi kwamba mtu mmoja awe na laini moja ya simu au akitaka ya pili apate kibali, vitu hivi vya ajabu vinatoka wapi?

"Huu uchumi tulio nao, leo tunao 'mobile operators' karibu watano, sita na kila mmoja anataka aingie sokoni. Sasa kama mlitaka hivi, kwa nini muwape leseni hawa operators wote? Hivi hapa kuna agenda gani? Au mnataka kumpandisha mtu mmoja? Kama mlikuwa na ajenda hiyo, kwanini mlitoa leseni kwa wote hao?

"Kwanini mnatubana tusiwe na simu? Leo mimi nataka simu ya jimboni kwangu, simu ya ofisi yangu, uchumi huu unatakiwa ukue kwa kasi, simu zingine mie napokea za nje tu itakuwaje?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu hoja hiyo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, alisema utaratibu mpya wa usajili wa laini za simu kwa kutumia vitambulisho vya Nida unataka kila mtu kusajili laini moja kwa kila mtandao.

Alisema lengo ni kudhibiti matumizi ya mtandao kwa njia ya simu, akisisitiza kuwa ni vigumu kumzuia mtu kujipiga picha chumbani kwake, lakini picha hiyo chafu ikitoka chumbani na kusambaa mitaani, atashughulikiwa na vyombo vya dola kwa matumizi mabaya ya mtandao.




Mkurugenzi Mtendaji wa Songas, Nigel Whittaker, akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 47 kwa wanafunzi wa Ubungo Kisiwani jana. Kampuni hiyo ya uzalishaji wa gesi imetoa msada huo kama mchango wao katika kuisaidia serikali kuboresha miundombinu ya elimu nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Chui aibua hofu wakazi Dar

**Na Romana Mallya**

WANANCHI wa maeneo ya Goba jijini Dar es Salaam, wamekumbwa na hofu ya usalama wa maisha yao baada ya kuzagaa kwa habari za kuonekana chui eneo la Zone C maarufu kwa Prof. Msanjila.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Musa Taibu, alithibitisha jana kuwapo kwa chui huyo na kwamba wanawatafuta maofisa wanyamapori kwa ajili ya ufuatiliaji zaidi.

"Ni kweli tumesikia kuwa huko Goba kuna chui ameonekana, taarifa hizi nimezipata baada ya DC (Mkuu wa Wilaya Kinondoni) kunipigia simu dakika kumi zilizopita kunijulisha ili hatua ziweze kuchukuliwa, kwa sasa tunawasiliana na maofisa wanyamapori," alisema.

Kamanda Taibu alisema endapo watakawakosa maofisa wanyamapori, Jeshi la Polisi litakwenda ili kuhakikisha hali ya usalama eneo hilo inaimarika.

Taarifa iliyopo mtandaoni iliwataarifu wananchi wa Kibululu Goba kuwa Ofisi ya Serikali ya Mtaa imewataka wachukue tahadhari kwa sababu kuna chui ameonekana maeneo ya Zone C.

"Habari zenu ndugu wajumbe, taarifa kwa wana Kibululu, Ofisi ya Serikali ya Mtaa inapenda kuwataarifu wananchi wote kuwa kuna chui ameonekana maeneo ya Zone C Kwa Prof. Msanjila, hivyo tuwe na tahadhari wakati tunawasubiri mamlaka husika kufika na kuchukua hatua za haraka," ulisema ujumbe huo

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa Kibululu, Goba ni maeneo ya Stanza, shule ya Precious kutokea Makongo.

Mkurugenzi wa Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Maurus Msuha, alisema wanatuma watu eneo hilo ili kumkamata chui huyo.

# Balozi Iddi aagiza vibali vya mchanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameiagiza Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na kamati maalum inayosimamia rasilimali ya mchanga kutoa kibali cha upatikanaji wa mchanga kwa miradi mikubwa ya Serikali.

Amesema lengo ni kuepusha kukwama kwa utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema haitapendeza ufikie wakati kuwanyooshea vidole wahandisi wa kampuni ya ujenzi wa miradi mikubwa kwa madai ya kuchelewesha kazi waliyopewa wakati baadhi yao wameshatoa taarifa ya kukumbwa na changamoto ya upatikanaji wa mchanga kwa wakati.

Balozi Iddi alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya kutembelea ujenzi wa miundombinu ya madaraja, mitaro ya maji ya mvua pamoja na kukagua maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko ya mvua za masika zinazoendelea.

Pia alikwenda kuwafariji wananchi waliopatwa na athari hizo katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema upo urasimu unaofanywa na baadhi ya wasimamizi wa utoaji wa vibali vya rasilimali ya mchanga, na kuwa zipo dalili zinazoanza kuonekana za kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya miradi ambayo ni muhimu kwa taifa na wananchi.

Alisema kazi kubwa iliyofanywa na wahandisi wa makampuni yanayojenga madaraja ya Kibonde Mzungu na Mwanakwerekwe imeleta faraja kubwa kwa taifa na wananchi wengi.

Balozi Iddi alisema changamoto ya kujaa kwa maji katika madaraja hayo inaanza kuwa historia kwa vile licha ya kutokukamilika rasmi kwa ujenzi wake, lakini wananchi wapitao kwenye madaraja hayo hivi sasa wanaendelea na harakati zao kama kawaida katika maeneo ambayo ilikuwa mwiko kupita katika kipindi hiki.

Akitoa pole kwa wananchi walioathiriwa na mafuriko kutokana na makazi yao kujaa maji katika maeneo ya Mwanakwerekwe, Kwamtumwa Jeni, Sebleni na Jong'ombe, Balozi Iddi aliwanasihi kuwa na utamaduni wa kutupa taka katika sehemu maalum zilizotengwa.

Alisema Serikali imekuwa ikichukua jitihada kubwa za kujenga miundombinu ya mitaro ya maji ya mvua, lakini wapo watu wasiozingatia jitihada hizo, jambo ambalo linarejesha nyuma utekelezaji wa mipango ya kuwahudumia katika kuimarisha ustawi wao.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wa maeneo yanayopitishwa ujenzi wa mitaro mipya ya maji ya mvua kuwa na subira katika kipindi hichi cha mpito cha ujenzi unaoendelea kwa kuwa ukamilikaji wa miradi hiyo utaleta faraja ya kudumu hapo baadae.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**


**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA


## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya tarehe 14/05/2019 hadi 25.05.2019 kampuni ya **TANZANIA STEEL PIPES LTD** inategemea kusafirisha mizigo yake ( Machine Goods) yenye vipimo vikubwa Kutoka **NAMANGA kuja DAR ES SALAAM , Gari hizo lenye namba za usajili:**
   - **I) KCG 385Y/ZF 4413**
   - **II) KBV 128J/ZB 4979**
2. Gari tajwaa zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 17**
   **Upana - mita 3.0**
   **Kimo - mita 3.5**
3. Njia itakayotumika ni kutoka NAMANGA hadi DAR ES SALAAM.gari litasafiri muda wa mchana tu(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115224702

## KUPOTEA KWA VYETI



**Bimkubwa Hamad Said** anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne vifuatavyo : index namba **P.030-0005,** kilichotolewa na shule ya Sekondari Fidel Castro mwaka 2007, na cheti chenye index namba **P.1304-0015** kilichotolewa na Shule ya Sekondari Chanja Mjawiri mwaka 2003. Yeyote atakeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa : **OCHKA/A.16/VOL.IV/1676/2019**

115224902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Jemima Njunde** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4506-0069** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika shule ya sekondari Makurumla. Yeyote atakaeiona ator taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/256/2019**

115224602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIAS K. MBAPILA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SUZUKI CARRY YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.569 CEF** RANGI NYEUPE CHASSIS NAMBA **DC51T534200** ENGINE NAMBA **F6AEAA4200.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **SMT/RB/6024/2019**

215225002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Zaina Hussein Nyagongo** anatangaza kupotelewa kawa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T265 DCG** aina ya **TOYOTA NOAH** yenye chasis namba **SR400178812,** Engine namba **3S4752812.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KJN/RB/6529/2019**

115225302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;107/2019**

**Ombi la AHMADI RAMADHANI SIMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI FUNDI SIMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/05/2019.



215225402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;104/2019**

**Ombi la AMIR SALUM SAID Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALUM SAID AMER**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/05/2019.



215225502


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# TOURE AKANUSHA KUSTAAFU SOKA

**LONDON,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester City na Barcelona, Yaya Toure amekanusha kwamba amestaafu soka licha ya wakala wake kudai kwamba kiungo huyo ameamua kutundika daluga rasmi.

Wiki iliyopita, wakala wa mchezaji huyo, Dimitry Seluk, alisema kwamba Toure amestaafu kucheza soka na kwa sasa mipango yake ni kuingia katika ukocha, lakini taarifa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, imekanusha.

"Kumekuwa na mkanganyiko kuhusu majaliwa yangu," aliandika Toure kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Nataka kuweka wazi kwamba, napenda soka na bado nina nia ya kuendelea kucheza kwa miaka kadhaa ijayo.

Toure amekuwa mchezaji huru tangu alipoondoka katika Klabu ya Olympiakos ya Ugiriki alikocheza kwa miezi mitatu mwaka jana.

"Na wala msihofu muda ukifika nitatangaza rasmi kwamba ninaachana na soka na nitatangaza mimi mwenyewe."

Toure alifurahia kipindi kizuri cha uchezaji wakati alipotwaa mara mbili ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barca kabla ya kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu ya England na moja la Ligi na lile la FA akiwa na Man City.

# Man United yataka kusajili beki Juventus

**ROME,** Italia

KLABU ya Manchester United imetuma maombi ya kumsajili beki wa Juventus, Joao Cancelo, lakini italazimika kuwatoka pauni milioni 51.

Mabingwa hao wa Italia wamesema hawawezi kumpiga bei beki huyo wa kulia kwa fedha chini ya kiwango hicho katika usajili wa majira ya kiangazi.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer anataka kujenga upya kikosi chake katika usajili ambao utamfanya kupangua kikosi.

Solskjaer anataka kujenga timu imara na ameamua kuanza na kuimarisha ngome yake kwa kumsajili Cancelo.

Nafasi ya beki wa kulia Man United inachezwa na Ashley Young ambaye alimpoka namba Antonio Valencia.

Wachezaji wote wawili walipelekwa kucheza nafasi ya beki wakitokea katika nafasi za viungo wa pembeni.




# Solskjaer: Nitaifumua upya Manchester United



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amedokeza mabadiliko makubwa kipindi hiki cha majira ya joto, akisema kwamba Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward na wamiliki wa klabu wanajua kwamba wanahitaji kuijenga upya timu hiyo pale Old Trafford.

United imemaliza msimu huu ikipitwa pointi 32 na mabingwa Manchester City baada ya kufungwa 2-0 nyumbani na Cardiff iliyoshuka daraja kwenye mchezo wa mwisho wa ligi hiyo juzi Jumapili.

Na hili limemuacha Solskjaer na mlima mkubwa wa kupanda kuwezesha klabu hiyo kurudi kwenye zama zake, na amesema kwamba wamiliki na bodi wanajua kazi inayotakiwa kufanyika.

"Nilikuwa na majadiliano na yamekuwa yakiendelea vizuri, tunajua wapi tulipo," alisema.

"Mwishoni mwa msimu itaonyesha wazi wapi tumefikia na kiwango tulichonacho.


"Tulicheza soka la kuvutia muda wote na kuendelea mwishoni mwa msimu kila wakati, na hata matarajio yetu yalikuwa tofauti."

Solskjaer alianza kazi ya ukocha hapo kwa ushindi wa mechi 14 kati ya 17 kwenye mashindano yote, lakini amemaliza msimu kwa ushindi wa mechi mbili kati ya 12 za mwisho.

## HABARI MICHEZO

# AUBAMEYANG, SALAH NA MANE WAGAWANA KIATU



**LONDON,** England

WACHEZAJI Sadio Mane, Pierre-Emerick Aubameyang na Mohamed Salah kila mmoja ameshinda Kiatu cha Dhahabu baada ya wote kuibuka wafungaji bora kwenye Ligi Kuu ya England.

Mabao mawili aliyofunga Aubameyang katika mechi ya Arsenal dhidi ya Burnley yamemaanisha kujiunga na Salah na mchezaji mwenzake wa Liverpool, Mane aliyeifunga Wolves mara mbili juzi na wote kila mmoja kufikisha mabao 22.

Hii ni mara ya kwanza kwa wachezaji zaidi ya mmoja kushinda tuzo hiyo tangu msimu wa 2010-11, wakati Dimitar Berbatov na Carlos Tevez waliposhinda pamoja tuzo hiyo.

Aubameyang mchezaji wa kimataifa wa Gabon aliyefunga mara mbili baada ya kipindi cha mapumziko huko kwenye Uwanja Turf Moor, alisema: “Napokea taji hili na wachezaji wengine wawili ninaowapenda, wachezaji bora na Waafrika. Tunaiwakilisha Afrika, ni vizuri.

“Ninafurahi tumeshinda, na napokea tuzo hii na watu ninaowapenda. Wachezaji wenzangu walijua kuhusu tuzo hii. Mimi sikusema kitu. Sikutaka wacheze wakinilenga mimi. Mimi napenda kushirikiana na wenzangu.”

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ameeleza mshtuko na furaha kwa mchezaji huyo wa zamani wa Dortmund aliyemsajili kutoka Saint-Etienne mnamo mwaka 2013, alipokuwa anakiongoza kikosi hicho pale Westfalenstadion.

“Auba pia? Wapewa tuzo tatu? Ni vizuri. Wote ni wachezaji wangu,” alisema.

Salah, mwenye umri wa miaka 26, amefunga mabao 32 msimu uliopita. Idadi hiyo ni rekodi ya mabao mengi zaidi katika kampeni ya mechi 38.

Amekuwa mchezaji wa sita kushinda taji hilo katika misimu inayofuatana.

Harry Kane wa Tottenham mchezaji wa mwisho kulitwaa taji hilo la Ligi Kuu England baada ya kulishinda msimu wa 2015-16 na 2016-17, alimaliza kwa mabao 17 baada ya kuwa majeruhi.

# *Brighton yaamua kumtimua Hughton*



**LONDON,** England

KLABU ya Brighton imetangaza kumfukuza kazi kocha wake, Chris Hughton baada ya miaka minne na nusu katika klabu hiyo.

Hughton alijiunga na klabu hiyo mwaka 2014 na wakaweza kupanda kucheza Ligi Kuu mwaka 2017, ikiwa ni mara ya kwanza kucheza kwenye Ligi kubwa tangu mwaka 1983.

Hata hivyo, kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, aliiongoza kwa mafanikio kikosi hicho kutoshuka daraja msimu huu.

Katika taarifa rasmi ya klabu hiyo ilibainisha kwamba: “Brighton & Hove Albion inathibitisha kwamba, Chris Hughton ameondoka klabuni.

“Pia msaidizi wa Hughton, Paul Trollope na kocha wa kikosi cha kwanza, Paul Nevin ameondoka.”

Baada ya tangazo hilo Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Tony Bloom alibainisha: “Chris alifanya kazi nzuri na sisi kwa kipindi cha miaka minne na nusu iliyopita.

“Kwanza kuiwezesha klabu yake kuwa imara, na kufuzu kucheza Ligi Kuu na kuendelea kubakia kwenye ligi hiyo kwa misimu miwili mfululizo.”

# Hazard afunguka kuondoka

**LONDON,** England

NYOTA wa Chelsea, Eden Hazard, amebainisha kwamba aliiambia klabu yake mpango wake wa kuondoka na kwenda Real Madrid wiki kadhaa zilizopita, lakini bado anasubiria mpango huo kufikia makubaliano.

Msimu wa Ligi Kuu ya England ulimalizika Jumapili wakati wakitoka sare ya bila kufungana na Leicester City, na Hazard sasa ataingia mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake kipindi cha majira ya joto na anaweza kuondoka akiwa huru msimu ujao.

Akizungumza na Gazeti la Daily Mail baada ya mchezo huo wa mwisho, Hazard alikiri kwamba tayari alishazungumza na maofisa wa Chelsea kuhusu mpango wake wa kutaka kuondoka.

Alisema: “Nimeshafanya maamuzi, lakini sio peke yangu. Niliiambia klabu wiki kadhaa zilizopita. Nilitaka kubainisha wazi, lakini hilo halikutokea. Bado nasubiri kama mashabiki wanavyosubiri.

“Tumecheza mchezo wetu wa mwisho na nitaona nini kitatokea. Hakujakuwa na muingiliano wowote. Wakati unapokuwa uwanjani, akili yao inakuwa kwenye kucheza soka tu.

“Wakati nikiwa uwanjani najaribu kuonyesha uwezo wangu kadri niwezavyo. Sifikirii kuhusu hili na hali yangu au klabu nyingine. Ninachokuwa akilini mwangu ni kushinda mchezo.”

Kumekuwa na uvumi wa muda mrefu kwamba, Hazard atakuwa wa Real Madrid.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: UBINGWA WA EPL MGUMU SANA

## Tunapaswa kusema hongera kwa Liverpool, bila shaka, na asanteni sana...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola ameishukuru Liverpool kwa kutoa msukumo kwa Manchester City kuifikia kabla ya kuipiku kwa pointi hata alipodhani ilikuwa vigumu kutetea ubingwa wao, lakini pia akifafanua kwamba katika maisha yake kama kocha hajawahi kutwaa ubingwa kwa tabu namna hii.

**Man City ilitokea nyuma ugenini dhidi ya Brighton na kufanikisha ushindi wa 14 mfululizo, ambao uliwawezesha kuhitimisha msimu wakaiwa na pointi 98, hivyo kuwa timu ya kwanza kutetea ubingwa wa EPL tangu mwaka 2009.**

Liverpool ilikuwa katika mbio za kutwaa ubingwa huo kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 29, lakini ikajikuta ikimaliza pointi moja nyuma ya mabingwa Man City, lakini Guardiola aliwapigia saluti 'Wekundu' hao kwa kutoa changamoto kubwa kwake ya kutwaa ubingwa katika historia ya wasifu wake kisoka.

"Kwanza kabisa, tunapaswa kusema hongera kwa Liverpool, bila shaka, na asanteni sana," Kocha huyo wa City aliiambia Sky Sports.

"Walitusaidia kutoa msukumo kwetu na kuongeza ubora wetu wa msimu uliopita kwa sababu kushindana dhidi ya timu hii inatusukuma kufanya tulichokifanya.

"Ni ajabu, pointi 198 katika misimu miwili kushinda mfululizo. Tumeweka ubora wa hali ya juu msimu uliopita na Liverpool imesaidia kuwa pale wakati wote. "Kutwaa kombe hili tulipaswa kushinda mechi 14 mfululizo. Tulijua kwa miezi miwili ama mitatu tusingeweza kupoteza pointi moja. Hili lilikuwa kombe gumu zaidi tuliloshinda katika wasifu wangu kisoka hadi kufikia sasa."

Hii ni mara ya nane ubingwa wa EPL kuamuliwa siku ya mwisho wa msimu, na Manchester City ikishinda mara tatu kati ya hizo (msimu wa 2011-12, 2013-14 na 2018-19).

Ma City bado ina nafasi ya kubeba 'ndoo' nyingine ya ndani kama Jumamosi itaichapa Watford kwenye fainali ya Kombe la FA.

Guardiola amesisitiza kuwa ni juhudi za pamoja za kikosi chake, na si kwa mchezaji mmoja mmoja, ndicho kitu kilichoiwezesha City kutawala, na akaonya kuwa mabingwa hao watarejea na nguvu zaidi msimu ujao.

"Tumetwaa Ngao ya Jamii, Kombe la Ligi ['Carabao Cup'], EPL na tupo katika fainali ya Kombe la FA Cup," Mhispania huyo aliongeza.

"Hatuna mchezaji mmoja ambaye anaweza kuleta tofauti, tunapaswa kufanya hili kama timu. Hiyo ndiyo siri.

"Tunatoa msukum kowa kila mmoja, ninatoa msukumo kwao, na wanatoa msukumo kwangu na uongozi.

"Unaweza kushinda [kombe] moja, hilo linaweza kutokea, lakini wakati unaposhinda mawili mfululizo katika ligi hii dhidi ya makocha wa kushangaza na klabu zinazowekeza fedha nyingi, inamaana umefanya vizuri sana. Huo ndio ukweli.

"[Msimu ujao] utakuwa mgumu, lakini tutakuwa imara pia. Nina hisia msimu ujao kuwa tutarejea na kujaribu tulipo kwa sasa."

## ZISIKUPITE

### HAZARD AFUNGUKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, 28, ameiambia klabu hiyo kuhusu uamuzi wake kujiunga na Real Madrid. ***(Daily Mail)***

### LACAZETTE APAGAWA NA BARCA

STRAIKA wa Arsenal, Alexandre Lacazette, 27, amesema alipagawa baada ya tetesi kumhusisha na Barcelona. ***(Goal)***

### COUTINHO ATEGWA CHELSEA

CHELSEA inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Philippe Coutinho, 26, kama wataweza kushinda kesi ya kufungiwa kusajili. ***(Cadena Ser via Daily Mail)***

### CARDIFF YATIBUA SOLSKJAER

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alitupilia mbali mkutano wa mwisho wa msimu kwa sababu ya kuchefuliwa na kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya washuka daraja, Cardiff juzi, Jumapili. ***(Sun)***

### POGBA, MASHABIKI WATIBUANA

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, alitibuana na mashabiki baada ya kusema anapaswa kuuzwa baada ya timu hiyo kupoteza dhidi ya Cardiff. ***(Daily Mail)***

### PELLEGRINI KUMWACHIA RICE

KOCHA wa West Ham, Manuel Pellegrini, amekiri kwamba hataweza kumbakiza kiungo wa England, Declan Rice, 20, kama timu kubwa zitataka kumnunua. (Mirror)

### EVERTON HOFU KUMKOSA GOMES

KOCHA wa Everton, Marco Silva, amesema hana uhakika kama majira haya ya joto klabu hiyo itaweza kushinda vita ya kumsajili jumla kiungo Mreno Andre Gomes, 25, anayeichezea kwa mkopo. ***(Liverpool Echo)***

### BENITEZ, NEWCASTLE KUTETA

KOCHA wa Newcastle, Rafael Benitez, atafanya mazungumzo na mmiliki wa klabu hiyo, Mike Ashley wiki ijayo kuhusu mustakabali wake wa baadaye. ***(Daily Mail)***

### ZIDANE AMWANIKA BALE

ZINEDINE Zidane amesema mustakabali wa baadaye wa Gareth Bale, 29, hapo Real Madrid "upo wazi" baada ya straika huyo wa kimataifa wa Wales kuacha kwa mara nyingine katika kikosi cha timu hiyo. ***(AS)***

### ABRAHAM AWINDWA A.VILLA

ASTON Villa itafunga safari kwenda kumsajili staika wa Chelsea na England, Tammy Abraham, 21, kwa dili la pauni milioni 25 kama itafanikiwa kurejea Ligi Kuu England, EPL. ***(Telegraph)***

### BATSHUAYI KURUDISHWA

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson amesema atakuwa ni mwenye furaha kumrejesha straika wa Chelsea, Mbelgiji Michy Batshuayi, 25, katika dimba la Selhurst Park msimu ujao. ***(Football London)***

### BUTLAND ASILIKIZIA OFA

KIPA wa England na Stoke City, Jack Butland, 26, kwa sasa anasikilizia ofa kutoka Bournemouth na Crystal Palace. ***(Stoke Sentinel)***

HABARI MICHEZO

# MATOLA: SABABU LIPULI KUCHEZEA VICHAPO HIZI

Na Mwandishi Wetu

KOCHA wa Lipuli FC, Selemani Matola, amesema uzembe na hali ya kubweteka ulioonyeshwa na mabeki wake, ndio sababu kuu ya wao kupoteza mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo sasa inaelekea ukingoni.

Kauli hiyo ya Matola, nahodha na kiungo wa zamani wa Simba na Supersport ya Afrika Kusini, ilikuja baada ya kuchapwa mabao 3-0 na Mbeya City, katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM-Samora mkoani Iringa.

Ijumaa iliyopita Lipuli ilifungwa mabao 2-0 na Ruvu Shooting ya Pwani huku pia ikichapwa mabao 3-0 na Biashara United katika mchezo mwingine wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

**Matola aliliambia gazeti hili kuwa, baada ya kumaliza mechi ya Kombe la FA dhidi ya Yanga ambapo waliibuka na ushindi, wachezaji wake walionekana "kuridhika" na kucheza soka la kiwango cha chini na hivyo kupoteza mechi hizo za Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Kocha huyo alisema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa katika mchezo huo huku pia washambuliaji wake wakionekana kukosa umakini wanapopata nafasi za kufunga na kujiweka katika nafasi mbaya.

"Wamecheza kizembe sana, kizembe kabisa, naona wamebweteka tangu tulipopata ushindi katika mechi dhidi ya Yanga, nimeliona hili, tutalifanyia kazi ili turudi katika ubora wetu, bado ligi haijamalizika, tunahitaji kupata ushindi katika mechi zilizobaki," alisema Matola.

Lipuli FC imecheza mechi 35 na ina pointi 48 wakati katika msimamo wa ligi hiyo ambayo Simba ndio bingwa mtetezi, tayari African Lyon ya jijini Dar es Salaam yenye pointi 22 imeshashuka daraja.

Lakini pia Simba na Yanga ndizo zimebakia katika mbio za kuwania ubingwa ili kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwakani.



Mshambuliaji wa KRC Genk, Mtanzania Mbwana Samatta akiwatoka mabeki wa Club Brugge katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza A Ubelgiji iliyopigwa Uwanja wa Jan Breydel mjini Brugge juzi. Genk ilifungwa 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# Alliance yahofia Biashara kuihujumu

Na Mwandishi Wetu

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa inaelekea ukingoni, uongozi wa Alliance FC umeitaka Bodi ya Ligi kuhakikisha mechi yao dhidi ya Biashara United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma inaonyeshwa mubashara.

Biashara United ambao ni wenyeji na wamecheza mechi 34 wana pointi 40 na Alliance FC kutoka jijini Mwanza wao wana pointi 41, lakini wameshuka dimbani mara 35.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Alliance FC, Yusufu Budodi, alisema wameomba mchezo huo urushwe hewani mubashara kwa sababu wanaamini itasaidia kupunguza vitendo vya uonevu ambavyo vimekuwa vikijitokeza katika uwanja huo.

Budodi alisema wanaifahamu vema Biashara United na wangependa kuona timu inayostahili inapata pointi zake kihalali katika mechi hiyo.

"Tunajuana vema, pale Musoma pamekuwa na historia ya vurugu, ni vizuri mchezo wetu ukaonyeshwa "live", hii itawafanya wale wenye nia mbaya wakaacha kwa sababu watajua wataonekana," alisema kiongozi huyo.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura, alisema ofisi yake haijapokea barua yoyote kutoka kwa Alliance FC, lakini inafanya kazi kwa weledi kuhakikisha mechi zote zinachezeshwa kwa haki.

Wambura alisema kuwa bodi inatuma wasimamizi mbalimbali wanaojulikana na wasiojulikana katika mechi zote zilizobaki na kuwaondoa hofu wadau ambao wana wasiwasi na hali ya upangaji matokeo.

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19, inatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28, mwaka huu na msimu huu utafungwa kwa mchezo wa fainali ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa Juni Mosi kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi kwa kuwakutanisha Azam FC na Lipuli FC.

## Kamati ya Ligi ZFA yaishukia Gulioni FC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya kusimamia Ligi na Mashindano ya Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), imewapiga faini ya Sh. 500,000 timu ya Gulioni FC inayoshiriki Ligi Daraja la Pili Taifa kwa kuonyesha vitendo vya utovu wa nidhamu.

Hayo yamebainishwa na Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hussein Ahmada wakati akizungumza na mwandishi wetu ofisini kwake, Amaan ambapo alisema timu hiyo inadaiwa kufanya vurugu katika mchezo wao wa mwisho wa kumalizia ligi hiyo walipocheza dhidi ya Bweleo.

Katika mchezo huo, miamba hiyo ilishuka uwanjani hapo kutafuta tiketi ya kupanda daraja ili mwakani kucheza Ligi Daraja la Kwanza Taifa ambapo matokeo ya mchezo huo yalikuwa sare tasa, hivyo Bweleo Worious kupanda rasmi daraja.

Bweleo ilishuka uwanjani hapo ikiwa na pointi tisa na Gulioni iliyokuwa na pointi sita ilitakiwa kushinda kwa zaidi ya mabao matatu ili kupanda daraja.

Kufatia matokeo hayo ya kutokufungana na Gulioni kukosa nafasi ya kupanda daraja, ndipo ilipodaiwa kuanza kufanya vurugu na kamati hiyo baada kujiridhisha kwa kupitia ripoti ya mwamuzi ikaamua kuwapiga faini hiyo ambayo imetakiwa hadi Mei 25, mwaka huu iwe imelipwa.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 33 | 26 | 4 | 3 | 69 | 14 | 82 |
| 2. Yanga | 35 | 25 | 5 | 5 | 54 | 25 | 80 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Mtibwa Sugar | 35 | 14 | 7 | 14 | 36 | 29 | 49 |
| 5. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 6. Kinondoni MC | 35 | 10 | 16 | 9 | 35 | 25 | 46 |
| 7. Singida United | 35 | 11 | 11 | 13 | 28 | 35 | 44 |
| 8. Ndanda | 34 | 11 | 11 | 12 | 22 | 31 | 44 |
| 9. Coastal Union | 35 | 10 | 14 | 11 | 31 | 41 | 44 |
| 10. Tanzania Prisons | 35 | 10 | 13 | 12 | 27 | 28 | 43 |
| 11. Kagera Sugar | 35 | 10 | 13 | 12 | 31 | 37 | 43 |
| 12. Mbao | 35 | 11 | 10 | 14 | 23 | 35 | 43 |
| 13. Ruvu Shooting | 35 | 10 | 12 | 13 | 33 | 40 | 42 |
| 14. Alliance | 35 | 10 | 11 | 14 | 28 | 38 | 41 |
| 15. Stand United | 35 | 11 | 8 | 16 | 33 | 44 | 41 |
| 16. Mbeya City | 34 | 12 | 7 | 15 | 35 | 36 | 43 |
| 17. Biashara United | 34 | 10 | 10 | 14 | 26 | 31 | 40 |
| 18. JKT Tanzania | 35 | 9 | 13 | 13 | 22 | 32 | 40 |
| 19. Mwadui | 35 | 10 | 7 | 18 | 38 | 48 | 37 |
| 20. African Lyon | 34 | 4 | 10 | 20 | 21 | 46 | 22 |

# Michezo



Jumanne Mei 14, 2019
Nipashe

**Man United yataka kusajili beki Juve** HABARI UK.28



Wachezaji wa Manchester City, wakisherehekea ubingwa kwa kumpongeza Kocha wao, Pep Guardiola, kwa kumrusha juu baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England juzi kufuatia kuifunga Brighton nyumbani mabao 4-1 kwenye mechi yao ya funga msimu juzi. **HABARI UK. 30**

# Simba yaipa nafasi Yanga

## ●●● Azam yaitibulia, ubingwa sasa shughuli pevu, vijana wa Zahera kurejea kileleni leo endapo...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wameshindwa kuendeleza kipigo dhidi ya Azam FC kwenye mechi yao ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo baada ya kulazimishwa sare tasa katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana na hivyo kutoa nafasi kwa watani zao, Yanga kurejea kileleni leo.

**Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyopigwa uwanjani hapo, mwezi uliopita, Simba ilishinda 3-1, matokeo ambayo yaliukera uongozi wa Azam na hivyo kuamua kumtimua Kocha Mkuu, Mholanzi Hans van der Pluijm pamoja na msaidizi wake, Juma Mwambusi.**

Kwa matokeo hayo ya jana, yanaifanya Simba kufikisha pointi 82 baada ya mechi 33, wakati Yanga yenye alama 80 zilizotokana na michezo 35, inaweza kurejea kileleni mwa ligi hiyo endapo itaibuka na ushindi dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Uhuru leo.

Lakini huenda ikakumbana na upinzani mkali kutoka kwa Ruvu Shooting inayokamata nafasi ya 13 ikiwa na pointi 42, kwani nayo inahitaji pointi tatu ili kujinasua kwenye janga la kushuka daraja, au kwenda kwenye mechi za mtoano 'play off.'

Sare hiyo kwa Simba imekuja wakati ikitoka kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar katika mechi iliyopita ambayo ilipigwa uwanjani hapo.

Hata hivyo, makocha wa timu hizo wameeleza kuwapo changamoto ya maji kwenye uwanja ambayo yametuama na kusababisha mpira wakati mwingine kukwama kutembea na kupoteza ladha ya mchezo.

Katika mchezo huo, timu zote mbili zilifanya mashambulizi kwa kupokezana, Simba wakikosa bao kipindi cha kwanza, baada ya Emmanuel Okwi kuunganisha krosi ya Nicolaus Gyan, huku Claotus Chama akigongesha mlingoti wa goli baada ya kutokea piga nikupige kwenye lango la Azam.

Azam ambayo matokeo hayo yanaifanya kufikisha alama 69 baada ya mechi 36, nayo ilipata nafasi nzuri kipindi cha kwanza kupitia kwa Donald Ngoma, aliposhindwa kuunganisha vizuri krosi kutoka kwa Bruce Kangwa, huku Obrey Chirwa akimpa mikononi kipa Aishi Manula alipobaki naye ana kwa ana kipindi cha pili.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Sokoine, wenyeji Prisons walikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya KMC kwenye mechi kali ya kusisimua.

## Zahera: Huruma sasa basi

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za kuwania ufalme wa soka nchini msimu huu zinatarajiwa kuendelea leo wakati Yanga itakapovaana na Ruvu Shooting kutoka Mlandizi, Pwani, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Yanga itamkosa beki wake wa kati, Andrew Vincent "Dante" ambaye ana kadi tatu za njano lakini nahodha wake, Ibrahim Ajibu aliyekuwa mgonjwa amerejea kikosini baada ya afya yake kuimarika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema watashuka uwanjani wakiwa hawana huruma na wapinzani wao kwa sababu wanahitaji kupata pointi zote tatu za mchezo huo.

Zahera alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo, lakini wanajua hautakuwa mwepesi kutokana na mazingira yaliyopo.

Kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema ligi yoyote inapoelekea ukingoni ushindani huongezeka huku akiitaja changamoto ya hali ya hewa ya mvua pia itachangia kupunguza ubora wa viwango vya wachezaji.

"Tumejiandaa na mechi kama vile tunavyojiandaa katika mechi nyingine, niseme tu hatuna huruma na timu yoyote iliyoko mbele yetu, tunahitaji kupata ushindi, hakuna jambo lingine," alisema kocha huyo ambaye mechi yake iliyopita alifungwa bao 1-0 na Biashara United.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema hawana hofu wala wasiwasi wowote wa kuwavaa Yanga ambao bado wana nafasi ya kuivua Simba ubingwa endapo itateleza katika michezo yake iliyobakia na wao wakishinda yote.

"Yanga inafungika, walianza kufungwa na Lipuli ambao sisi ni wababe wao, wakafungwa pia na Biashara United, njooni muone tunavyowafundisha kandanda," alitamba kiongozi huyo.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Biashara United dhidi ya Alliance FC, timu zote zikihitaji ushindi ili kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >